# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Tisa - Tarehe 13 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):-**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 396

**Tatizo la Maji *Lower Rombo***

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Tangu tupate Uhuru Wilaya ya Rombo hasa maeneo ya tambarare *(Lower Rombo)* yanakalibiliwa na matatizo makubwa ya maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuwapatia maji wananchi wa maeneo hayo hasa ikizingatiwa kuwa hakuna mabwawa ya kuhifadhia maji ya mvua na ile nia ya kutumia maji ya Chala haipo kutokana na kuwa na kina kirefu ingawa wenzetu wa Kenya wananchi wake wanaendelea kutumia maji hayo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Rombo hasa maeneo ya tambarare yanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama. Katika kutatua tatizo hilo, Serikali inatekeleza mradi wa maji katika vijiji kumi (10) kwa vijiji vya Ngoyoni, Ngareni, Shimbi Mashariki, Ushiri, Kiraeni, Msaranga, Mahorosha, Kahe, Leto na Urauri. Utekelezaji umeanza kwa vijiji vya Ushiri na Kahe ambavyo vimepata vyanzo vya maji. Ujenzi wa miundombinu ya maji kwa vijiji hivyo unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2013. Kwa vijiji vya Mahorosha, Msaranga, Kiraeni, Ngoyoni, Urauri, Ngareni na Shimbi Mashariki ambavyo havikupata vyanzo vya maji, vitapata maji kupitia bomba la *East Kilimanjaro Trunk Main* linalopeleka maji Tarakea. Aidha, kijiji cha Leto kilichobaki kitapata maji kutoka kwenye visima vitano (5) vilivyochimbwa na Bonde la Pangani kijijini hapo. Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji kwa visima hivyo wanatarajia kupatikana mwishoni mwa mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekamilisha utafiti wa awali na kuanisha maeneo saba yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa. Maeneo hayo ni kwenye makorongo ya mito ya Kikelelwa, Shia, Nalemuru, Marwe, Ungwasi, Washi na Tarakea. Kati ya Makorongo hayo saba, Wilaya kwa kushirikiana na Ofisi za Umwagiliaji Kanda ya Kaskazini watafanya usanifu wa kina kwa kuanza na makorongo ya Mto Marwe na Ungwasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chanzo cha maji cha Ziwa Chala, tayari nchi za Tanzania na Kenya zimesaini makubaliano ya usimamizi na matumizi ya maji ya Ziwa Chala mnamo tarehe 14 Februari, 2013 Mjini Kisumu. Hivyo, Serikali inatekeleza makubaliano ya nchi hizo mbili kuhusu ziwa hilo.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda sana kuishukuru Serikali kwa sababu majibu yake yanaonyesha kwamba kuna dhamira ya dhati ya kutatua tatizo la maji kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali la nyongeza, ningependa kujua, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati anazindua barabara ya Tarakea Mkuu aliahidi kwamba kabla hajamaliza kipindi chake atakuwa amewezesha ujenzi wa malambo mawili katika Jimbo la Rombo ili kutatua tatizo hili la maji. Je, ujenzi wa malambo haya utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa maji ya Ziwa Chala yanatumiwa na wenzetu wa nchi ya Kenya, je, Serikali itaanza lini mkakati ili maji yale yatumiwe pia na wananchi wa upande wa Tanzania hasa vijiji ambavyo viko ukanda wa chini wa Jimbo la Rombo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa pongezi alizozitoa, tunazipokea na tutaendelea kufanya kazi kufikisha maji mahala pote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza kuhusu ahadi ya Rais alipokuwa anazindua barabara, hilo ni agizo, tunalichukua na litatekelezwa kama alivyokuwaameagiza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, kwamba upande wa Kenya wanatumia yale maji, kwa taarifa nilizonazo mimi bado hakuna nchi kati ya hizi mbili ambazo zinatumia hilo Ziwa. Kilichofanyika ni kusaini mkataba wa makubaliano ambao ndiyo utaanisha muundo na mfumo wa kusimamia hizi rasilimali za maji na matumizi yake ambao utaonyesha ni

miradi aina gani katika nchi gani na nani asimamie. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi bado hakuna nchi ambayo inatumia rasilimali za maji hayo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Longido inapakana na Wilaya ya Rombo na Longido ni tambarare zaidi, kwa hiyo, ina matatizo ya maji zaidi ya Wilaya ya Rombo. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili la maji Longido kwa sababu limekuwa sugu na ndiyo linalodidimiza uchumi wa Wilaya ya Longido?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lipo tatizo kubwa la maji katika Wilaya ya Longido na ni kweli kabisa Mheshimiwa Laizer ameshafika ofisini kwangu na kwa Mheshimiwa Waziri na tumeahidi kwamba tutalitekeleza suala hili ikiwemo kufanyia utafiti ambao ameuwasilisha ofisini kwetu kutoa maji kwenye milima ya Meru na kuyafikisha maeneo ya Longido. Mheshimiwa Waziri ameahidi kwamba ili aweze kujifunza vizuri atatembelea Wilaya hii ya Longido na Mheshimiwa Mbunge anafahamu hilo. Kwa hiyo, tutatekeleza na kuhakikisha wananchi wanapata maji.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Tunajua Serikali inajitahidi kuhakikisha wanapeleka maji safi na salama kwa Watanzania lakini tatizo tulilonalo kubwa na Wabunge watakubaliana na mimi baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakikwamisha mipango ya Serikali kuhakikisha miradi ya maji inakamilika kwa muda unaotakiwa na wengine wamekuwa wakiharibu katika Halmashauri zingine lakini wamekuwa wakipewa *tender* kwenye Halmashauri zingine. Sasa nataka kujua Serikali inachukua hatua gani kwa wakandarasi ambao hawafanyi kazi kama inavyotakiwa na kumaliza miradi kwa wakati waliopangiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane na yeye kwamba ni kweli wapo wakandarasi

ambao wamekuwa wakichelewesha miradi hii na imekuwa ikisuasua maeneo mengi. Niseme kwamba suala la utekelezaji wa miradi hii linasimamiwa na wadau wengi tuko Wizara ya Maji, TAMISEMI na Halmashauri. Kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ni kufuatilia ile mikataba ambayo inakuwa imeingiwa kati ya mkandarasi na Halmashauri na pale kwenye mkataba kuna vipengele vinavyoonyesha kwamba mkandarasi kama akiwa amekiuka anapewa onyo au ananyang'anywa ile kazi kama ambavyo mmekuwa mkishuhudia maeneo mengine. Kwa hiyo, tushirikiane kupeana taarifa ili kila mtu aweze kutekeleza pale panapomhusu na kutoa agizo linalotakiwa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii. Kwa kuwa tatizo la maji limekuwa tatizo sugu katika maeneo yote nchini na Jimboni kwangu katika vijiji vya Igagala, Kabage, Kabungu, Nyagala na maeneo ya Katuma, ni lini Serikali itatoa kauli ya kuvipelekea maji vijiji hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, hutendi haki kwa Mheshimiwa Waziri, swali lingine kabisa lakini Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu unajua mambo haya naomba ujibu, kama unajua.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, vijiji alivyovitaja, ninahakika vitakuwa ni moja kati ya vijiji vitakavyofaidika na ongezeko la fedha ambazo zimepitishwa hapa Bungeni mwezi huu wa nne. Kwa hiyo, tuwasiliane ili tuone kama vijiji hivi vipo na kama havipo basi maana yake vitatekelezwa kwenye awamu inayofuata.

Na. 397

## Taa za Barabarani Mjini Dodoma

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Kwa kuzingatia umuhimu wa maendeleo ya Mji Mkuu wa Tanzania, taa za barabarani ziliwekwa mjini Dodoma:

(a) Je, kwa nini ndani ya kipindi kisichozidi mwaka mmoja taa hizo haziwaki tena?

(b) Ni lini taa hizo zitawaka tena Dodoma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahimu Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli katika kipindi kifupi baada ya taa za barabarani kuwekwa hazikuwaka, hii ilitokana na Kampuni ya *A1 Outdoor (T) Limited* iliyoingia mkataba na Manispaa ya Dodoma kushindwa kutekeleza baadhi ya vipengele vilivyo ndani ya mkataba wa makubaliano ya kuweka taa za barabarani, kuziwasha, kuweka vibao vya matangazo katika barabara ya Dar es Salaam na Kiwanja cha Ndege, Arusha na Nyerere, kuzifanyia matengenezo taa zote, kuilipa *TANESCO* bili za umeme na kuilipa Manispaa Kodi ya Mapato yatokanayo na matangazo ya biashara ya asilimia 50 kwa kila tangazo la biashara lililowekwa kwenye nguzo.

(b) Mheshimiwa Spika, hivi sasa taa zinawaka karibu maeneo yote isipokuwa baadhi ya nguzo chache katika maeneo ambayo yamekamilika uwekaji wa taa hizi. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na huduma mbalimbali mijini kwa kuuweka Mji wa Dodoma katika Miji ya kimkakati Tanzania ambapo inaendelea kutekeleza mradi wa *Tanzania Strategic Cities Programme (TSCP)*. Mradi huu utajumuisha uwekaji wa taa barabani katika barabara za Mwangaza, Mwanza, Kondoa, Chamwino – Chang'ombe, Nkuhungu, Hospitali pamoja na barabara ya 11. Zoezi la uwekaji taa utagharimu jumla ya Tsh.732,780,000/-. Maeneo yote haya yote taa zitawashwa baada ya kukamilika. Pia Manispaa ya Dodoma ina mpango wa kuweka taa katika barabara toka Chuo Kikuu cha

Dodoma hadi karibu na makazi ya Waziri pamoja na barabara ya Kilimani kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo na baadhi ya makampuni yameonyesha nia ya kuweka taa hizi.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kulikuwa na mkataba baina ya hii kampuni ya *A1 Outdoor (T) Limited* pamoja na Manispaa; na kwa kuwa walihalifu ahadi hii, hatua gani zilichukuliwa kutokana na mkataba uliopo baina ya Manispaa na kampuni hii? Hilo ni swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa nchi nyingi duniani hasa Bara la Afrika sasa hivi hutumia taa zinazotokana na mwanga wa jua na kwa kuzitaja nchi chache ni Zambia, Magodishu - Somalia na Zanzibar. Je, Serikali haioni kwamba badala ya kutumia fedha hizi shilingi milioni 733/- wakaongeza kiwango cha fedha kidogo wakaweka taa zinazotumia mwanga wa jua ambao utatoa unafuu wa kulipa umeme kwa Manispaa na Halmashauri zetu ili taa hizi ziendelee katika miji yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Manispaa ya Dodoma walipoweka mkataba wa Kampuni ya *A1 Outdoor (T) Limited* imeshindwa kufanya kazi yake lakini katika mwaka wa fedha 2007/2008 na mwaka 2008/2009 kampuni hii ilikuwa inadaiwa na Manispaa ya Dodoma zaidi ya shilingi milioni 314/- kama kodi ya matangazo yake ya kibiashara. Pia Halmashauri walifungua kesi dhidi ya Kampuni hii Mahakama Kuu ya Dodoma na sasa kutokana na kesi hizi, Manispaa imeingia mkataba tena na kampuni inaitwa *Ashton Media* ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuweka taa tena na vibao vya matangazo kwenye maeneo yote lakini pia nakiri kwamba hali hii ndiyo iliyopelekea kuvunjwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kuiga nchi nyingine ambazo zimeweka taa za kutumia umeme wa jua, hili tutaliangalia tena kwenye mkataba huu wa *strategic cities* ambao pia unaendelea kwa sasa ili tuweze kuziokoa hizi fedha ambazo tunazitumia.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa taa zinazozungumzwa katika swali la msingi ni taa kwa ajili ya usalama na kupendesha mji lakini kwa kuwa mji wa Dodoma sasa unakuwa kwa kasi, magari yameongezeka sana na kuwa na taabu kubwa katika makutano ya barabara jinsi magari yanavyoweza kupishana. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuweka taa za kuongoza magari katika mji wa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi mji wa Dodoma umepanuka kwa huduma za jamii lakini pia idadi kubwa ya magari tunaanza kuona na misururu mingi, uko umuhimu wa baadhi ya maeneo yenye maunganisho kuwekwa taa za kuongoza magari. Mkakati huu Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo pia inashughulikia na uboreshaji wa miji yote Tanzania, tutaweza kuuweka katika mipango yetu ili mji wa Dodoma uwe ni miongoni mwa miji ambayo sasa inatakiwa kuwekwa taa za barabarani.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa uzoefu wangu wa kukaa hapa Dodoma, hizi taa zinazozunguka Mji wa Dodoma zinawaka wakati wa Vikao vya Bunge na wakati Viongozi Wakuu wanapokuja katika mji wa Dodoma. Sasa naomba Serikali iniambie, hizi taa zimewekwa kwa ajili ya wananchi au wakati Viongozi na Vikao vya Bunge vinavyofanyika Dodoma? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba taa hizi za hapa Dodoma zinawaka tu wakati

wa Bunge labda kwa maana ya kulenga ujio wa Bunge na wageni wengine wa kiserikali. Taa hizi zinawaka wakati wote labda inapotokea tatizo la au ulipaji wa kodi kama nilivyoeleza kwamba taa za mjini hapa zinawaka kutokana na mikataba iliyowekwa kati ya Manispaa na kampuni ya *Outdoor* na hii kampuni ya *Ashton* ambayo niliyoeleza na kama kuna tatizo linatokea basi ni la kampuni hiyo kutolipia bili kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nadhani ushauri wa Mheshimiwa Sanya ni mzuri zaidi kama ambavyo ameshauri kwamba sasa tuweke taa za gharama nafuu ili haya makampuni tunayoingia nayo mikataba yasije yakaingia kwenye tatizo hili ambalo sasa Mheshimiwa Nkamia anadhani kwamba taa hizi zimewekwa hasa kwa ajili ya Wabunge, hapana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu wa uwekaji wa taa bado upo, kwa nini kwa kuanzia mradi huu basi tusianze katika maeneo muhimu kama vile kuelekea Ofisi ya Waziri Mkuu, *General Hospital* na barabara ya Chuo Kikuu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba Manispaa ya Dodoma sasa baada ya kuingia kwenye mgogoro na Kampuni ya *A1 Outdoor*, sasa wamekubaliana na kampuni ya *Ashton Media* ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuweka taa kwenye maeneo yale ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

Mheshimiwa Spika, sasa tunasubiri utaratibu huo ukamilike ili kuweka taa hizo kuanzia kwenye maeneo hayo mpaka makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda Hospitali ya Mkoa ambayo nimeitaja pia hapa na mkataba huu ni wa miaka mitano kuanzia tarehe 18 Desemba, 2011 na utaishia tarehe 15 Desemba, 2016. Kwa hiyo tunatarajia maeneo yote taa zitawaka.

Na. 398

**Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya ya Rorya**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Wilaya ya Rorya inakabiliwa na ukosefu wa huduma za afya kwa sababu hakuna hospitali ya Wilaya, wala vituo vya Afya na Zahanati za kutosha:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa, inajenga na kukamilisha zahanati kwa kila kijiji Wilayani ya Rorya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Rorya haina hospitali ya Wilaya. Hata hivyo kwa sasa wananchi wa Rorya wanapata huduma za rufaa kupitia hospitali ya *DDH Shirati* ambayo ina mkataba na Halmashauri kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwapo kwa hospitali ya Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imetenga eneo la hekta tano katika eneo la Ingri na kiasi cha shilingi milioni 85 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa sasa Halmashauri inakamilisha ujenzi wa Bohari ya Dawa na mwaka ujao wa fedha hospitali hii imeombewa maombi maalum ya shilingi bilioni moja. Aidha, ujenzi pia utaendelezwa kwa kutumia fedha za mpango wa MMAM.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhamira ya kila Kata kuwa na kituo cha afya na kila Kijiji kuwa na zahanati, Serikali kupitia mpango wa MMAM kila mwaka huingiza kwenye mipango ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati, ambazo wananchi wameziibua wakati wa zoezi la uandaaji wa mipango shirikishi ngazi za kijiji.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu huu shirikishi, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, umewezesha kujenga zahanati nne(4) na nyumba moja (1) ya watumishi wawili. Aidha, Serikali pia imepanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 66 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Kwa kuwa, uibuaji mipango kwa njia shirikishi inataka miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa katika kijiji iwe ni kipaumbele cha jamii, nichukue nafasi hii kumwomba Mbunge kushirikiana na Halmashauri ili kuelimisha jamii kuibua mipango ambayo italenga kuboresha afya zao hasa ujenzi wa zahanati.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake la msingi ametambua jitihada za Halmashauri na kwamba tayari wameshatenga eneo na wametenga bilioni 75, pia wameomba maombi maalum, ninataka kujua, ni lini Serikali itatoa hiyo shilingi bilioni moja ili kuunga mkono jitihada za Halmashauri za Wilaya ya Rorya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kituo cha afya cha Manyamanyama kilichopo Wilaya ya Bunda kwa sasa hivi kimepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya Wilaya, lakini mbali na maombi ambayo yameletwa na Mganga Mkuu wa Wilaya, bado Hospitali hiyo inapewa mgawo wa vifaatiba na dawa kama kituo cha afya. Ni lini watapewa vifaatiba na dawa kama hospitali ya Wilaya kwa sababu inatoa huduma si kwa Wilaya ya Bunda tu hata Wilaya ya Musoma Vijijini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hospitali hiyo sasa imepandishwa hadhi kuwa hospitali ya Wilaya badala ya kuwa kituo cha afya na baada ya utaratibu huo ndipo inapofuata sasa mabadiliko ya mgawo wa dawa ili uendane na hospitali ya Wilaya. Tunachoweza kumwambia Mbunge ni kwamba Mganga Mkuu wa Mkoa atume maombi rasmi ili tubadilishe mgawo kuwa mgawo wa hospitali ya Wilaya. Jambo hilo halina tatizo kwa sababu imeshakubalika kwamba hospitali hiyo ipandishwe hadhi, kwa hiyo kinachofuata ni utaratibu tu wa kawaida (*formalities*) za kuwezesha kupata mgawo unaostahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanamrisho Abama nimekuona umesimama?

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Sikusimama.

**SPIKA:** Hukusimama, haya Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swlai la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wananchi wa Same Mashariki wao hawangoji kujengewa Zahanati, wamejinyima wamejenga Zahanati kama Kirangare, Pinji, Kalemawe na Mwale, lakini zahanati hizi hazina Waganga, hazina Wauguzi bado zinabaki kama magofu. Je, Serikali haioni kwamba kwa kutokuwasaidia wananchi wanaojenga zahanati wenyewe kuwapelekea kila kitu, inawavunja moyo wananchi katika kuchangia maendeleo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kuna zahanati nyingi, vituo vya afya na hospitali nyingi za Wilaya, Mikoa na hata hospitali za Rufaa ambazo hazina wafanyakazi wa kutosha katika maeneo hayo na ndiyo maana kama Serikali tumetambua umuhimu wa kuongeza idadi ya wadahiliwa katika vyuo vya afya. Tunavyozungumza sasa tumefikia 7500 na lengo ni kufikia idadi ya wanafunzi 10,000 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu wa kuongeza wadahiliwa katika vyuo vya afya, tumetoa vibali vya ajira, mwaka huu vimepatikana vibali 5600 ambavyo vimeshatangazwa, karibu Halmashauri zote za Wilaya zimepata mgawo. Hatusemi kwamba tutamaliza tatizo, tunachosema ni kwamba huu ni mwanzo na tumeahidiwa kwamba mwaka ujao wa fedha tutapata idadi ya vibali 11,000. Tukiendelea na hatua hizi, ni matumaini yetu kwamba baada ya muda mfupi tutaweza kupunguza sana tatizo la uhaba wa wafanyakazi wa afya katika vituo vya afya.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kuwa, Serikali imeanzisha Wilaya mpya takribani 14 ili kusogeza huduma kwa wananchi kama vile huduma ya afya, ikiwemo na Itilima, ni lini wataleta mpango kabambe ambao utatoa hospitali za Wilaya katika hizo Wilaya mpya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeanzisha Wilaya mpya nchini kote na Wilaya hizi sasa ndiyo tunaanza kujenga uwezo wake wa kuanza kufanya kazi zake vizuri ikiwemo kupeleka rasilimali watu na fedha, lakini pia kuona huduma muhimu za jamii ikiwemo na ujenzi wa hospitali unafanyika. Kwa sasa maeneo haya mapya yaliyoanzishwa yanayo hospitali zozote ambazo zinaweza kuingia mkataba ili kuanzisha huduma kwa sasa wakati Serikali tunaweka utaratibu mwingine wa kuwezesha Wilaya hizi kuwa na hospitali zake zitakazokuwa na hadhi ya Kiwilaya, tunashauri Halmashauri ya Wilaya Mama ambazo zimeibua Wilaya mpya kusaidia kuweka utaratibu huo ili na sisi TAMISEMI tuweze kujua ni hospitali gani imeteuliwa tuweze kusaidia kuweka taratibu vizuri za mikataba hiyo ili kuwa na huduma hii ya afya mara moja.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Tatizo la Rorya linafanana sana na tatizo lililopo Kibaha Mjini. Kwa kuwa sasa hospitali ya Tumbi imepandishwa ya kuwa ni hospitali ya rufaa, kituo cha afya cha pale Mkoani, bado hakijaweza kupewa hadhi ya kuwa hospitali ya Wilaya na hii inapelekea wananchi kuhangaika

na kutokuweza kupata matibabu, jambo ambalo hata Naibu Waziri amejionea mwenyewe kiasi kwamba hata Mganga pamoja na Muuguzi hawana ofisi. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupandisha hadhi kituo kile cha afya na kukifanya kuwa hospitali ya Wilaya?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupandisha hadhi hospitali au vituo vya afya kuwa hospitali za Wilaya, ni lazima uanze kwenye Halmashauri husika. Ninachoweza kumshauri Mbunge ni Kwamba sasa waanze mchakato wa maombi rasmi kwamba kituo hicho cha Afya kipandishwe hadhi kuwa hospitali ya Wilaya baada ya ile hospitali yao ya Wilaya kuwa hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Kwa maana hiyo ni kwamba watakapokuwa wameleta maombi hayo rasmi, Wizara yangu itayafanyia kazi na kukipandisha hadhi kituo hicho kuwa hospitali ya Wilaya na hivyo kuweza kupata mgawo wa dawa pamoja na wafanyakazi wanaoendana na Hospitali ya Wilaya.

Na. 399

**Msamaha wa Karo kwa Wanafunzi wenye Ulemavu**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR)** aliuliza:-

Tarehe 27 Agosti, 1999 aliyekuwa Rais wa Tanzania katika mahojiano na watoto kutoka shule mbalimbali nchini alitoa agizo la kusamehewa karo kwa wanafunzi wote wenye ulemavu na taarifa ya agizo hilo lilipelekwa Wizarani na kwa Makatibu Tawala wote:-

(a) Je, kwa nini agizo hilo la Rais la kuwasamehe karo watoto wenye ulemavu limepuuzwa hadi leo?

(b) Je, ni kwa nini watu wenye ulemavu wanasahaulika kiasi kwamba hata zinazopotolewa kauli na viongozi juu ya haki zao na jitihada za kuwapunguzia ugumu wa maisha hazipewi uzito?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tarehe 27/8/1999, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo la kusamehewa karo kwa wanafunzi wote wenye ulemavu. Nakiri pia kuwa taarifa ya agizo hilo ilipelekwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa ufafanuzi, dhana ya agizo hili la msamaha linalenga wanafunzi hao walipiwe karo na mahitaji yao mengine ya kielimu na Halmashauri zao. Zipo Halmashauri zilizoweka utaratibu mzuri ambao unatimiza agizo hilo la kuwalipia wanafunzi wenye ulemavu. Ili kuweza kuwabaini walengwa, Halmashauri inatakiwa kuweka utaratibu kutoka ngazi ya shule, Kata, na Halmashauri husika. Hivyo, wazazi wa watoto wenye ulemavu wanaostahili kulipiwa na Halmashauri na hawalipiwi, washauriwe kutoa taarifa kwa uongozi wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, si kwamba haki za wenye ulemavu zinapuuzwa au hazipewi uzito, bali kwa upande wa kielimu inatokana na ukosefu wa mawasiliano mazuri kati ya wazazi, shule na Halmashauri husika. Ikumbukwe pia siyo wazazi wote wa watoto wenye ulemavu hawana uwezo wa kulipia watoto wao karo za shule, bali pia wapo wazazi wengine wanaoweza kugharimia elimu ya watoto wao wenye ulemavu. Aidha, wapo watoto wengine wasio na ulemavu lakini wazazi wao wana ulemavu na wengine hawana uwezo kabisa, hivyo huhitaji sana kulipiwa na Halmashauri. Kinachohitajika ni busara zitumike ili watoto wenye wazazi wasioweza kumudu kulipa karo wawezeshwe kusoma.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa rai kwa Halmashauri zote kuchukua hatua za kuwawezesha wanafunzi wote wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu ambao wanastahili kulipiwa ada wafanyiwe hivyo kwa wakati.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru pia Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba zipo Halmashauri ambazo zimeweka utaratibu mzuri kwa ajili ya kutimiza agizo hili, ina maana inakiri kabisa kwamba zipo Halmashauri ambazo hazijaweka utaratibu mzuri. Ningeomba Serikali ituambie imechukua gani kwa zile Halmashauri ambazo hazikuweka utaratibu mzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wanawashauri wazazi ambao walipaswa kulipiwa na hawakulipiwa waende kutoa taarifa kwenye uongozi wa Halmashauri hizo. Hili ni agizo la Rais na Halmashauri zimekaidi, ninaomba Serikali itoe kauli kwamba ni nani mwenye ruhusa ya kukaidi agizo la Rais?(*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuna Halmashauri ambazo nimesema kwamba zinafanya vizuri, ninaweza nikazitaja baadhi ya hizo Halmashauri ni kama vile Ilala, Kinondoni, Kwimba, Tabora Manispaa, Singida, Songea, Manispaa ya Dodoma, hizi na zingine zimefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile ambazo mpaka hivi sasa hazijafanyakazi vizuri, kama nilivyosema katika jibu la swali la msingi kwamba, ninatoa wito kwamba zijipange vizuri ziweze kutimiza jambo hili ambalo ni muhimu sana kwa mustakabali wa wananchi wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, zile ambazo hazijafanya hivyo kwa maana ya swali la pili, tutaendelea kuzibana na nitaomba

Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ifanye kazi hiyo kwa umakini zaidi ili kuhakikisha lile ambalo Mheshimiwa Rais Mkapa alilifanya basi linatekelezwa kwa ukamilifu wake.

**MHE. DKT. PUDENCIANA D. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, uzoefu unaonesha kwamba si tu walemavu wanaoshindwa kulipa karo bali pia zipo familia zinazoishi katika mazingira magumu ambayo imekuwa ni tatizo katika ulipaji wa karo hasa kwa shule za sekondari. Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa kufikiria namna ya kufuta karo katika shule hizo za sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba inatoa elimu kwa watoto wote katika nchi yetu ya Tanzania na Serikali itaendelea hivyo mwaka hadi mwaka kadri uwezo unavyopatikana kuhakikisha kwamba inapunguza mzigo kwa wananchi wake kama ambavyo hivi sasa shule za msingi hamna ada na shule ya sekondari kwa kutwa ni shilingi 20,000 na bweni 70,000. Shilingi 20,000 haiwezi kumsomesha mtoto lakini huu ni mchango wa mzazi au mlezi katika shule hizo. Kwa hivyo, tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunapunguza mzigo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wasiokuwa na uwezo, kuna utaratibu maalum hivi sasa katika Halmashauri zetu wa kuweza kuwatambua wanafunzi hawa kuanzia ngazi ya shule mpaka ngazi ya Kijiji, ngazi ya Kata na Halmashauri zimetakiwa zitenge katika bajeti zao za maendeleo kila mwaka ili kuweza kuwahudumia wanafunzi hawa ambao wanatambuliwa kuwa hawana uwezo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Serikali imesaini Mikataba ya Kimataifa ya kutetea Watu Wenye Ulemavu na wanafunzi wenye ulemavu wanahitaji mambo mengine maalum kwa mfano Albino wanahitaji miwani, mafuta na vitu vingine ili

waweze kusoma tofauti na wanafunzi wengine. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea vifaa maalum wanafunzi hawa? Nalisema hili kwa sababu Mikataba ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu inataka nchi wanachama kusaidia haki za watu wenye ulemavu ili wapate elimu kama watu wengine. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali hii inatambua wajibu wake wa kuwahudumia wananchi wake wenye ulemavu kama ni wananchi sawa na wengine katika Taifa letu. Serikali imeendelea kuhakikisha katika ngazi zote za elimu inaweka mifumo inayowezesha vijana wa kike na wa kiume kuweza kufanikisha malengo yao katika elimu.

Mheshimiwa Spika, tuna Sera ya Elimu Shirikishi, kuwachanganya wao pamoja na wasiokuwa na ulemavu na tunahakikisha kwamba tunapeleka vifaa vinavyowasaidia wale wasioona, Albino na wenye ulemavu wa aina nyingine ili kuhakikisha kwamba na wao wanafaidika. Kuanzia mwaka jana kwa walemavu hata mitihani yao tumehakikisha kwamba inatengenezwa kwa namna tofauti, si sawasawa na wengine kwa sababu wao uoni wao siyo mzuri. Tunachukua hatua zote kuhakikisha kwamba wanapokuwa shuleni wanaweza kupata masomo yao kwa njia ya mafanikio zaidi.

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nilikuwa napenda kujua kwa kuwa Serikali ilikwishakutoa tamko la kuweza kuwasamehe watoto wenye ulemavu na wale ambao wanaishi katika mazingira magumu na kwa kuwa katika Halmashauri zetu watoto wanapomaliza shule wananyimwa vile vyeti vya shule kwa sababu wanaambiwa Halmashauri hazijapeleka hela na mpaka leo hii watoto wanazurura mitaani hawana vyeti hivyo. Je, Serikali itatoa lini kauli ya kuweza kuwashinikiza Halmashauri hizo ili ziweze kupeleka hizo fedha kwa haraka ili wale watoto waweze kupata vyeti vyao vya shule? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama kuna Halmashauri ambazo hazijapeleka pesa na zimesababisha wanafunzi wasiokuwa na uwezo ambao wametambulika na kupangiwa na Halmashauri walipiwe karo zao na Halmashauri hizo, basi natoa wito hapa kwamba Halmashauri hizo zifanye jambo hilo mara moja. Halmashauri hizi ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nina hakika kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya hapa itahakikisha kwamba Halmashauri hizo zinafanya hivyo. Kwa wale wazazi ambao hawajalipa madeni yao katika shule ndiyo maana vijana wa *Form Four* na wengine wanakosa vyeti vyao, nawaomba wazazi na walezi hawa wahakikishe kwamba hawanyimwi haki zao watoto wao hawa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli Halmashauri zetu zimejitahidi kusaidia kulipia au kutoa mafunzo bure kwa watoto wenye ulemavu lakini watoto hawa wanapojitahidi na kufanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha sita wanapata taabu sana kuendelea na elimu ya juu kwa sababu utaratibu wa kupewa mkopo uliowekwa hauwatambui. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, ni kitu gani kitasaidia au utaratibu gani utakaosaidia ili watoto hao waweze kutambulika na kupata mikopo au kusamehewa kabisa? Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, vigezo vya kupewa mikopo kwa ajili ya elimu ya juu au kwa wanafunzi wa elimu ya juu vimeweka msisitizo katika uhitaji wa mwombaji, uhitaji ndiyo jambo kubwa kwamba mwanafunzi huyo anauhitaji wa mikopo na hana uwezo wa kujigharamia. Utambuzi wa uhitaji, moja katika mambo makubwa yanayoangaliwa ni uyatima, ulemavu ama uwezo wa kiuchumi wa mzazi au mlezi. Kwa hiyo, ukiwa yatima au mlemavu hiyo ni *guarantee* ya kwanza kabisa na ya mbele na ndivyo imekuwa ikifanywa kila mwaka na itaendelea kufanywa hivyo mpaka pale tutakapoweza kumpa kila mwanafunzi wa Tanzania pesa za kwenda kusoma katika vyuo vikuu. Hawabaguliwi, wao wanakuwa ndiyo watu wa kwanza kabisa katika kupewa mikopo hii.

Na. 400

**Idadi ya Watu Wazima Wasiojua Kusoma na Kuandika**

**MHE. VITA R.M. KAWAWA (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Zoezi la kutoa elimu kwa watu wazima lilikuwa linafanywa na Walimu wa shule za msingi kwa kuwapa *honoraria* ili wawafundishe watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu lakini sasa hivi mpango huo umesimama kwa muda mrefu:-

(a) Je, watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu wamemalizika?

(b) Kama hawajamalizika, je ni wangapi ambao bado wana tatizo hilo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha elimu ya watu wazima?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu ya watu wazima ni jukumu mojawapo kati ya majukumu ya Wizara yangu. Kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 kila asasi ya elimu, shule ya msingi, shule ya sekondari, ama vyuo katika nchi yetu, vyote hivi ni vituo vya kutolea elimu ya watu wazima. Uamuzi huo wa kisera ulifikiwa ili kuwezesha utoaji wa elimu hiyo kutumia miundombinu ya asasi hizo ambazo ni pamoja na madarasa, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, Walimu na vyenzo nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu hawajamalizika. Sensa ya mwaka 2012 haijatoa mchanganuo wa takwimu za watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Hata hivyo, takwimu za sensa ya mwaka 2002 zilionyesha kuwa kati ya watu wazima na vijana wenye umri miaka 15 na kuendelea watu milioni 6.2 sawa na asilimia 31 walikuwa hajui kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha elimu ya watu wazima, Serikali inatekeleza yafuatayo: imefufua na kuboresha mpango wa awali wa elimu ya watu wazima kupitia program ya Ndiyo Ninaweza, yenye lengo kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika nchini na inatumia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mpango wa uwiano kati ya elimu ya watu wazima na jamii ama tukiita MUKEJA ambao mpaka mwaka 2012 ulikuwa na jumla ya wanakisomo 907,771.

Mheshimiwa Spika, juhudi za pamoja zinahitajika ili kuwaondolea wananchi wetu kadhia ya kutojua kusoma na kuandika. Natoa wito kwa viongozi wa kada na ngazi zote, Mikoa, Wilaya, Kata, vituo, viongozi wa dini na asasi zisizo za Serikali kujihusisha kikamilifu katika kuhamasisha jamii na kuleta msukumo mpya katika kutekeleza mpango wa elimu ya watu wazima nchini.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa umuhimu wa kufahamu takwimu za wasiojua kusoma na kuandika kwa sasa ni mkubwa sana. Kama wito wako uliotoa Mheshimiwa Waziri, kada zote za ngazi za viongozi wa Mikoa, Wilaya waweze kufanyia kazi suala hili, je, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali inaweza kuhimiza Idara hii ya Takwimu itoe haraka mchanganuo huu wa watu wasiojua kusoma na kuandika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Idara ya Elimu ya Watu Wazima ndiyo ambayo husimamia ufundishaji wa elimu ya watu wazima lakini hutengewa fedha kidogo sana kupitia Halmashauri zetu. Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha katika Idara hii ili iweze kufanya kazi yake kikamilifu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu takwimu za wasiojua kusoma na kuandika zitoke mapema sana. Napenda kutoa taarifa kwamba Idara hii ya Takwimu chini ya wanaoendesha sensa au chini ya Kamishna wa Sensa, sasa hivi iko kwenye mchakato wa kuzikamilisha takwimu hizi. Tutarajie tu kwamba hivi karibuni sana nadhani tuite mawiki wala siyo miezi, taarifa hizi zitatolewa hadharani ili Taifa zima lijue kwamba sasa hivi tumefikia wapi katika kuondosha kadhia hii ya kutokujua kusoma na kuandika na mimi matengemeo yangu ni kwamba tutakuwa tumeboreka zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2002. Kwa sababu ya mambo mengi ambayo tumeyafanya hapa katikati, tumepiga hatua nzuri. Nina imani kwamba takwimu zitakapotoka hivi karibuni zitakuwa ni takwimu ambazo zitaonyesha juhudi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuondosha kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Watu Wazima kupewa pesa, Idara ya Watu Wazima hasa katika Wizara, tumeendelea kuipigania ili iweze kupata pesa nyingi zaidi. Waheshimiwa Wabunge mridhie wapate pesa nyingi zaidi ili kuweza kufanya kazi hii. Tumeandaa mpango huu mpya ambao tunauita kwa jina Ndiyo Ninaweza na mwaka huu wa fedha ambao unamalizika Juni ulikuwa umetengewa na kupewa pesa jumla ya shilingi bilioni mbili na milioni hamsini na mwaka ujao au mwaka mpya wa fedha umetengewa jumla ya Sh.1,555,300,075 kwa ajili ya kutekeleza mpango huu ambao utakapokuwa unatekelezwa unahakikisha kwamba asiyejua kusoma na kuandika ndani ya miezi minne anakuwa ametolewa katika giza hilo la kutokujua kusoma na kuandika.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa katika Mkutano wa Elimu ya Wazima uliofanyika Brazil mwaka 2009, Serikali ilikubali kuunda Kamati ya Pamoja kushirikisha sekta binafsi ili kuendeleza suala la elimu ya watu wazima nchini. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, Kamati hiyo imeshaundwa?

**SPIKA:** Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, samahani sikulielewa swali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Likokola, uliza tena swali lako.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa *CONFINTEA* uliofanyika Brazil mwaka 2009 kuhusiana na elimu ya watu wazima, Serikali ilikubali na kuazimia kuunda Kamati ya Pamoja kushirikisha sekta binafsi ili kuendeleza elimu ya watu wazima nchini. Je, Kamati hiyo imeshaundwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nikiri tu kwamba sina taarifa ya Azimio hilo lakini nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kwamba tunalifuatilia kama tulikuwa na jukumu hilo tuweze kutekeleza kikamilifu.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo hili la elimu ya watu wazima ni kwa Taifa zima na mfumo unaotegemewa zaidi na Serikali ni mfumo rasmi wa elimu na kuna mifumo mitatu ya elimu yaani ule *formal, non-formal and informal education.* Serikali haioni ni busara kutumia mifumo mingine ya elimu na hasa *non-formal,* ulio nje ya utaratibu wa mfumo rasmi ili iweze ika-*speed up* kasi ya kupunguza ongezeko watu wasiojua kusoma na kuandika?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, mfumo ambao tunatumia hivi sasa kupunguza idadi ya wananchi wasiojua kusoma na kuandika, ni ule mfumo ambao tunauita ni Mfumo wa Elimu ya Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Madarasa haya na mpango huo wa Ndiyo Tunaweza yanatoka kwenye ule mfumo ambao tunauita rasmi. Kama alivyopendekeza kwamba tunaangalia na mifumo mingine ili kuhakikisha kwamba giza hili la kutokujua kusoma na kuandika tunaliondosha. Katika mfumo rasmi tunaanza mwaka huu na kitu tunachokiita kuwa ni Utambuzi Gunduzi katika darasa la pili. Mwisho wa mwaka darasa la pili huwa hatuna mtihani hatuangalii kama vijana

wanajua ama kuandika. Wanaenda tu mpaka wanafikia darasa la nne. Kuanzia mwaka huu, tutawa-*test* vijana lakini sio kwa mtihani wa kila mmoja bali kwa *sample* ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wa darasa la pili wanajua kusoma na kuandika na kama tukigundua kwamba kuna idadi kadhaa ambayo haijui kusoma na kuandika katika darasa la tatu, tutaweka madarasa maalum kuhakikisha kwamba kundi hili halipandi juu likiwa halijui kusoma na kuandika mpaka lifikie kumaliza darasa la saba. *(Makofi)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Katika Mkoa wa Rukwa, sisi ni miongoni mwa waathirika kati ya waathirika namba moja wasiojua kusoma na kuandika na katika Mkoa wetu wa Rukwa kuna wakulima stadi kama mnavyojua. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza kupeleka elimu hiyo katika Mkoa wa Rukwa ili watu waweze kusoma *instructions* za kilimo pale wanaponunua dawa zao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri. Tutashirikiana naye ili tuweze kuleta mafanikio kwa Mkoa wa Rukwa pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Tumeweza kuogelea kwa nguvu kwa sababu maswali yalikuwa machache lakini bado tujifunze kuuliza maswali kwa kifupi na kujibu maswali kwa kifupi kusudi tuweze kupata wachangiaji wengi katika kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo ya wageni. Napenda kutoa taarifa ifuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, nalazimika kutoa maelezo mafupi kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti atoe kuhusu Taarifa ya Kamati ya Majumuisho.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu ya Mkutano ilionyesha kwamba vilitengwa siku sita za kufanya majumuisho

kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 105(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013 ambayo inasomeka kama ifuatavyo:-

Baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa makadirio ya Wizara zote ndani ya siku sita kabla ya hotuba ya bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoishia na makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Waheshimiwa Wabunge, nia ya Bunge kuweka masharti haya ya Kanuni ni kuwezesha Serikali kuzingatia maoni na ushauri unaotokana na hoja zenye maslahi ya taifa zilizotolewa na Kamati za Kudumu za Bunge au Wasemaji Wakuu wa Upinzani na maoni yanayotokana na michango ya Wabunge mbalimbali waliopata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba za bajeti zilizowasilishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tulipoweka masharti haya, yapo mambo ambayo yalizingatiwa kama vile kwenye Kanuni ya 105(3) ya Kanuni hizi ambapo inaweka masharti ya Kamati ya Bajeti, Serikali na Kamati ya Uongozi chini ya Uenyekiti wa Spika kupata maelezo ya msimamo wa Serikali kuhusu masuala haya muhimu na kwa namna ambavyo yamezingatiwa. Aidha, Kanuni ya 105(8) imeweka masharti ya utaratibu ambao utafuatwa wa uwasilishaji wa hotuba mbalimbali zinazohusu bajeti kwa maana ya wasemaji wote, Waziri anayeshughulikia Mpango, Waziri wa Fedha, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Msemaji wa Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya zoezi la mchakato wa bajeti, niliitisha kikao cha Kamati ya Bajeti ili kuhitimisha majumuisho kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni 105(1) na Kanuni ndogo (3) juu ya hoja zilizojitokeza wakati Bunge lilipopokea utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaoanzia tarehe 1 Julai, 2013.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya mashauriano na Serikali, nimeona ni vizuri mkapata taarifa fupi ya makubaliano tuliyofikia katika maeneo yote yaliyojitokeza na baadaye mtapewa bango kitita kama kabrasha hivi lenye maelezo ya jumla.

Waheshimiwa Wabunge, naomba muelewe kwamba taarifa itakayotolewa na Mwenyekiti wa Kamati siyo maoni ya Kamati kuhusu bajeti bali ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kufahamu yale mliyokuwa mmechangia jinsi Serikali ilivyoyazingatia.

Waheshimiwa Wabunge, tunachosema, mpaka sasa tumemaliza awamu ya kwanza ya bajeti pale tulipojadili Wizara mbalimbali, Kamati zenu kutoa maoni yake, yale maoni yalifanyiwa kazi na Kamati ya Bajeti. Maoni yale baada ya kufanyiwa kazi na Kamati ya Bajeti inabidi tuwape mrejesho kabla hatujaingia kwenye awamu hii ya pili ya bajeti.

Hii awamu ya pili tunajaribu kuona jinsi mlivyojadili kule nyuma kwenye Wizara mbalimbali ni vitu gani Serikali imesikiliza na vitu gani pengine wameshindwa kusikiliza, kwa hiyo, ndio atakachosema basi, ni kuleta mrejesho kwenu kwamba kuna hatua zilizochukuliwa na zingine zimeshindikana kwa sababu ya maelezo yatakayotolewa.

Kwa hiyo, basi kwa maana hiyo, namwomba Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge aweze kutoa taarifa fupi ya majumuisho kwa niaba yangu. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ridhaa yako kama Mwenyekiti wa Kamati ya Majumuisho kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti kwa Mujibu wa Kanuni ya 105(1) na (3) naomba kutoa taarifa fupi ya mashauriano hayo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha

taarifa ya majumuisho kuhusu uchambuzi wa hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Kamati za kisekta kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Kamati ya Bunge ya Bajeti imepewa jukumu la kuchambua mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/13 unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 unaoanza rasmi tarehe 1 Julai, 2013. Kwa mujibu wa Kanuni ya 105(1), Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti imepewa jukumu la kufanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta kama zilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, Taarifa hii ni mrejesho kwa Bunge lako Tukufu wa matokeo ya mashauriano hayo. Hivyo ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati yangu imetekeleza jukumu hilo kikamilifu. Kazi hiyo imefanyika kwa muda wa miezi miwili tangu tulivyowasili hapa Dodoma kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bajeti ulioanza tarehe 8 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, jinsi Kamati Ilivyofanyika Kamati Ilivyofanya kazi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote zilizowasilisha hoja zao kwa Mheshimiwa Spika. Aidha, Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta zilizokuwa na hoja walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusu hoja hizo. Hatua hii ililenga kupata maoni yao kuhusu hoja hizo ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kama inavyostahili. Mfano kwa maeneo ambayo yalihitaji fedha za nyongeza, Kamati ilihitaji kupata mchanganuo juu ya maombi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja nyingi zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta zilihusu maombi ya nyongeza za fedha kwenye Wizara mbalimbali kwa ajili ya

matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo, Kamati iliona busara kumshirikisha Waziri wa Fedha kila ilipobidi na pia Kamati ilifanya kazi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Hazina kwa kuwa wao ndio wanahusika na ugawaji wa fedha kwenye mafungu mbalimbali ya Bajeti ya Serikali. Pia Kamati ilishirikisha wataalamu kutoka Tume ya Mipango kwa kuwa Tume ya Mipango ndiyo inahusika moja kwa moja na Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kamati pia ilifanikiwa kukutana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi kwa lengo la kushauriana namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wataalamu na wadau hawa walishirikiana vema na Kamati katika kujadili na kushauri masuala mbalimbali yanayohusu taratibu za ugawaji wa fedha kwenye mafungu mbalimbali, hatua ambayo iliisaidia Kamati kufanya maamuzi. Aidha, kwa kuwa baadhi ya wataalamu hao walikuwa ni wawakilishi wa Serikali, walikuwa wakiwasiliana na Serikali mara kwa mara kwa ajili ya kupata maelekezo kuhusu maombi ya fedha za nyongeza na kutoa ufafanuzi wa hoja nyingine ambazo zilihitaji maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha ufuatailiaji wa hoja hizo, Kamati yangu imeainisha hoja hizo na namna zilivyoshughulikiwa katika mfumo wa bango kitita *(matrix)* ambalo ni sehemu ya taarifa hii na litagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Bango kitita hilo lina sehemu *(columns)* kuu nne.

Sehemu ya kwanza inahusu Hoja za Kamati za Kisekta; Sehemu ya pili inahusu Maelezo ya Serikali ambayo yametolewa kupitia Wataalamu kutoka Hazina na Tume ya Mipango walioshiriki katika vikao vya Kamati; Sehemu ya tatu ni Maelezo ya Kamati ya Bajeti na Sehemu ya nne inaainisha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge na zile zilizoridhiwa na Kamati ya Bajeti na kupendekeza zitolewe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kutekeleza Kanuni ya 105(1)na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, Kamati ya Bajeti ilikutana na Kamati ya Uongozi ya Bunge pamoja na Serikali kwa ajili ya mashauriano ili

kuzingatia hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kupitia bajeti ya Serikali. Hivyo, kufuatia mashauriano hayo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa masuala kadhaa yameridhiwa kupitia vikao hivyo kama nitakavyoeleza hivi punde.

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na Mijadala ya Hoja. Kamati ilipokea takribani hoja sabini na moja (71) kutoka katika Kamati za Kisekta Kumi (10). Kati ya hoja hizo, hoja 32 zilihusu maombi ya fedha za nyongeza kwenye Wizara na taasisi mbalimbali kwa mwaka 2013/2014 na hoja 39 zilihusu masuala mengine, mfano maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013, maombi ya kubakiza (*retention)*, malipo ya madeni na kadhalika. Kamati imechambua kwa kina hoja zilizohusu ongezeko la fedha na kuazimia kupendekeza nyongeza ya fedha katika hoja za Mafungu kumi na tatu (13) na mafungu mawili yaliongezewa fedha na Bunge bila kupitia katika Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya kuongeza fedha katika baadhi ya Mafungu yalifikiwa baada ya uchambuzi, mijadala na mashauriano marefu kati ya Kamati ya Bajeti, Wenyeviti wa Kamati za Kisekta, Mawaziri pamoja na maoni na ushauri kutoka kwa wataalam wa Hazina na Tume ya Mipango. Jumla ya fedha za nyongeza zilizoombwa ni shilingi bilioni 654.21. Fedha za nyongeza ambazo tayari zimeidhinishwa rasmi na Bunge ni kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 49 - Wizara ya Maji - shilingi bilioni 184.5. *(Makofi)*

(ii) Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi - shilingi bilioni 30. *(Makofi)*

(iii) Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara - shilingi bilioni 30. *(Makofi)*

(iv) Fungu 96 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - shilingi bilioni 9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha hizo kuna nyongeza ya fedha katika mafungu yafuatayo ambayo iliidhinishiwa na Bunge bila kupitia kwenye Kamati ya Bajeti. Nyongeza hiyo ni katika mafungu yafuatayo:-

(i) Fungu 35 -Idara ya Kurugenzi ya Mashtaka - shilingi bilioni 10. *(Makofi)*

(ii) Fungu 40-Mfuko wa Mahakama - shilingi bilioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha za nyongeza katika Mafungu hayo sita ni shilingi bilioni 283.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na fedha hizo za nyongeza ambazo ziliripotiwa Bungeni, yapo maombi mengine ya fedha za nyongeza kiasi cha shilingi bilioni 370.71 yaliyoridhiwa na Kamati na kuwasilishwa Serikalini kwa mashauriano. Kati ya fedha hizo, Serikali imekubali kutoa kiasi cha shilingi bilioni 229.5. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi - shilingi milioni 350. *(Makofi)*

(ii) Fungu 43- Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika (ruzuku ya mbolea na mbegu bora) - shilingi bilioni 21.15. *(Makofi)*

(iii) Fungu 53-Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake) - shilingi bilioni 2. *(Makofi)*

(iv) Fungu 58- Wizara ya Nishati na Madini (Umeme Vijijini- *REA*) - shilingi bilioni 186. *(Makofi/Vigelegele)*

(v) Fungu 99- Wizara ya Mifugo na Uvuvi - shilingi bilioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, baada ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali, imekubalika

kwamba kati ya shilingi bilioni 654.21 zilizopendekezwa na Kamati kuongezwa kwa Mafungu mbalimbali, shilingi bilioni 513 zitaongezwa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 78.42 ya fedha yote iliyopendekezwa kuongezwa. Kiwango hiki si haba, tunaishukuru sana Serikali kwa uelewa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa mahitaji ya fedha ni mengi kuliko mapato ya Serikali na kutokana na taratibu zilizopo, Kamati haikuweza kujua vyanzo vipya vya mapato vinavyopendekezwa na Serikali kwa sababu Kitabu cha Kwanza cha Makadiro ya Mapato (*Revenue Estimates*) hakikutolewa na Serikali hadi tunaandika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati ililazimika kuchukua hoja hizo chache tu kwa ajili ya kuongezewa fedha. Hoja hizo zilichukuliwa kutokana na uzito na uharaka wake. Aidha, Kamati pia ilifanya maamuzi kwa kuzingatia umuhimu wa hoja kama zilivyowasilishwa na Kamati za Kisekta pamoja na mchanganuo wa matumizi ya nyongeza ya fedha hizo kama ulivyowasilishwa na Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Mafungu mengine yaliyoombewa fedha za nyongeza na Kamati za kisekta hayakuweza kuongezewa fedha kutokana na upungufu wa fedha usiolingana na mahitaji. Kamati inashauri kwamba Serikali iendeleze juhudi katika ukusanyaji wa mapato ili fedha hizo zipatikane na kisha ziwasilishwe Bungeni katika mfumo wa Bajeti ya Nyongeza *(Supplementary Budget).*

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza wakati wa uchambuzi. Kwa kuwa huu ni Mkutano wako wa kwanza wa Bunge lako Tukufu ambapo utaratibu mpya wa kujadili na kuidhinisha bajeti ya serikali umeanza kutumika tofauti na utaratibu uliozoeleka kwa kipindi kirefu huko nyuma, Kamati imekutana na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kitu kipya wakati wote kina changamoto zake. Kamati imebaini changamoto mbalimbali ikiwemo ya mafungu mengi kutotengewa fedha ya kutosha katika miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha miradi

mingi ya maendeleo kutotekelezwa kikamilifu na kushindwa kukamilika kwa wakati. Utaratibu uliotumika wa kupitisha hoja mahsusi kupitia Kamati hii ya Bajeti umewezesha kubaini hali hiyo. Hivyo, Kamati inaamini kwamba katika mwaka ujao wa fedha, utaratibu huu mpya utaendelea kuboreshwa na maeneo yanayoeonekana kuwa na upungufu yataboreshwa na kuimarishwa. Kwa msingi huo, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kuhusu maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uzito wa hoja. Hoja zilizowasilishwa kwenye Kamati hii zilibainishwa kama Hoja Mahususi na nyingi zilijielekeza katika maombi ya bakaa ya fedha kwa mwaka 2012/2013 na nyongeza ya fedha kwa mwaka 2013/2014, malipo ya madeni ya ndani, yakijumuisha madeni ya wazabuni, watumishi wa umma, wastaafu, michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, maombi ya fedha za kubakiza *(retention)* na maombi kuhusu kupatiwa fungu linalojitegemea kwa baadhi ya Taasisi. Kimsingi, Kamati yangu ilijielekeza zaidi katika kutafuta suluhisho kwa hoja zilizohusu nyongeza ya fedha. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa hoja nyingine ambazo hazikuhusu maombi ya fedha zilikuwa zina uelekeo wa kifedha (*financial implication),* Kamati iliona busara kutoa maoni na ushauri kwa Serikali juu ya kutatua hoja hizo kama zinavyoelezwa kwenye bango kitita katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa kwa baadhi ya hoja, mfano hoja za kuomba nyongeza ya watumishi; Kamati imeshauri hoja kama hizo kwa siku za usoni zishughulikiwe na Kamati za kisekta kupitia Wizara husika. Aidha, Kamati ya Bajeti ina maoni kwamba ipo haja kwa Kamati hizo kujadili na kuchambua hoja mahsusi zenye maslahi ya kitaifa kwa undani zaidi kabla ya kuamua kuwasilisha hoja hizo mbele ya Kamati ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, hatua za mapato. Kamati inatambua utaratibu uliopo wa mapendekezo ya Makadirio ya Mapato kuwekwa wazi baada ya Waziri wa Fedha kusoma bajeti ya Serikali Bungeni. Utaratibu huu umekuwa ni changamoto kwa Kamati ya Bajeti katika kutekeleza

majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 Nyongeza ya Nane Kifungu 9(f) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013. Kwa kuwa mfumo huu mpya wa bajeti umeanza kutumika wakati maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 yameshaanza, Kamati haikupata fursa ya kutekeleza jukumu hilo la kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali. Hata hivyo, Kamati itatoa maoni yake baada Waziri wa Fedha kusoma Bajeti yake na kuweka Mezani Muswada wa Fedha *(Finance Bill, 2013/2014).* Kwa msingi huo, Kamati inaamini kuwa katika siku zijazo itaweza kupata fursa ya kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mapendekezo ya makadirio ya mapato mapema kabla ya Mwongozo, Matazamio na Upeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linatolewa katika misingi ya kutambua umuhimu wa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika hatua muhimu za maandalizi ya bajeti, kuichambua, kuipitisha na kusimamia utekelezaji wake. Kwa kuwa sehemu kuu ya bajeti ya Serikali inatokana na makusanyo ya mapato ya ndani, hivyo itakuwa ni vema kwa Kamati ya Bajeti kushirikishwa na kufahamu mapema vyanzo vya mapato vinavyopendekezwa na Serikali ili na yenyewe iweze kutoa maoni na ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwasilisha maombi ya nyongeza ya fedha. Kimsingi Kamati ya Bajeti imetambua umuhimu wa utaratibu huu mpya wa kuwasilisha maombi ya fedha za nyongeza kupitia Kamati hii. Kwa kuwa kuna baadhi ya nyongeza ya fedha zilifanyika bila kupitia Kamati hii, Kamati inapendekeza na kusisitiza kwamba ili kuepuka kuleta mikanganyiko na mvutano baina ya Kamati ya Bajeti na Serikali, ni vema maombi yote ya nyongeza za fedha yanayofanywa na Serikali yapitie kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya uchambuzi kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele vilivyowekwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, uhamisho wa fedha ndani ya fungu. Kamati ilibaini kuwepo kwa maombi ya uhamisho wa

fedha ndani ya fungu. Katika hili, Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa uhamisho huu hauathiri mafungu mengine na mchakato wake sio mgumu kwa kuwa unahitaji kuwepo kwa makubaliano na Wizara husika, masuala kama haya yaishie tu kwenye Kamati za Kisekta. Iwapo Wizara husika itaafiki juu ya uhamisho huu basi hatua inayofuata ni kuiarifu Wizara ya Fedha ili iweze kufanya marekebisho katika vitabu vya Bajeti kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vipaumbele. Wakati wa kuchambua hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta na hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge Bungeni, Kamati ya Bajeti ilijielekeza zaidi kwenye maeneo yafuatayo:- maji, kilimo, viwanda, mifugo, uvuvi, nishati ya umeme na miundombinu.

Hata hivyo, kutokana na upungufu wa rasilimali fedha, Kamati haikupata nyongeza ya fedha kwenye maeneo mengine licha ya kutambua umuhimu wake. Kwa kuwa utaratibu huu ndio umeanza, katika kipindi kijacho, Kamati itajielekeza zaidi katika kubainisha vyanzo vya mapato ili kuishauri Serikali kukusanya mapato ya kutosha ili yaweze kugawiwa katika maeneo mbalimbali ya vipaumbele kwa lengo la kuimarisha ukuaji wa sekta hizo na hivyo kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa, inatenga fedha za kutosha katika maeneo yote muhimu kwa maslahi ya Taifa ili kuepuka ongezeko la maombi ya fedha za nyongeza kila mwaka. Vilevile, ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati na kwa gharama zilizopangwa, Kamati inapendekeza kuwa fedha zilizotengwa kwenye miradi ya maendeleo zilindwe (*ringfenced*) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla. Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Bunge lako Tukufu inapenda kukushukuru kwa kulishirikisha Bunge katika utaratibu wa huu mpya wa mchakato mzima wa bajeti ambapo faida zake zimeanza kuonekana. Licha ya utaratibu huu kuanza wakati mchakato

wa bajeti umeanza, Wabunge wameweza kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya bajeti. Aidha, utaratibu huu umetoa fursa nzuri kwa Kamati za Kisekta, Serikali na sekta binafsi kujadiliana kwa kina mambo mbalimbali yanayohusu bajeti ya Serikali kupitia Kamati ya Bajeti. Hivyo, matokeo ya utaratibu huu ni kwamba Serikali imeweza kuongeza fedha kwenye baadhi ya Mafungu na pia Bajeti ya Serikali kwa mara ya kwanza itaanza kutekelezwa mara moja kuanzia tarehe 1/07/2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanza kwa utaratibu huu ni jambo moja na utekelezaji wake ni jambo jingine hivyo Kamati ina maoni yafutayo ili kuweza kuboresha utaratibu huu katika siku zijazo:-

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya bajeti. Kamati imebaini kwamba kuna umuhimu wa kusisitiza juu ya nidhamu katika kutayarisha, kupitisha na kusimamia utekelezai wa bajeti ya Serikali kama inavyokuwa imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kutokana na uchambuzi uliofanywa, Kamati imebaini kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kutolewa na Hazina mara nyingi inapelekwa kwenye maeneo ambayo sio yale ya vipaumbele vilivyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati wa maandalizi ya bajeti, Hazina inatoa ukomo *(ceiling)* kwa kila fungu na kutoa fursa kwa Maafisa Masuhuli kugawa fedha katika Mafungu wanayosimamia. Hata hivyo, imebainika kwamba kasma *(items)* za vipaumbele zimekuwa hazitengewi fedha za kutosha na badala yake fedha hizo kuelekezwa katika maeneo yasiyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati inatambua utaratibu wa uhamisho wa fedha kutoka Fungu moja kwenda Fungu jingine au Mafungu mengine unaofanywa na Waziri wa Fedha unafanyika kisheria. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba utaratibu huu unavuruga utekelezaji wa Bajeti hasa kwa upande wa Miradi ya Maendeleo. Ni maoni ya Kamati kwamba ipo haja kwa Bunge lako Tukufu kuangalia upungufu

wa kisheria ya utaratibu huu na kufikiria kutunga Sheria ya Bajeti *(Budget Act)* itakayowezesha Bunge lako Tukufu kusimamia Bajeti ya Serikali kikamilifu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utoaji wa fedha. Kuhusu kutolewa kwa fedha kwa njia ya *exchequer warrant,* ambayo imekuwa ikitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha (Julai-Septemba), Kamati inashauri kuwa fedha hiyo iendelee kutolewa. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa Serikali imekuwa ikijielekeza katika kutoa fedha za matumizi ya kawaida katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha, itumie utaratibu huo kutoa pia fedha za maendeleo ili kuruhusu miradi ya maendeleo kuanza kutekelezwa haraka iwezekanavyo pindi Bunge lako linapoidhinisha Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dokta William M. Mgimwa, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Saada Mkuya na Mheshimiwa Janet Mbene, kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Nawashukuru kwa dhati wataalamu wote kutoka Hazina na Tume ya Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika kutoka ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta hadi kukamilika kwa bango kitita ambalo litagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Naomba niwatambue wataalamu hao kwanza ni Ndugu John M. Cheyo, Ndugu Ezekiel Mpanda, Ndugu Augustine K. Ollal, Ndugu Edwin Makamba, Ndugu Robert Masatu na Ndugu Jacob Focus. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja hizo na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa

Christina M. Lissu, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo na Mheshimiwa Rita Mlaki.

Mheshimiwa Spika, aidha nawashukuru Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Peter Serukamba ambao walikuwa ni wajumbe washiriki wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upya wa Kamati hii, majukumu mazito iliyonayo pamoja na changamoto zilizopo, Wajumbe hawa wamefanya kazi kwa uvumilivu, kwa kipindi kirefu, kwa umakini ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa D. Mbise na Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto na Michael Kadebe kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila jambo jipya linakuwa siyo rahisi lakini busara inatumika kwamba hicho ambacho siyo rahisi ndiyo hicho hicho ukifuate kabisa mpaka kifike. Kwa hiyo, unakuta tofauti yake ni kwamba badala ya Serikali kuahidi tu tutatoa hapa, tutatoa hapa, kienyeji tu lakini safari hii tumekaa meza moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo na wao Serikali sasa hivi hawaoni shida, wanajua kabisa mahali ambapo watafanya nyongeza kwa mujibu wa taratibu tulizo kubaliana. Kwa hiyo, ni utaratibu

ambao ni mzuri. Lengo ni kurudisha nidhamu ya bajeti katika nchi kwa sababu kila tunachopitisha sisi ni vizuri kikajulikana na kesho tukakiulizia maswali. Kwa hiyo, tunazo Kamati za kisekta, Kamati za Kisekta pia zina wajibu. Haya tutakayopitisha hapa baada ya awamu ya pili, Kamati za Kisekta lazima zisimamie halafu baada ya hapo Kamati za *Watchdog* nazo zinasimamia sasa matumizi halisi.

Kwa hiyo, mfumo wa kuwa na *Internal Auditor* inasaidia hizi sekta mbalimbali, mfumo wa kuwa na *CAG* inasaidia zile Kamati za *Watchdog*. Sasa pamoja tunaweza kufanya kazi nzuri ya kusimamia Serikali na bajeti ikiwa bajeti ambayo ina nidhamu inayostahili. Kwa hiyo, uwazi ni wa lazima hakuna namna ya kuficha, unafichaje bajeti ya Serikali na itakuja hapa? *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kusimamia utaratibu huu, hawana wataalam wa kwao, wameazima Hazina tunashukuru, lakini ni muhimu kuwa na wataalam ambao watafanya kazi na *Budget Committee* wakati wote.

Eneo la mapato bado hatujafanya vizuri, ni muhimu tukafanya nalo vizuri kusudi tunaposema tunataka matumizi lakini na mapato pia tunafahamu yanatoka wapi. Hilo nalo ni muhimu itabidi tuzingatie.

Kwa hiyo, niipongeze Kamati ya Bajeti, niwapongeze Waheshimiwa wote kwenye Kamati zenu za sekta ambao mlitoa kama malighafi kwa Kamati ya Bajeti iliyofanyia kazi na ahsante kwa Serikali kwa kushirikiana vizuri katika suala hili.

Kwa hiyo, kuanzia sasa tunaanza sehemu ya pili ya bajeti. Kabla sijamwita Waziri anayehusika na mambo ya Mipango, naomba niwatambue wageni tulionao hapa. Tunao wageni wanaochangia Bajeti Kuu ya Serikali yaani *General Budget Support Development Partners,* wanaongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Balozi Lennarth Jelmaker, Balozi wa Sweden*, if you could stand up, thank*

*you very much.* Halafu amefuatana na Mabalozi na viongozi wengine, yupo Mheshimiwa Balozi Sinikka Antila, Balozi wa Finland, ahsante sana. Yupo Mheshimiwa Marshall Elliot, Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Uingereza, ahsante. Yupo Mheshimiwa Filiberto Ceriani Sebregondi, Balozi wa *EU,* ahsante sana. Yupo Mheshimiwa Philippe Dogia, Mwakilishi wa Benki ya Dunia Tanzania. Yupo Mheshimiwa Jonny Flento, Balozi wa Denmark, naona wengine watakuja mchana. Yupo Tonio Kandiero, Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, wengine kama hawasimami watakuja mchana. Yupo Mheshimiwa Thomas Baunsgaard, Mwakilishi wa *IMF* Tanzania halafu na yupo Profesa Beno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Yupo Dokta Natu E. Mwamba, Naibu Gavana Benki Kuu ya Tanzania, ahsante. Yupo Dokta Philip Mpango, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango, ahsante sana. Hawa ndiyo wageni wetu rasmi ambao inabidi tuwakaribishe. *(Makofi)*

Baada ya hapo tunaendelea, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/14. Taarifa hizi ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ambao ulipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2011. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ambaye ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa maelekezo yake ambayo yametuwezesha kuwasilisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mzingatie utulivu, kama mnaondoka, muondoke kimyakimya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Aidha, napenda kutumia nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha taarifa hizi. Vilevile, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kutupatia maoni na ushauri ambao umesaidia kuboresha taarifa ninazowasilisha hivi leo. Tutaendelea kuipatia Kamati ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake na kuzingatia maelekezo yanayotolewa katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa mipango ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dokta William Augustao Mgimwa, kwa ushirikiano wake wakati wa maandalizi ya taarifa na hotuba hii. Aidha, nawashukuru Ndugu Ramadhani Khijjah, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Dokta Philip Mpango, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda niwashukuru wafanyakazi wote wa Taasisi hizi mbili pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini yao kwa kufanikisha utayarishaji wa taarifa na Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Mawaziri wenzangu na wabunge wote, kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na Mpendwa wetu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, aliyekuwa Mbunge wa Chambani Pemba *(CUF)* ambaye alifariki Dunia mwezi Machi 2013. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Aidha, wapo wananchi waliofariki dunia katika

maafa na ajali mbalimbali nchini. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote na kuwatakia afya njema wote waliojeruhiwa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ninayowasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tano: kwanza ni maelezo kwa kifupi kuhusu mwenendo wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012; pili ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013; tatu, ni miradi ya kitaifa ya kimkakati ambayo Serikali inatarajia kutekeleza kwa mwaka 2013/2014. Sehemu ya nne inaelezea kwa ufupi gharama za utekelezaji wa mpango, tathmini na ufuatiliaji, mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno ya utangulizi, naomba sasa nianze kwa kuelezea kwa muhtasari Taarifa ya Hali ya Uchumi katika kipindi cha mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa uchumi wa Dunia. Katika mwaka 2012 uchumi wa dunia haukuimarika ipasavyo kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu ni pamoja na: wasiwasi kuhusiana na ulipaji wa madeni kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Ulaya; sera za kubana matumizi nchini Marekani na kudhoofika kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa China. Katika kipindi hicho, pato la dunia lilikua kwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2011. Aidha, kasi ya ukuaji wa pato la nchi zinazoendelea katika bara la Asia, hususan China na India ilipungua na kuwa asilimia 6.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.1 mwaka 2011. Hata hivyo, taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Aprili 2013 *(World Economic Outlook),* inaonesha kuwa hali ya uchumi wa Dunia imeanza kuimarika hasa kwa nchi zinazoibukia kimaendeleo na zile zinazoendelea *(emerging economies).* Ukuaji wa Pato la Dunia unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 3.3 kwa mwaka 2013 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi zinazoendelea bado una changamoto ya kujinasua kutoka katika ukuaji mdogo wa uchumi hasa kwa kuzingatia kudhoofika kwa

shughuli za kiuchumi na biashara ya kifedha katika nchi za Ulaya kulikosababishwa na mgogoro wa madeni *(Euro Debt Crisis)*, hususan katika nchi za Ugiriki, Ureno, Italia na Hispania. Kiwango cha ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea kilipungua na kuwa asilimia 1.2 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.6 mwaka 2011. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2011. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na sera za kubana matumizi na kudhibiti ujazi wa fedha katika nchi hizo, sanjari na uhaba wa mitaji ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha. Kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukuaji unaonesha taswira inayotofautiana kwa baadhi ya nchi kuwa na viwango vya ukuaji unaongezeka na nchi nyingine kushuka. Nchi za Tanzania na Kenya zimeonesha ukuaji mzuri ikilinganishwa na Rwanda, Burundi na Uganda kwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi Tanzania uliongezeka kutoka asilimia 6.4 mwaka 2011 hadi asilimia 6.9 mwaka 2012 na Kenya kutoka asilimia 4.4 mwaka 2011 hadi 4.7 mwaka 2012, wakati kwa upande wa Rwanda, Burundi na Uganda ukuaji ulishuka kutoka asilimia 8.6, 4.2 na 6.7 mwaka 2011 hadi asilimia 7.7, 4.0 na 2.6 mwaka 2012 kwa mtiririko huo. Matarajio kwa mwaka 2013 yanaonesha kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zitafanya vizuri zaidi na kuwa na ukuaji wa juu kuzidi ule wa mwaka 2012 kutokana na kuendelea kuimarika kwa uwekezaji katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Taasisi ya *Business Insider* ya Marekani kwa kutumia takwimu za Benki ya Dunia, Tanzania ni miongoni mwa nchi ishirini zitakazokuwa na ukuaji wa uchumi wa kasi zaidi duniani kati ya mwaka 2013 hadi 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, taarifa ya Kamisheni ya Uchumi ya Afrika *(UN Economic Commission for Africa)* ya

mwaka 2013, Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi zitakazokuwa na ukuaji wa kasi zaidi barani Afrika kati ya 2013 na 2015, ikiwa na ukuaji usiopungua asilimia saba. Nchi nyingine ni pamoja na Ethiopia, Zambia, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Ghana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa uchumi wa Taifa. Ukuaji wa Pato la Taifa. Pato halisi la Taifa kwa mwaka 2012, lilikua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2011. Ongezeko hili la ukuaji lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano pamoja na kuimarika kwa uzalishaji viwandani hasa baada ya jitihada za Serikali zilizolenga kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika sambamba na matumizi ya nishati mbadala katika uzalishaji viwandani. Aidha, ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo kufuatia kuwepo kwa hali nzuri ya hewa na jitihada za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa ruzuku ya mbegu bora na mbolea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, Pato la Taifa lilikuwa shilingi 44,717,663 milioni kwa bei za mwaka husika, ikilinganishwa na shilingi milioni 37,532,962 mwaka 2011. Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2012, Tanzania Bara ilikuwa na watu 43,625,354 katika mwaka 2012 ikilinganishwa na makadirio ya watu 43,169,305 mwaka 2011. Hivyo, pato la wastani la kila mtu liliongezeka kwa asilimia 17.9 na kuwa shilingi 1,025,038 mwaka 2012 ikilinganishwa na shilingi 869,436.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kasi ya upandaji bei. Kasi ya upandaji bei za bidhaa na huduma ilifikia wastani wa asilimia 16.0 mwaka 2012 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.7 mwaka 2011. Kasi hii ya upandaji wa bei ilisababishwa na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia na bei za chakula kulikotokana na mahitaji makubwa ya chakula katika baadhi ya nchi jirani. Fahirisi ya bei ya chakula ilichangia zaidi katika kupanda kwa kasi ya jumla ya upandaji bei kwa kuwa bidhaa za chakula huchukua karibu nusu ya bidhaa na huduma zinazotumika katika ukokotoaji wa fahirisi ya bei kwenye kapu la bidhaa za walaji.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, Serikali ilichukua hatua kadhaa zikiwemo: kuhakikisha kunakuwa na ugavi mzuri wa chakula unaoendana na mahitaji nchini; kupanua kilimo cha mazao ya chakula na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea, madawa na mbegu bora; kuendelea kuimarisha hifadhi ya chakula kwa kuongeza ununuzi wa mazao ya chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) pamoja na kujenga maghala ya kuhifadhi chakula; kutekeleza mpango mkakati wa kutatua tatizo la umeme nchini; na kupandisha kiwango cha riba ya Benki Kuu inayotozwa kwa mikopo iendayo kwenye taasisi za fedha nchini.

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha na karadha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kutoka shilingi bilioni 13,021.3, mwaka 2011 hadi shilingi bilioni 14,730.7 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Ukuaji huu ni chini ya lengo lililowekwa la asilimia 15.1. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye benki za biashara pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Rasilimali halisi za nje katika benki za biashara zilipungua kwa asilimia 28.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana *(M2)* uliongezeka kwa asilimia 16.0 na kufikia shilingi bilioni 10,724.5 mwaka 2012 kutoka shilingi bilioni 9,247.9 mwaka 2011. Kiwango cha ukuaji kilikuwa cha juu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.0 mwaka 2011 na cha chini ya lengo la asilimia 16.7 mwaka 2012. Aidha, karadha *(credit)* nchini iliongezeka kwa asilimia 25.2 kutoka shilingi bilioni 10,958 Desemba 2011 hadi shilingi bilioni 13,715 Desemba 2012. Kati ya hizo, shilingi bilioni 4,708.6 ni mkopo kwa Serikali Kuu na kiasi kilichobaki ni mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ulioishia Desemba 2012, mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 18.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 27.2 kipindi kama

hicho mwaka 2011. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulitokana na kupungua kwa kasi ya ongezeko la amana kwenye benki za biashara. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 21.1 ya mikopo yote, zikifuatiwa na shughuli za binafsi (20.4%), shughuli za viwanda (11.4%) na shughuli za kilimo (11.3%). Katika mwaka 2012, mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na asilimia 20.1 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viwango vya riba. Mwaka 2012, mwenendo wa riba za amana mbalimbali na zile za mikopo ziliimarika ikilinganishwa na zilivyokuwa mwaka 2011 kutokana na kupungua kwa ukwasi katika masoko ya fedha na pia kuongezeka kwa ushindani katika mabenki. Riba za mikopo ya mwaka mmoja ziliongezeka kutoka wastani wa asilimia 13.78 mwezi Desemba 2011 hadi kufikia asilimia 13.99 mwezi Desemba 2012, wakati riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka kutoka wastani wa asilimia 9.19 hadi asilimia 9.93. Hivyo, tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja zilipungua kutoka wastani wa asilimia 4.59 Desemba 2011, hadi kufikia asilimia 4.06 Desemba 2012.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilishuka kwa asilimia 0.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 10.3 mwaka 2011. Kasi ya kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilipungua kutokana na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu zikiwemo utekelezaji wa sera za fedha zenye lengo la kupunguza ukwasi kwenye uchumi na hatua nyingine za udhibiti wa benki za biashara. Kwa wastani, Dola moja ya Kimarekani ilinunuliwa kwa shilingi za Tanzania 1,583.7 mwaka 2012 ikilinganishwa na shilingi 1,557.4 mwaka 2011. Aidha, kufikia mwisho wa mwaka 2012, Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa Shilingi za Tanzania 1,571.6 ikilinganishwa na Shilingi 1,566.7 mwisho wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nje. Katika mwaka 2012, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka

kwa asilimia 15.5 kutoka Dola za Kimarekani milioni 7,398.2 mwaka 2011 hadi kufikia Dola milioni 8,544.4 mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa asilia ikiwemo kahawa, pamba na tumbaku, pamoja na ongezeko la mauzo ya bidhaa za viwandani, maua na samaki na mazao ya samaki.

Mheshimiwa Spika, aidha, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa mwaka 2012 iliongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka Dola za Kimarekani milioni 9,827.5 mwaka 2011 hadi dola milioni 10,324.9 mwaka 2012. Ongezeko hilo lilijitokeza katika makundi yote ya bidhaa ambayo ni bidhaa za ukuzaji mitaji, bidhaa za kati na bidhaa za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2012, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 4,069.1 ikilinganishwa na Dola 3,761.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2011. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2012 kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 3.9 ikilinganishwa na miezi 3.8 iliyofikiwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mitaji ya kigeni ya moja kwa moja. Mwaka 2012, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja *(Foreign Direct Investment)* iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,330.0 mwaka 2011 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,806. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilichangiwa na shughuli za uchimbaji wa visima vya gesi kutoka visima vitatu mwaka 2011 kufikia visima kumi mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali. Mapato. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2012/2013, jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 4,300.4, sawa na asilimia 93 ya makadirio ya shilingi bilioni 4,624.086 katika kipindi hicho. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 3,888.8 ambayo ni sawa na asilimia 97 ya lengo na mapato yasiyo ya kodi (yakijumuisha marejesho ya ununuzi wa *radar*) yalikuwa shilingi

bilioni 308.5 sawa na asilimia 72 ya lengo. Vilevile, mapato ya shilingi bilioni 103.1 yalikuwa ni makusanyo ya Halmashauri sawa na asilimia 57 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 181.1 kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo. Katika kipindi cha Julai - Desemba 2012, Serikali ilipokea misaada na mikopo ya kibajeti ya jumla ya shilingi bilioni 564.2, sawa na asilimia 67 ya makadirio ya shilingi bilioni 842.5 katika kipindi hicho. Kwa upande mwingine, kiasi cha shilingi bilioni 438.1 zilipokelewa kupitia mifuko ya kisekta, ikiwa ni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya shilingi bilioni 415.1 katika kipindi hicho. Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai – Desemba 2012 ilifikia shilingi bilioni 617.5 ambayo ni asilimia 33 ya ahadi ya shilingi bilioni 1,899.1 katika kipindi hicho kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, matumizi. Katika kipindi cha Julai - Desemba 2012, matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 7,252.3, sawa na asilimia 95 ya makadirio ya shilingi bilioni 7,634.00. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 5,247.5 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,004.9.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa. Hadi kufikia Desemba 2012, deni la Taifa lilifikia shilingi bilioni 21,028.61 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18,258.62 mwishoni mwa Desemba 2011. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 19,692.5 ni deni la Serikali na shilingi bilioni 3,019.4 ni deni la sekta binafsi. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya yenye masharti nafuu ya kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa Kundi la Paris ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kiuchumi kikanda na kimataifa. Mwaka 2012, wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walikubaliana kuendeleza miundombinu ya kipaumbele yenye sura ya kikanda inayowezesha kuiunganisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda nyingine hususan Utatu wa *COMESA-EAC-SADC* na nchi jirani Kusini

na Kaskazini mwa Afrika. Miundombinu ya kipaumbele iliyoidhinishwa ni ile ya reli, bandari, nishati na barabara. Aidha, wakuu hao walikubaliana kuendeleza miundombinu ya ndani ya nchi wanachama itakayoziwezesha nchi hizo kuzitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mtangamano, hususan Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, miradi mbalimbali ya maendeleo ya Kikanda iliendelea kutekelezwa ambapo ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – *Athi River* yenye urefu wa kilometa 104.4 kwa kiwango cha lami ulikamilika na kuzinduliwa na wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, uchambuzi wa kina wa ujenzi wa mtandao wa barabara za Arusha – Holili – Taveta – Voi na upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara za Malindi – Lungalunga na Tanga – Bagamoyo ulikamilika. Kwa upande wa ujenzi wa reli, upembuzi yakinifu wa awali wa mradi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Musongati ulikamilika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, mauzo ya bidhaa katika nchi za *SADC* na *EAC* yaliimarika ikilinganishwa na mwaka 2011. Kwa nchi za Afrika Mashariki, thamani ya mauzo iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 352.4 mwaka 2011 hadi Dola milioni 512.0 mwaka 2012 na kwa nchi za *SADC*, mauzo yaliongezeka kutoa dola milioni 1,158.8 hadi milioni 1,412.3 mwaka 2012. Hata hivyo, kasi ya ongezeko la mauzo kwa nchi za *EAC* ilikuwa ndogo ikilinganishwa na uagizaji, hali iliyosababisha kuwepo kwa nakisi katika urari wa biashara.

Mheshimiwa spika, maendeleo katika sekta za kiuchumi na kijamii. Sekta zinazokua kwa kasi zaidi (kati ya asilimia 7 mpaka 22) ni madini, ujenzi, mawasiliano, biashara na utalii na huduma za kifedha ambazo hazina uwezo wa kuajiri Watanzania walio wengi. Sekta hizi pia hazitoi soko la kutosha kwa mazao/bidhaa zinazozalishwa na sekta kama kilimo ambayo ndiyo mhimili wa uchumi wa Taifa kwa maana ya kuajiri wananchi walio wengi, (75%). Sekta hii imekua kwa wastani wa asilimia 3.6 tu kwa mwaka kwa kipindi cha miaka

kumi iliyopita. Ili kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi unapunguza umaskini kwa kiwango cha kuridhisha, Serikali itatilia mkazo zaidi uwekezaji katika maeneo/sekta ambazo wananchi walio wengi wamejiajiri. Msisitizo utawekwa katika kuelekeza rasilimali zaidi (fedha na watu) katika kuongeza tija katika sekta ya kilimo; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa wajasiriamali katika sekta rasmi na isiyo rasmi; na kuhuisha programu na mikakati ya kinga ya jamii kama *TASAF*, ikijumuisha uhawilishaji fedha kwa masharti maalum *(conditional cash transfers)* kwa walengwa, yaani makundi yenye umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nieleze kwa ufupi maendeleo ya ukuaji wa uchumi kwa sekta za kiuchumi na kijamii kwa kuwa maelezo ya kina yalishatolewa na mawaziri husika katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, kilimo, uwindaji na misitu. Shughuli za kiuchumi za kilimo, uwindaji na misitu mwaka 2012, zilikua kwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 2011. Aidha, shughuli ndogo za kiuchumi za mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa asilimia 4.7, 3.1 na 2.4 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.5, 3.9 na 3.5 mwaka 2011, kwa mtiririko huo. Kwa upande mwingine, shughuli za kilimo, uwindaji na misitu zilichangia asilimia 24.7 ya Pato la Taifa mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 24.6 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, uvuvi. Katika mwaka 2012, shughuli za kiuchumi za uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 2.9 ikilinganishwa na asilimia 1.2 mwaka 2011. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa idadi ya vyombo vya uvuvi na wavuvi. Aidha, shughuli za kiuchumi za uvuvi zilichangia asilimia 1.4 ya Pato la Taifa mwaka 2012 kama ilivyokuwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, viwanda na ujenzi. Shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani zilikua kwa asilimia 8.2 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2011. Ongezeko hili lilitokana na kuimarika kwa upatikanaji wa

umeme. Aidha, shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani zilichangia asilimia 8.4 katika Pato la Taifa mwaka 2012 kama ilivyokuwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilikua kwa asilimia 6.0 mwaka 2012, ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2011. Ongezeko hili lilitokana na juhudi za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kuimarisha miundombinu ya uzalishaji na usambazaji umeme. Shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilichangia asilimia 1.9 katika Pato la Taifa mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kilikuwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2011. Ukuaji huu ulitokana na: usimamizi, ufuatiliaji na udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato unaofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini (*TMAA*); kuanza upya kwa uzalishaji wa almasi katika mgodi wa *Wiliamson Diamonds Limited;* na ongezeko la tozo mbalimbali za madini. Mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe (*mining and quarrying*) kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.0 mwaka 2011. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kukamilika kwa miradi mingi ya ujenzi. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, ukuaji wa sekta ya maji ulikuwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2011. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa miradi ya maji ikiwemo ya uchimbaji visima na upanuzi wa mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Sekta ya maji ilichangia asilimia 0.3 katika Pato la Taifa mwaka 2012 kama ilivyokuwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, huduma. Shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma zilikua kwa asilimia 8.0 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2011. Shughuli ndogo nyingi zilikuwa na ongezeko la viwango vya ukuaji isipokuwa biashara na matengenezo; utawala; na elimu. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.9 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 44.0 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za biashara na matengenezo kilipungua na kuwa asilimia 7.7 mwaka 2012, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.1 mwaka 2011. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa mahitaji na biashara ya kikanda. Aidha, ongezeko la bei za umeme liliathiri shughuli za kibiashara na matengenezo na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wake. Hata hivyo, mchango wa shughuli ndogo za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 12.3 mwaka 2012 kutoka asilimia 12.2 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, shughuli ndogo za kiuchumi za huduma za mawasiliano zimeendelea kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji mwaka 2012 ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Shughuli ndogo za kiuchumi za huduma za mawasiliano zilikua kwa asilimia 20.6 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 19.0 mwaka 2011. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi na mauzo ya vocha za simu. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 2.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka. Idadi ya watu. Katika mwaka 2012, zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lilifanyika ambapo idadi ya watu Tanzania ilikuwa 44,928,923. Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya watu 43,625,354 sawa na asilima 97.1 na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,303,569, sawa na asilimia 2.9. Aidha, mchanganuo wa watu kijinsia unaonesha kuwa wanawake walikuwa 23,058,933 sawa na asilimia 51.3 na wanaume walikuwa 21,869,990 sawa na asilimia 48.7. Vilevile, matokeo haya yanaonesha kuwepo

kwa ongezeko la watu milioni 10.5 tangu sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, sawa na wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka. Kiwango hiki cha ukuaji wa idadi ya watu kimepungua ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 uliopatikana katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, mgawanyiko wa watu Kimkoa. Mgawanyiko wa watu kimkoa unaonesha kuwa kwa mwaka 2012 Mkoa wa Dar es salaam ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu nchini, ukiwa na watu 4,364,541 ukifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 2,772,509 na Mkoa wa Mbeya watu 2,707,410. Aidha, Mkoa wa Katavi ndio ulikuwa na watu wachache zaidi, ukiwa na watu 564,604. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa uliokuwa na idadi kubwa ya watu ni Mjini Magharibi wenye watu 593,678 na Mkoa wa Kusini Unguja ndio uliokuwa na idadi ndogo ya watu ukiwa na watu 115,588.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI. Mwaka 2012, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI kwa kutoa huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI. Idadi ya vituo vinavyotoa huduma za matunzo na matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI iliongezeka kufikia 1,176 ikilinganishwa na vituo 1,100 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Aidha, hadi Desemba 2012, Serikali ilikuwa imesambaza mashine 356 za kupima chembechembe za kinga za mwili (*CD4*) katika vituo vya kutolea huduma za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mazingira. Katika mwaka 2012, Serikali iliendelea kuhimiza wananchi kupanda na kutunza miti ili kuhifadhi mazingira. Katika kipindi hicho, jumla ya miti 111,994,448 ilipandwa katika Mikoa 11 nchini. Kati ya hiyo, miti 90,370,936 ilistawi, sawa na asilimia 80.7 ya miti iliyopandwa. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa kuondoa na kuteketeza viuatilifu chakavu ikiwa ni juhudi za kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, shehena ya viuatilifu chakavu iliyokuwa imelundikana nchini yenye ujazo

wa takriban tani 630 katika vituo 135, pamoja na udongo ulioingia viuatilifu hivyo takriban tani 415 vilikusanywa kwa ajili ya kuteketezwa.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA II na Malengo ya Milenia 2015. Katika mwaka 2012, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA-II 2010 - 2015) na Malengo ya Milenia 2015 (*MDGs*). Aidha, mwaka 2012 ulikuwa ni wa pili katika utekelezaji wa MKUKUTA-II ambapo tathmini ya kina iliripotiwa katika Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA (*MAIR* 2011/12). Katika uchambuzi wa viashiria mbalimbali vya MKUKUTA, kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha ingawa changamoto nazo zilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza umaskini wa kipato, Serikali iliendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa taarifa katika soko la ajira pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo. Kutokana na hatua hizo, jumla ya nafasi za ajira 250,678 zilipatikana. Fursa hizo za ajira zilipatikana katika maeneo yafuatayo: *TASAF* nafasi 34,516; ujenzi wa barabara nafasi 42,107; ujenzi wa majengo ya Serikali nafasi 17,685; Uwekezaji kupitia *TIC* nafasi 82,834; *EPZA* nafasi 15,100; Serikali nafasi 38,289; miradi ya kilimo nafasi 8,968; *SIDO* nafasi 9,946; miradi ya maji nafasi 49 na kampuni nyingine toka ofisi za ajira za Mikoa nafasi 1,184.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2012, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi ilitoa mikopo yenye masharti nafuu ya thamani ya shilingi bilioni 8.5 kwa wajasiriamali 8,497 (wanaume 5,331 na wanawake 3,166). Mikopo hiyo ilipitia vyama 49 vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Singida, Rukwa, Manyara, Ruvuma, Dodoma, Pwani, Tanga, Mbeya na Kagera.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kutumia Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza ajira kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu, maarufu kama Mabilioni ya Kikwete ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi

bilioni 49.65 kupitia benki na asasi za kifedha. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wajasiriamali 72,197. Kati yao wanaume ni 45,858 na wanawake 26,339.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu waliokuwa wanapata maji safi na salama vijijini na mijini (ukiondoa Dar es Salaam) mwaka 2012, ilifikia wastani wa asilimia 56.6 na 86 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, kiwango hicho kilikuwa chini ya lengo la MKUKUTA la asilimia 90 kwa wakazi wa mijini na 65 kwa wakazi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2012/13. Sasa naomba nitoe maelezo kwa ufupi juu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa hadi robo ya tatu ya mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mawaziri wa kisekta wameshaeleza kwa kina utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa sekta zao, naomba nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013 hasa kwa maeneo ya kimkakati ambayo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) ulipanga kuyatekeleza. Kimsingi, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13 mafanikio yamepatikana katika sekta mbalimbali licha ya kuwepo kwa changamoto kadhaa. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la reli, mradi wa kutandika reli yenye uzito wa ratili 80 kwa yadi unaotekelezwa na Kampuni *ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)* kati ya Stesheni ya Malongwe na Kitaraka (kilomita 89) uliendelea kwa kutandika kilomita 13 za reli na matengenezo katika maeneo 32 yaliyopo kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe yaliyokuwa yameharibiwa na mvua yamekamilika. Mafanikio mengine ni pamoja na kuanza kwa usafiri wa reli jijini Dar es Salaam kati ya stesheni za Dar es Salaam –Mwakanga na Dar es Salaam –Kurasini kwa reli ya *TAZARA* na Ubungo Maziwa kupitia Tabata hadi

Stesheni ya Dar es Salaam chini ya Kampuni ya *TRL*. Aidha, ujenzi wa madaraja matatu umeanza na vipuri kwa ajili ya ukarabati wa injini na mabehewa 125 ya mizigo vimeshawasili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli za kikanda, taratibu za kumpata mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha – Musoma zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu ya ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka –Kigali- Keza -Msongati (kilomita 1,464) kupitia kampuni ya *CANARAIL* ya Canada imekamilika. Serikali imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kupata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa reli (kilomita 197-80lb/yards) na kukamilisha ununuzi wa mataruma 2,200 kwa ajili ya ukarabati wa reli ya kati. Serikali imekamilisha mchakato wa kumpata Mtaalam Elekezi kwa usanifu wa kina wa reli eneo la Isaka - Kigali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha na kuongeza kina cha maji katika gati nambari moja hadi nambari saba katika bandari ya Dar es salaam; kutengwa kwa eneo lenye ukubwa wa ekari 1,468 kwa ajili ya kituo cha uchukuzi wa Mizigo Kisarawe, Pwani pamoja na kufanya tathmini kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi wa eneo hilo; kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani - Tanga, Mbegani - Bagamoyo na upanuzi wa bandari ya Mtwara; na kuendelea kwa ujenzi wa gati katika bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya umeme, maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi (Mtwara - Dar es Salaam) yameanza ambapo jiwe la msingi liliwekwa Novemba 2012. Serikali imeingia mkataba na Mkandarasi (*Jacobsen*) wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme Kinyerezi (*MW 150*). Hatua iliyofikiwa katika upanuzi wa gridi ya Kaskazini-Magharibi yenye msongo wa kV 400 kutoka mkoa wa Shinyanga hadi Mbeya kupitia Mikoa ya Kigoma na

Rukwa ni kuwasilishwa kwa maombi ya mkopo katika Benki ya *Exim* ya China kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo. Aidha, fidia kwa wananchi watakaopisha njia kuu ya umeme wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 670 kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida mpaka Shinyanga imelipwa na taratibu za kupata makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme zipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga na kuimarisha barabara zetu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa kilomita 374.65 ikilinganishwa na lengo la kilomita 414 za barabara kuu kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 90.5; ukarabati wa kilomita 140.6 dhidi ya lengo la kilomita 135 za barabara kuu kwa kiwango cha lami; kukamilika kwa ujenzi wa kivuko cha Rugenzi na kuendelea kwa ujenzi wa vivuko vya Msangamkuu na Ilagala.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madaraja, daraja la Malagarasi - kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 81; daraja la Kilombero-Mkandarasi amepatikana na vifaa kwa ajili ya ujenzi vimeshafikishwa eneo la kazi; ujenzi wa daraja la Kigamboni unaendelea; daraja la Kirumi – hatua za kumpata mhandisi mshauri wa kufanya usanifu wa kina na ukarabati zinaendea; ujenzi wa daraja la Nanganga umekamilika; ujenzi wa daraja la Nangoo upo katika hatua za mwisho; na ujenzi wa daraja la Sibiti umeanza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo. Mashamba ya mfano kwa ajili ya kilimo cha mpunga, yaliandaliwa katika skimu za umwagiliaji wa Mgololo (Mufindi); Ngana na Makwale (Kyela); Kidogovelo (Bagamoyo); Komtonga (Mvomero); Ilonga, Kinyamvumi na Rudewa (Kilosa); Kinyope (Mtwara); na Kitere (Lindi) na kubaini kuwa maeneo haya yanafaa kuendelezwa kwa kilimo. Aidha, ujenzi wa ghala la kuhifadhia nafaka katika Kanda ya Songea lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 liko katika hatua za mwisho; eneo la umwagiliaji liliongezeka kutoka hekta 363,514 mwaka 2011/2012 hadi hekta 450,392

mwezi Aprili, 2013 na Kampuni ya *YARA Limited* ya binafsi imeanza ujenzi wa ghala la kuhifadhi mbolea jijini Dar es Salaam, lenye uwezo wa kuhifadhi tani 45,000.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya mifugo, ukarabati wa maabara ya uhawilishaji wa viiini tete yaani *(embryo transfer)* Mpwapwa, Dodoma umekamilika kwa asilimia 80. Aidha, ujenzi wa mfumo wa kuhifadhi taarifa za utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo itakayosaidia kuwa na kanzi data *(database)* ulianza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi, Serikali iliendelea na ujenzi wa ghala la kutunzia mwani katika kijiji cha Jibondo huko (Mafia); kuendelea na ujenzi wa mialo ya Nyamisati (Rufiji), Kilwa – Masoko na Kilindoni (Mafia) na kuweka mitambo ya barafu na majokofu kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Aidha, maboya 63 ya kuweka mipaka ya hifadhi za bahari ya Mafia, Mnazi *bay* na maingilio ya Mto Ruvuma na maeneo tengefu ya Dar es Salaam na Maziwe (Pangani) yamenunuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, michoro *(layout design)* pamoja na zoezi la upimaji wa viwanja na maeneo ya miundombinu ya eneo la viwanda la *TAMCO* Kibaha, Pwani lenye ukubwa wa hekta 88 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya imekamilika; mradi wa Magadi Soda - Bonde la Engaruka, Arusha uchorongaji wa mashimo 12 ili kuhakiki kwa ufasaha zaidi, wingi na ubora wa magadi umekamilika. Mafaniko mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa majengo mawili ya usanifu wa kina wa mitambo ya kiwanda cha Viuadudu – Kibaha, Pwani na kukamilika kwa kiwanda cha saruji cha *Rhino Cement Company* cha Mkoani Pwani. Aidha, miradi mingine ya viwanda vya saruji iko katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwa ni pamoja na *Lee Construction Materials Company Limited* na MEIS *Cement Company* vilivyopo Lindi, Dar es Salaam *Cement Company, Lake Cement Company,* vya Dar es Saalam, *Fortune Cement Company* – Pwani; *Athi River Cement Company*–Tanga na Kisarawe *Cement Company* kilichopo Pwani, vyote viko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji – *EPZ/SEZ,* jumla ya shilingi bilioni 16.9 zimelipwa kama fidia kwa awamu ya kwanza na pili katika eneo la Bagamoyo ambapo jumla ya eneo lililokwishalipiwa fidia ni hekta 1,600 kati ya hekta 5,700. Aidha, Mpango Kamambe wa eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo umekamilika. Tathmini kwa ajili ya kulipa fidia katika mradi wa kituo cha biashara na huduma Kurasini ipo katika hatua za mwisho. Vilevile ajira katika maeneo maalum ya uwekezaji zimeongezeka kutoka watu 16,105 Juni, 2012 hadi watu 26,400 Mei, 2013; kuongezeka mtaji uliowekezwa kutoka dola za Kimarekani milioni 792 Juni hadi dola milioni 1,017 Mei, 2013; kuongeza mauzo nje yatokanayo na maeneo haya kutoka dola milioni 440 Juni, 2012 hadi dola milioni 602 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, mkataba wa miezi 15 wa ujenzi wa bomba la maji la Ruvu chini umesainiwa Septemba, 2012 kati ya *DAWASA* na *SINO HDYRO* kutoka China. Mkandarasi ameanza kufunga vifaa mbalimbali katika mtambo mpya. Kwa upande wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu; kazi ya usanifu wa upanuzi wa mtambo pamoja na nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi zimekamilika. Kwa upande wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera, mkandarasi wa uchimbaji wa visima vinane vya kukamilisha tathmini ya mwenendo wa maji ardhini alipatikana Septemba 2012. Serikali itaendelea na uchimbaji wa visima 20 na kazi ya kuthamini mwenendo wa maji ardhini na kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa mradi katika eneo la Kimbiji na Mpera.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine katika sekta ya maji ni pamoja na kukamilika kwa Ripoti ya mwisho ya Mazingira kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidunda; kukamilisha Hati ya Makubaliano kati ya *DAWASA* na *TANESCO* kuhusiana na umeme utakaozalishwa Kidunda; na kukamilisha uthamini wa fidia kwa eneo linalozunguka bwawa hilo, ambapo thamani yake ni shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji katika jiji la Mbeya. Mradi huu

ulihusisha ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kitekeo vya maji yaani *(intake) ma*eneo ya Imeta, Iyela, Ivumwe na Halewa; na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji katika maeneo ya *Forest,* Iwambi, Iganzo, *VETA*, Iganjo, Nsoho, na Idunda ambayo yana jumla ya mita za ujazo wa 6,900. Mradi ulihusisha ulazaji wa boma kuu lenye urefu wa kilomita 56.8 na mabomba ya usambazaji maji kilomita 280.16.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji vijijini, Serikali imeendelea kujenga miradi mipya, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji katika Halmashauri mbalimbali. Uboreshaji huo unatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Idadi ya wananchi wanaoishi vijijini ambao wanapata huduma ya maji safi na salama na ya kutosha karibu na makazi imeongezeka kutoka watu 16,308,651 mwezi Desemba, 2005 ambao ni sawa na asilimia 53.74 ya watu wote waishio vijijini hadi kufikia watu 20,634,227 mwezi Desemba 2012 ambao ni sawa asilimia 56.57 ya watu wote waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 katika usafiri wa anga ni pamoja na; kukamilika kwa kiwango cha lami na kuanza kutumika kwa njia za kurukia na kutua ndege, njia ya kuingia na kutoka uwanjani na maengesho ya ndege katika kiwanja cha Songwe; kukamilika kwa njia ya kurukia na kutua ndege katika kiwanja cha Kigoma; kukamilika kwa njia ya kurukia na kutua ndege yenye urefu wa mita 1,780 kwa kiwanja cha Tabora na kumalizika kwa uwekaji wa lami katika sehemu ya kurukia ndege yenye ukubwa wa mita 420 katika kiwanja cha ndege Arusha. Ukarabati unaendelea katika viwanja vya ndege vya Mwanza; Bukoba, Mafia na Kiwanja cha Julius Nyerere; Dar es Salaam. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Tatu la abiria *(Terminal III)* katika kiwanja cha ndege cha Julius Nyerere umekamilika na mkandarasi wa ujenzi amepatikana ambapo ujenzi rasmi wa jengo hilo utaanza katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa sekta ya huduma na maendeleo ya rasilimali watu ni kama ifuatavyo: Wataalm 295 wameendelea kugharamiwa na Serikali, kati ya hao, 195 ni wa Shahada ya Uzamili na 100 ni wa Uzamivu; Chuo cha Madini Dodoma kimeanza kuendesha mafunzo ya Diploma *in Geo-Science* kwa wanafunzi 61, ili kuandaa wataalamu katika eneo la gesi na mafuta; Serikali imefadhili vijana wa Kitanzania 122 katika fani ya mafuta na gesi katika vyo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali inakamilisha utaratibu wa kuwapeleka vijana 20 nchini Brazil na China kusoma Shahada za Uzamili na Uzanivu katika fani za gesi na mafuta. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha taasisi mbalimbali za utafiti ikiwa ni pamoja na: Taasisisi ya Utafiti ya Kizimbani – Zanzibar; Taasisi ya Utafiti wa Viwandani; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; Teknolojia ya Ngozi za Wanyama; Taasisi a Utafiti wa Afya na Tiba, Tume ya Taifa ya Mionzi na Taasisi ya Utafiti ya Ugonjwa wa Saratani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za fedha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imesajiliwa rasmi Septemba, 2012, Bodi ya Wakurugenzi imeshaundwa na mchakato wa kuajiri Maafisa Waandamizi unaendelea. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 60 kimeshatolewa kama kianzio cha mtaji wa benki hiyo. Katika kuongeza mtaji wa Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* ili kuiwezesha kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya maendeleo nchini jumla ya shilingi bilioni 40 zimeongezwa katika mwaka 2012/2013 kama mtaji. *TIB* imeendelea kufungua matawi zaidi na kuifanya benki kuwa na matawi matano hadi sasa ambayo ni Mbeya, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam (Samora na Mlimani). Benki ya Wanawake Tanzania ilipewa jumla ya shilingi milioni 200 na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mtaji wa shilingi bilioni saba. Mwaka 2012, benki iliendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake na wanaume ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.9 zilitolewa kwa wateja 14,663. Aidha, benki hiyo inakusudia kufungua tawi lake mjini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji. Katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/2013, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikijumuisha: ufinyu

wa rasilimali fedha; washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi kwa wakati; taratibu za manunuzi kuchukua muda mrefu na ulipaji wa madeni ya miaka iliyopita; maombi ya dharura; upatikanaji wa mikopo ya kugharamia miradi ya maendeleo na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Aidha, kutokamilika kwa tathmini ya fidia na ulipaji wa fidia kwa wakati imekuwa ni changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Kukosekana kwa miundombinu na huduma wezeshi kama barabara, maji na umeme katika baadhi ya maeneo ya miradi kulisababisha kuchelewa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014. Mpangao wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2013/2014 hautofautiani sana na ule wa mwaka 2012/2013. Kimsingi Mpango wa mwaka 2013/2014 ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016. Katika Mpango wa mwaka 2013/2014, vipaumbele vitaendelea kuwa vilevile vya Mpango wa Miaka Mitano ambavyo ni miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha. Katika mwaka 2013/2014, miradi ya maendeleo imegawanyika katika sehemu kuu mbili, miradi ya kitaifa ya kimkakati na miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Serikali itaendelea kujikita katika kuwezesha sekta binafsi kuchangia kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2013/2014 kuelekea 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kutoka asilimia 6.9 mwaka 2012, asilimia 7.0 mwaka 2013, asilimia 7.5 mwaka 2014, asilimia 8.0 mwaka 2015 na asilimia 8.5 mwaka 2016;

(b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimbu moja katika kipindi cha muda wa kati;

(c) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka asilimia 18.2 ya Pato la Taifa mwaka 2012/2013, 19.1 mwaka 2013/2014, 19.5 mwaka 2014/2015 na asilimia 20.0 mwaka 2015/2016;

(d) Kuongeza mapato yasiyo ya kodi kutoka asilimia 15.7 ya Pato la Taifa mwaka 2011/2012 hadi asilimia 16.6 mwaka 2012/2013 na asilimia 18.1 ifikapo mwaka 2015/2016;

(e) Kupunguza kazi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana yaani *(M3)* kufikia asilimia 17.4 mwaka 2012/2013 na kuibakisha katika kiwango vya asilimia 15 katika vipindi vya muda wa kati sambamba na lengo la kupunguza mfumuko wa kasi ya upandaji bei;

(f) Kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 20.0 ya Pato la Taifa Juni 2014;

(g) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) hadi kufikia asilimia 5.5 au chini zaidi katika kipindi cha muda wa kati; na

(h) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, misingi ya mpango kwa kipindi cha 2013/2014:-

(a) Kuendelea kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii;

(b) Kuwepo kwa nishati ya umeme kwa uhakika;

(c) Kuendelea kutekeleza Mapango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016;

(d) Kuimarika kwa thamani ya shilingi;

(e) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;

(f) Kuimarisha utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti;

(g) Kuendelea kuimarika kwa mahusiano na washirika wa maendeleo;

(h) Kuendelea kutekeleza sera ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi;

(i) Kuendelea na utekelezaji wa maboresho katika sekta ya umma;

(j) Kupunguza utegemezi;

(k) Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo; na

(l) Kuhakikisha ukuaji wa uchumi unapunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya Kitaifa ya kimkakati. Maeneo yanayopewa kipaumbele ni pamoja na miundombinu hasa uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya nishati, kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa bomba la gesi Mtwara, hadi Dar es Salaam utakaofanywa na sambamba na ujenzi wa mitambo miwili ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi katika eneo la Kinyerezi Dar es Salaam. Vilevile, kuimarisha usambazaji umeme nchini ikijumuisha uwekezaji katika miradi ya njia kuu ya kusafirisha umeme (220 Kv) kwenye eneo la kilometa 250 Makambako – Songea, umeme wa Msongo wa 400 Kv (Iringa – Shinyanga), umeme wa Msongo wa 400Kv (*North – West Grid)* na miradi ya upelekaji wa umeme vijijini.

Mheshimwia Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mradi wa usafirishaji kwa njia ya reli, barabara, anga na majini. Miradi ya reli inayokusudiwa kuendelezwa inajumuisha

kubadilisha njia ya reli kwa kuweka njia nzito ya kiwango cha ratili 80 kwa yadi; ukaratbati wa ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa; ukarabati wa reli (Kaliua – Mpanda na Isaka – Mwanza), mradi wa reli Mtwara – Mbambabay na Mchuchuma – Liganga, kuendeleza mrddi wa reli ya kikanda (Tanga – Arusha – Musoma na DSM – Isaka – Kigali) na kuanzisha njia mpya ya reli jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara, miradi itakayoendelezwa ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa barabara katika maeneo yenye kufungulia fursa za kiuchumi na ambazo zitaongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko kwa wakulima wakubwa na wadogo, ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro *Expressway* ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo inayounganisha jiji la Dar es Salaam na Mikoa mingine, ujenzi wa barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani pamoja na barabara za kupunguza msongamano mijini hususan katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa majini, shughuli zitakazoendelezwa ni pamoja na kuongeza kina cha gati, kufanya upanuzi na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa boya la mafuta katika bandari ya Dar es Salaam; kufanya usanifu wa kina na kuandaa michoro kwa ajili ya upanuzi wa bandari ya Kigoma na bandari kavu ya Katosho huko Kigoma; kukamilisha usanifu wa kina na kuandaa michoro katika bandari ya Tanga; kufanya usanifu wa kina na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi katika bandari ya Mbegani Bagamoyo; ujenzi wa jengo la abiria pamoja katika uzio wa bandari katika bandari ya Kasanga pamoja na upanuzi wa bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la usafiri wa anga, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka na kurefusha njia za kuruka na kutua ndege yaani *(runway)* katika viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora; kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria, jengo la hali ya hewa, barabara za kiwanjani na

uzio wa usalama katika kiwanja cha ndege Songwe; ukarabati viwanja vya Bukoba, Arusha na Mwanza pamoja na ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Serikali itaendelea kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini ili kuhakiikisha huduma za mawasiliano zinapatikana kiurahisi na kwa uhakika; kuendelea kutekeleza mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta; kuanzisha vituo vya kijamii vya mawasiliano vijijini na kuanza kwa ujenzi wa kijiji cha kisasa cha mawasiliano *(ICT Park Technology)* katika eneo la ukanda maalum wa uwekezaji *(SEZ)* pale Bagamoyo).

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya kilimo, vipaumbele vitakuwa ni kuendelea na miradi yenye kukuza uzalishaji wa mazao yenye thamani kubwa; kuogeza uzalishaji wa mazao ambayo ni malighafi ya viwandani; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya *SAGCOT* na kuzalisha chakula kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje na kuongeza ubora wa bidhaa za kilimo ili kukidhi viwango na mahitaji ya soko. Maeneo mengine ambayo ni kipaumbele yatajumuisha; ujenzi wa maghala mawili Mbozi na Songea yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za nafaka kila moja, kufanya tafiti mbalimbali na kukarabati miundombinu katika vituo vya utafiti; kuendelea na ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu 10 zenye jumla ya hekta 11,090, ujenzi wa mabwawa sita (6) yenye hekta 2,160 na kukarabati skimu 27 zenye jumla ya hekta 8,800 hususan kwa zao la mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya mifugo, vipaumbele vitakuwa ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo; kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na utambuzi wa mifugo; kuimarisha taasisi za tafiti za mifugo na kukamilisha michoro ya jengo na kuanza ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, Serikali itaendelea kukuza huduma na uzalishaji wa Samaki; na kuimarisha taasisi zinazoshughulikia tafiti za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa maji safi mijini na vijijini kwa mwaka 2013/2014, Serikali imepanga kutekeleza miradi ifuatayo: kujenga na kukarabati mtambo wa maji wa Ruvu Chini na Ruvu Juu; kuchimba visima 20 katika maeneo ya Kimbiji na Mpera; kulipa fidia na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 76 kutoka Ngerengere hadi Bwawa la Kidunda; kutekeleza mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe; kuimarisha usimamizi wa rasilimali maji; kulinda na kutunza vyanzo vya maji dhidi ya uchafuzi na uharibifu; na kuimarisha miundombinu ya maji vijijini chini ya mradi wa vijiji 10 katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya viwanda, vipaumbele vitakuwa ni kuendeleza viwanda hasa vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini; viwanda ambavyo msingi wake ni mazao ya kilimo, mifugo, samaki na rasilimali misitu; viwanda vinavyoongeza thamani ya madini yanayochimbwa hapa nchini; viwanda vikubwa vya mbolea na saruji; kanda maalum za kiuchumi zitakazokuwa na viwanda vya kutengeneza bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na lile la kikanda pamoja na viwanda vya kieletroniki na vile vinavyohusiana na TEHAMA. Katika eneo hili miradi itakayoendelea kutekelezwa ni pamoja na: mradi wa makaa ya mawe na chuma - Mchuchuma na Liganga, kukamilisha kiwanda cha Viuadudu Kibaha; mradi wa magadi soda Natron na Bonde la Engaruka; kiwanda cha magurudumu ya magari Arusha na uendelezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(EPZ & SEZs)* ya Bagamoyo, Ruvuma, Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi, mkazo utawekwa katika maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa huduma za jamii. Serikali itaendelea kuongeza idadi ya Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri katika ngazi zote za elimu hususan katika fani/

masomo ya Sayansi, Hisabati, Teknolojia na ubunifu; ujenzi na ukarabati wa miundombinu vyuo vikuu vya Dodoma, Mzumbe, Sokoine , Ardhi, Taasisi ya Sayansi za Bahari, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; kukamilisha Mpango kabambe wa uendelezaji wa Kampasi ya Mlonganzila; ujenzi wa Maktaba ya kisasa katika Taasisi Uhasibu Arusha; kuimarisha Mamlaka ya Elimu; ukarabati wa vyuo vitano vya elimu na vyuo vya maendeleo ya wananchi; na kuimarisha vyuo vya *VETA*. Aidha, huduma katika maeneo ya utalii, biashara na fedha zitatiliwa mkazo unaostahili kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Pamoja na kuwepo kwa miradi ya kitaifa ya kimkakati, miradi mingine muhimu inayochangia ukuaji wa uchumi itazingatiwa ambapo miradi itatekelezwa katika: kuimarisha sekta ya elimu na mafunzo; mifugo na uvuvi; afya na maendeleo ya jamii; misitu na wanyamapori; ardhi, nyumba na makazi; hali ya hewa; madini; pamoja na utawala bora; utambulisho wa kitaifa na mchakato wa kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya misitu, Serikali itatekeleza ya programu ya Taifa ya misitu na ufugaji nyuki; mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu; na kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu kwa wananchi, viongozi wa jumuiya zinazosimamia na kuendeleza misitu katika Wilaya mbalimbali za Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanyamapori, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya *Selous Niassa Wildlife Protection Corridor* na *Kilombero and Lower Rufiji Wetland Ecosystem*.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya madini miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu katika taasisi za madini; kuanza ujenzi wa ofisi za madini katika Mikoa ya Katavi, Mtwara na Dodoma; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali za madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ardhi, nyumba na makazi, Serikali itaendelea na mradi wa ujenzi wa mji wa kisasa wa Kigamboni; kuimarisha shughuli za utafiti na maendeleo ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; kuimarisha mipaka saba ya kimataifa na kupima mipaka ya vijiji 100 vilivyoongezeka katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ushirikiano wa kikanda, Jumuiya ya Afrika Mashariki itaendelea na kuimarisha utekelezaji wa Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja ikijumuisha kukamilisha ujenzi wa vituo vya utoaji huduma za pamoja mipakani vya Rusumo/Rusumo, Kabanga/Kobero na Namanga/Namanga na kukamilisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Soko la Pamoja. Aidha, kazi nyingine ni kuanzisha vituo vya mtangamano wa kikanda katika mipaka baina ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kukamilisha majadiliano ya Umoja wa Fedha na mpango kazi wa utekelezaji wa Umoja wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utawala bora, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango kazi wa kitaifa wa kujitathmini katika masuala ya utawala bora *(African Peer Review Mechanism - National Plan of Action, APRM-NPoA)*; maboresho ya sekta ya sheria; mradi wa mapambano dhidi ya rushwa (STACA); mradi wa kuwajengea uwezo Wanasheria katika mikataba na mafunzo kwa vitendo; na kuimarisha na kuboresha mazingira ya kazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi. Aidha, Tume ya kuratibu mabadiliko ya Katiba itaendelea kuchambua maoni ya Mabaraza ya Katiba; kuandaa na kuchapisha Rasimu ya Katiba; kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge la Katiba; na kuchapisha Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Vitambulisho vya Taifa utaendelea kutekelezwa ambapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itaendela na zoezi la kutoa vitambulisho katika Mkoa na Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sensa ya watu na makazi, Serikali itaendelea na kazi ya kuchambua takwimu za sensa na makazi na kutoa machapisho ya sensa kijinsi, umri, na kisekta.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la biashara na masoko, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Mkakati wa Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo *(Commodity Exchange Market);* kuendeleza miundombinu ya masoko ya Mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mpakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda; na kufanyia majaribio Mkakati na Mfumo Mpana wa Unganishi wa Taarifa za Masoko nchini (*IMIS*).

Mheshimiwa spika, utafiti wa nguvukazi nchini (*Intergrated Labour Force Survey)* wa mwaka 2006 umebaini kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira nchini ni asilimia 11.7. Aidha, kiwango cha ukosefu wa ajira mijini ni asilimia 22.3 na vijijini ni asilimia 7.1. Kwa upande wa vijana walio na umri wa miaka 15 hadi 34, kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 13.2. Ili kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana na kuwawezesha vijana kuwa wazalishaji wa fursa za ajira, Serikali itaimarisha mikakati ya kupunguza umaskini na kuongeza ajira ikiwa ni pamoja na kusisitiza yafuatayo:-

(i) Kuongeza tija katika kilimo ili kufanya sekta hiyo kuwa chanzo muhimu cha ukuaji wa uchumi;

(ii) Kuhakikisha kwamba mfumo wa elimu unatayarisha nguvukazi yenye ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira;

(iii) Kutoa msaada *(packaged support)* kwa vikundi vya vijana vinavyojishughulisha na uzalishaji (msaada wa kitaalam, huduma za biashara na mikopo); na

(iv) Kutafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili sekta isiyo rasmi na kuboresha mazingira ya uzalishaji kwa wajasiriamali wadogo, pamoja na kuondoa vikwazo vya kukua kwa mitaji na faida.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kukuza ajira ikiwa ni pamoja na mradi wa kuwezesha wanawake kiuchumi kupitia Benki ya Wanawake Tanzania *(TWB);* Programu ya Ajira kwa Vijana nchini; na kuhamasisha mazingira wezeshi Kisera na Sheria. Serikali itaendelea kuiongezea mtaji benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili kuimarisha upatikanaji wa mikopo na huduma hususan kwa wakulima wadogo wadogo, kuongeza mtaji katika Benki ya Rasilimali nchini *(TIB)* ili kuimarisha huduma ya utoaji mikopo na kuimarisha huduma za upatikanaji wa mikopo kwa kuwawezesha wananchi kupitia mifuko kama vile Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali wadogo (*SELF),* Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo (*NEDF*), Mfuko wa Maendeleo wa Vijana (*YDF*), *SACCOS*, na *VICOBA*. Vilevile, Serikali itashirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Benki ya *CRDB* kuwawezesha vijana walio hitimu elimu ya juu kwa kuwapatia elimu ya ujasiriamali na mikopo yenye masharti nafuu kwa udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja sasa, uchumi wa Taifa umekua kwa wastani wa asilimia saba kwa mwaka lakini umasikini umepungua kwa kiwango kidogo cha takriban asilimia mbili. Hivyo, kwa mwaka 2013/2014, Serikali itachukua hatua zinazolenga kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unapunguza umasikini. Hatua hizo ni pamoja na: (i) Kuwezesha taasisi za wakulima wadogo ili kuinua kiwango cha uzalishaji na ubora wa mazao, mifugo na uvuvi kupitia vyama vya ushirika na kilimo cha mkataba; (ii) Kuhuisha programu na mikakati ya kinga ya jamii (*social protection*), ikijumuisha uhawilishaji fedha kwa masharti maalum (*conditional cash transfers*) kwa walengwa yaani makundi yenye umasikini uliokithiri; (iii) kupanua huduma za fedha vijijini ikijumuisha mikopo na bima, na kuendelea kuwezesha usindikaji wa mazao na upatikanaji wa taarifa za masoko; na (iv) Kuongeza kasi ya kupunguza vikwazo vinavyowakabili wajasiriamali katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014. Katika kugharamia mpango wa maendeleo wa miaka mitano

ilikadiriwa kuwa shilingi trilioni 8.9 zitahitajika kila mwaka, kati ya hizo shilingi trilioni 2.9 zitatokana na fedha za ndani katika bajeti ya Serikali na shilingi trilioni 6.0 zitatokana na uwekezaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imekadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 5.67 sawa na asilimia 31.09 ya bajeti yote kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.69 ni fedha za nje na shilingi trilioni 2.98 ni fedha za ndani. Aidha, Serikali itaendelea kugharamia miradi ya maendeleo kupitia vyanzo vingine vya fedha kama vile, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na utaratibu wa ufuatiliaji kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa mpango na bajeti 2013/2014. Katika utaratibu huo, suala la ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya kimkakati litabaki kuwa jukumu la Tume ya Mipango na Sekta husika na miradi ya ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itakuwa ni jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado kuna changamoto katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo, Serikali imefanya maamuzi ya kuanzisha mfumo mpya wa kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo hapa nchini kwa kutumia uzoefu wa nchi ya Malaysia. Aidha, Serikali imeunda chombo kinachoitwa *President's Delivery Bureau* (*PDB*) ambacho kina majukumu yafuatayo: kupanga na kuendesha shughuli za uchambuzi wa kina wa kimaabara *(labs)* utakaowezesha kupatikana mipango iliyochanganuliwa kwa kina itakayosaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa; kuwezesha kuandaa mikataba ya kupima utendaji wa Mawaziri kwenye miradi na programu za maendeleo katika Wizara zao; kutoa ushauri wa kitalaam kwa Serikali kuhusu maeneo muhimu ya kitaifa; kuishauri Serikali kuhusu maeneo machache ya kipaumbele yenye kuleta matokeo ya haraka kwa kushirikiana na Tume ya Mipango na kusaidia sekta binafsi kuwekeza kwenye maeneo

hayo na vilevile kufanya tathmini huru ya utendaji kwa Mawaziri katika utekelezaji wa maeneo muhimu ya kitaifa yenye kuleta matokeo makubwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Baada ya kuelezea hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo, mwenendo wa ukuaji wa uchumi jumla kwa mwaka 2012 na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/ 2013, ni dhahiri kuwa malengo ya Serikali katika kutekeleza program mbalimbali yamefanikiwa licha ya changamoto iliyopo ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili ukuaji wa uchumi uweze kuwiana na maendeleo kwa kumnufaisha mwananchi wa kawaida kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kusisitiza kuwa masuala yatakayopewa kipaumbele katika kipindi cha mwaka ujao, ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015. Hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi katika viwango vya juu na endelevu inahitajika kuweza kupunguza umaskini wa kipato na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi. Ili kufikia malengo hayo, juhudi zaidi na endelevu zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikujumuisha ukuaji wa Pato la Taifa, kasi ya upandaji bei, na mapato ya ndani;

(b) Kuendeleza uwekezaji katika maeneo machache ambayo yatakuza na kuibua shughuli nyingine za uchumi kwa haraka;

(c) Kuendelea kutekeleza sera na programu zitakazoibua fursa za kiuchumi na kujenga uwezo wa kujikwamua kiuchumi;

(d) Kuendelea kujenga mazingira ya biashara na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika

Kanda Maalumu za Kiuchumi (*SEZs* na *EPZs*) zitakazozalisha bidhaa na huduma bora kwa wingi;

(e) Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika utekelezaji wa sera na mipango ya nchi, ikijumuisha utunzaji na usimamizi endelevu wa mazingira, hususan katika mabonde na maeneo yenye vyanzo vya maji, kupanda na kuitunza miti, kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi; na

(f) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwa kila mwananchi kutii sheria bila shuruti na kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru sekta binafsi kwa kuendelea kuwekeza katika miradi ya maendeleo na kuwa kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi wa Taifa. Aidha, napenda kuwashukuru wote waliotusaidia katika hatua mbalimbali za kufanikisha miradi ya maendeleo. Ninapenda nizitaje baadhi ya nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo: Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*); Mashirika mbali mbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNIDO*, *UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, FAO, WFP* na *WHO*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Mfuko wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Uzalishaji Mafuta (*OPEC Fund*), Shirika la Maendeleo la Norway (*NORAD*), Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*), Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), Shirika la Maendeleo la Finland (*FINNIDA*), Shirika la Maendeleo la Kanada (*CIDA*), Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*), Serikali ya Uswisi, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, China, Afrika ya Kusini, Kuwait, Italia, Korea Kusini, Ireland na nchi zingine marafiki na mashirika mbalimbali ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (*NGO's*). Wote hawa wametoa mchango mkubwa sana katika maendeleo yetu. Aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba washirika wetu wa maendeleo kutusaidia katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bunda kwa kuendelea kuniamini. Nawahakikishia uwakilishi uliotukuka. Pamoja na shughuli nyingi nilizonazo, naendelea kuyapa matatizo ya Jimbo letu kipaumbele cha hali ya juu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, si mnafahamu kwamba baada ya hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mipango, mbona hampigi makofi? Pigeni tu!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana!

Kwa hiyo, baada ya hotuba hii, saa kumi ndiyo ataingia Waziri wa Fedha na kutoa hotuba yake. Waheshimiwa Wabunge kwanza, hiyo saa kumi naomba wote muwahi, maana leo asiyekuwa na kadi haingii *gallery*, ambaye atakuwa hana kadi ya mwaliko basi atakuwa pale chini kwenye *basement,* wanaongia *public gallery* ni wale tu wenye *invitation card.*

Sasa ninyi wageni wamefika halafu sisi tunakuja mmojammoja kwa kuchelewa, hapana, haifanyiki hivyo! Tuwahi kasorobo tunakuwa tumekaa na Waziri wa Fedha *promptly* saa kumi anasoma hotuba yake. Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana muwahi na muwaambie wenzenu.

Nina tangazo lingine kwamba kuanzia leo Wizara ya Fedha imeandaa maonyesho ya hali ya uchumi kwa mwaka

2012 na machapisho mbalimbali ya viashiria vingine vya kijamii katika viwanja vya maonyesho ya Bunge. Kwa hiyo, kuna maonyesho mengine ambayo yameletwa na Wizara ya Fedha mnakaribishwa kupita pale kuanzia leo hii.

Waheshimiwa Wabunge, basi niwatakie mchana mwema mpaka saa kumi, hivyo basi nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

*(Saa 5.58 Asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014.

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014**

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2013/2014. Pamoja na hotuba hii, vimeandaliwa vitabu vinne vya Bajeti vinavyoelezea takwimu mbalimbali za Bajeti. Kitabu cha Kwanza, kinahusu makisio ya mapato; Kitabu cha Pili kinaelezea makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu kinahusu makisio ya matumizi ya kawaida kwa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Kitabu cha Nne

kinaainisha makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013 ambao ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema wote tuliopo hapa na kutuwezesha kushiriki mkutano wa nane wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uongozi wake thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vilevile, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa vikao vya Bunge kwa kuongoza majadiliano vizuri Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mapendekezo ya Bunge ya mzunguko mpya wa bajeti, Serikali imeridhia mapendekezo hayo ambayo yanatoa fursa ya kushirikisha wadau wengi zaidi na kuwezesha utekelezaji wa bajeti kuanza tarehe 1 Julai kila mwaka. Serikali imetekeleza mapendekezo hayo kwa kurekebisha muda na utaratibu wa hatua za uandaaji wa bajeti ambazo zimezingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya mwaka 2013/14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo, Serikali itakuwa inatayarisha Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti mwezi Agosti hadi Oktoba kila mwaka; kuidhinisha na kusambaza Mwongozo mwezi Novemba; kuandaa rasimu za mipango na bajeti za mafungu mwezi Novemba hadi Januari; kufanya uchambuzi wa rasimu za Bajeti na kuingiza takwimu kwenye mfumo wa *IFMS* mwezi Februari; kuwasilisha rasimu za Bajeti pamoja na randama kwenye Kamati za Bunge za Kisekta mwezi Machi; kuchapisha na kuwasilisha Bungeni vitabu vya bajeti mwezi Aprili; kuchambua na kuidhinisha bajeti Bungeni mwezi Aprili hadi

Juni na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zilizoidhinishwa muda wote wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko hayo, Wizara zote zinatakiwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha na kuhitimishwa na hotuba hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninazishukuru Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali walioshiriki kufanikisha matayarisho ya bajeti hii. Kwa namna ya pekee, ninaishukuru Kamati ya Bunge ya Bajeti, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa kuchambua kwa kina bajeti za mafungu yote na kutoa mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naishukuru Kamati Maalum ya Mheshimiwa Spika kuhusu mapendekezo ya mapato ya Serikali; Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara inayoongozwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa (Mb) na Waheshimiwa Wajumbe wengine wa Kamati hiyo pamoja na Wenyeviti wa Kamati nyingine za kisekta kwa ushauri, mapendekezo na maelekezo wakati wakichambua Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri na mapendekezo yao ambayo yamesaidia kuboresha Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa hotuba yake ambayo imefanya majumuisho ya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/13 na kutoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2013/2014. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa kuwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014 aliyoiwasilisha asubuhi hii. Vilevile, ninawapongeza Mawaziri wenzangu kwa kuwasilisha hotuba za bajeti za Wizara zao ambazo zimejumuishwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (Mb) na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb), Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu; Gavana wa Benki Kuu; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato; Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Viongozi wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara; Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wa Wizara ya Fedha na taasisi zake kwa michango yao katika maandalizi ya Bajeti hii.

Ninamshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Fedha wa mwaka 2013 na nyaraka mbalimbali za sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Aidha, ninamshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka zote za Bajeti kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2013/2014 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2010; na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II). Aidha, Bajeti hii inaendelea kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015. Madhumuni ya mipango na mikakati hii ni kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Vilevile, Bajeti hii inalenga kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu kupitia mfumo mpya wa utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ambayo italeta matokeo makubwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira (Mb), kuhusu utaratibu mpya wa uibuaji wa vipaumbele vya Taifa ambavyo vitaleta matokeo makubwa na ya haraka *(Big Results Now –BRN),* Bajeti ya mwaka 2013/2014, imedhamiria kutekeleza maeneo makuu sita yaliyobainishwa kama vipaumbele vya kitaifa. Maeneo hayo ni maji, nishati, uchukuzi, kilimo, elimu na kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutoa taarifa kuhusu mapitio ya utekelezaji wa

bajeti ya mwaka 2012/2013 na mwelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti ya Mwaka 2012/2013. Shabaha na malengo ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 yalijikita katika kukuza Pato halisi la Taifa kwa asilimia 6.8 mwaka 2012; kuongeza mapato ya ndani kufikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 18.0; kudhibiti mfumuko wa bei na hatimaye kuurudisha kwenye kiwango cha tarakimu moja; kuimarisha kiwango cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha pamoja na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kwa asilimia 20 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyozingatiwa katika misingi na shabaha ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa: kuwepo kwa nishati ya umeme wa uhakika na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia; kuimarika kwa utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti; kuimarika kwa mahusiano na Washirika wa Maendeleo; kutekeleza maboresho katika sekta ya umma ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa fedha za umma; kuboresha mazingira ya biashara pamoja na kuongezeka kwa tija na fursa za uwekezaji; kulinda na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za huduma za jamii; kuimarisha utawala bora na uwajibikaji; na kuimarisha utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP).*

Mheshimiwa Spika, Sera za Mapato. Katika mwaka 2012/2013, Sera za mapato zilizotekelezwa na Serikali zililenga kuongeza mapato ya ndani yatokanayo na kodi na yasiyo ya kodi ili kuimarisha uwezo wa Serikali wa kutoa huduma kwa umma na kupunguza utegemezi wa bajeti. Sera zilizotekelezwa zililenga katika kuimarisha taratibu za kukadiria na kukusanya mapato; kuboresha sheria za kodi; kuongeza matumizi ya kielektroniki katika kukusanya kodi; kupunguza misamaha ya kodi na kuwianisha viwango vya kodi na tozo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013, Bunge lilipitisha sera mbalimbali

za kodi ambazo zimetekelezwa na Serikali. Azma ya sera hizo ilikuwa ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa kodi, kuimarisha taratibu za kukusanya mapato pamoja na kupunguza misamaha ya kodi ili kuweza kugharamia kwa kiwango kikubwa matumizi ya Serikali kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa kuzingatia azma hiyo, Serikali imechukua hatua zifuatazo katika eneo la mapato:-

(i) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa kupitia upya mfumo wa ukadiriaji kodi, utoaji wa stakabadhi na leseni, pamoja na kuboresha viwango vya kubakiza maduhuli kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

(ii) Kupanua wigo wa kodi kwa kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo wa kodi;

(iii) Kufanya mapitio ya sheria za Wakala/Taasisi za Umma zinazokusanya maduhuli ili ziweze kuchangia zaidi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(iv) Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo;

(v) Kupitia upya mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo katika Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Miji Midogo ili kuuboresha zaidi;

(vi) Kufanya mapitio ya vyanzo vya mapato na mfumo wa ukusanyaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza mapato; na

(vii) Kujenga uwezo wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na Wakala wa Ukaguzi wa Madini ili kuweza kusimamia ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya madini, gesi na petroli.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji mapato ya ndani. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013, jumla ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 6,717.2, sawa na asilimia 93.2 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 7,209.2 katika kipindi hicho na asilimia 77.1 ya makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 8,714.7. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 6,371.3 ambayo ni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kipindi hicho na asilimia 79.0 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 8,070.1 na mapato yasiyotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 357.8 ikiwa ni asilimia 55.5 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 644.6.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya makusanyo ya mapato ya kodi inaonesha mwenendo wa kuridhisha ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, makusanyo ya ushuru wa forodha yalifikia shilingi bilioni 487.8, sawa na asilimia 84.6 ya kukusanya shilingi bilioni 576.7; mapato kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani yalifikia shilingi bilioni 1,965.5, sawa na asilimia 90.3 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 2,176.4. Kwa upande wa ushuru wa bidhaa, hadi kufikia mwezi Aprili 2013, jumla ya shilingi bilioni 1,050.7 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 90.3 ya kukusanya shilingi bilioni 1,163.1. Kwa upande wa kodi ya mapato kwa makampuni, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 2,381.9 hadi mwezi Aprili, 2013 ambayo ni sawa na asilimia 105.4 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 2,260.7

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa makusanyo ya kodi kulitokana, pamoja na sababu nyingine, na: kuongezeka kwa makusanyo ya kodi ya mapato ya makampuni; kuongezeka kwa kodi ya zuio inayotokana na malipo ya gawio katika makampuni ya madini; na ukusanyaji wa malimbikizo ya kodi. Hatua zingine za kiutawala zilizosababisha kuongezeka kwa mapato zinajumuisha: kuhakikisha mashine za kielektroniki zinatumika ipasavyo; kuendelea kuimarisha mfumo wa kusimamia vitalu vya kodi; kuboresha mfumo wa uthamanishaji bidhaa; kuimarisha ukaguzi wa hesabu za walipa kodi; mapato kutokana na mauzo ya hisa za kampuni ya *M/S BP Tanzania*; kuongezeka

kwa ushuru wa bidhaa wa muda wa maongezi wa simu; na utozaji wa ushuru wa bidhaa katika bidhaa zote zisizo za petroli zinazostahili kutozwa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo, baadhi ya kodi zimeonesha mwenendo usioridhisha tofauti na ilivyotarajiwa, hasa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli na kodi ya mapato inayotokana na ajira. Aidha, uzalishaji katika baadhi ya viwanda ulipungua na hivyo kusababisha makusanyo ya ushuru wa bidhaa na Kodi ya Ongezeko la Thamani kuwa chini ya matarajio. Vilevile, kumekuwa na ongezeko la uingizaji bidhaa kupitia njia zisizo rasmi bila kulipia ushuru na kodi.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yamekuwa hayaridhishi kutokana na: uwezo mdogo wa ukusanyaji na kukosa utaalam, vifaa duni na mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa mapato ambayo inachangia katika upotevu wa mapato. Baadhi ya wakala na Mashirika bado hayachangii ipasavyo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, baadhi ya Idara ambazo zilikuwa vyanzo muhimu zimegeuzwa kuwa Wakala zilizoundwa chini ya Wizara mbalimbali hivyo kupunguza michango yake kwenye mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2013, mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 177.4, sawa na asilimia 49 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 362.2.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo ya nje yenye masharti nafuu. Katika mwaka 2012/2013, Serikali ilikadiria kupata shilingi bilioni 842.5 kama misaada na mikopo ya kibajeti. Hadi kufikia Aprili, 2013, Serikali ilipata misaada na mikopo ya kibajeti ya shilingi bilioni 645.4 ambazo ni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande mwingine, shilingi bilioni 443.4 zilipokelewa kupitia mifuko ya kisekta, ikiwa ni sawa na asilimia 107 ya makadirio ya shilingi bilioni 415.1 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kipindi kilichoishia Aprili, 2013 ilifikia shilingi bilioni 1,235.7 ambayo ni asilimia 65 ya ahadi ya shilingi bilioni 1,899.1 kwa mwaka. Kumekuwepo na changamoto inayotokana na Washirika wa Maendeleo kuchelewa kutoa taarifa wanapotuma fedha moja kwa moja kwenye miradi husika; kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi; ucheleweshwaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi kutoka Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa na Serikali za mitaa; pamoja na mchakato mrefu wa ununuzi, hususan inapohusisha kupata idhini ya mfadhili (*no objection).*

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani. Katika kipindi cha Julai hadi Aprili 2013, Serikali ilikopa shilingi bilioni 1,364.7 kutoka soko la ndani la mitaji kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva pamoja na shilingi bilioni 809.1 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Mwaka 2012/2013 Serikali ilikadiria kupata mikopo yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 1,254.1, sawa na Dola za Kimarekani milioni 800 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika bajeti ya mwaka 2012/2013 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Hadi kufikia Mei 2013, Serikali ilipokea shilingi bilioni 947, sawa na dola milioni 600 kutoka benki ya Stanbic na shilingi bilioni 59.2, sawa na dola milioni 37 kutoka benk ya *Credit Suisse.*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Matumizi. Serikali ilitekeleza Sera za Matumizi kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/13, ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, sera za matumizi zililenga kupunguza nakisi ya bajeti kwa kuwianisha mapato na matumizi; kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma; kusimamia ulipaji wa mishahara; na kuendelea kuhakiki na kulipa madai ya wakandarasi, wazabuni, watoa huduma na watumishi, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikadiria kutumia shilingi bilioni 15,191.9 katika mwaka 2012/13. Mgawanyo wa matumizi ya Serikali katika kipindi hiki ulikuwa kama ifuatavyo: shilingi bilioni 10,597.1 zilitengwa kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4,594.8 zilikadiriwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi hadi kufikia Aprili 2013, matumizi ya kawaida bila kujumuisha malipo ya hatifungani zilizoiva *(rollover)* yalifikia shilingi bilioni 7,582.6, sawa na asilimia 82 ya makadirio ya mwaka. Kati ya kiasi hicho, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma yalikuwa shilingi bilioni 3,209.2 sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 3,781.1.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea na udhibiti wa ulipaji wa mishahara ya watumishi wa umma. Kwa mwaka 2012/2013, Serikali imekamilisha uhakiki wa watumishi na malipo ya mishahara kwenye Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa. Kazi hii ilianza rasmi mwaka 2011/2012 kwa kufanya uhakiki wa watumishi wa Serikali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote. Matokeo ya uhakiki wa watumishi yalisambazwa kwa waajiri kwa ajili ya kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imechukua hatua ya kusambaza mfumo wa malipo kwa waajiri wote ili marekebisho ya mishahara, waajiriwa wapya, kuondoa watumishi wanaomaliza utumishi wao (wanaostaafu, wanaofukuzwa, wanaofariki, wanaocha kazi) yaweze kufanyika mara moja baada ya tukio hilo kutokea kwenye kituo cha kazi. Katika mwaka 2013/2014 Serikali itaendelea na hatua za kudhibiti mishahara ya watumishi, ikiwa ni pamoja na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuendelea kukagua eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutoa kipaumbele katika kulipa Deni la Taifa. Katika kipindi hicho,

malipo ya riba kwa mikopo ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 438.8, sawa na asilimia 79 ya makadirio ya shilingi bilioni 555.2 kwa mwaka. Malipo ya deni halisi la mikopo ya nje yalikuwa shilingi bilioni 79.0, sawa na asilimia 34 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 1,364 kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali za muda mfupi na Hatifungani za Serikali zilizoiva. Vilevile, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 3,000.8 ikiwa ni asilimia 74 ya makadirio ya shilingi bilioni 4,070.9 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2013, jumla ya shilingi bilioni 3,956.3 zilitolewa katika miradi ya maendeleo ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya kutumia shilingi bilioni 4,594.8. Kati ya hizo, fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 2,277.2 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 2,280.6, sawa na asilimia 99.9. Aidha, fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 1,679.1 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 2,314.2 sawa na asilimia 73 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha za umma mwaka 2012/2013, Serikali ilianza kutekeleza mpangokazi wa miaka mitano wa kuiwezesha Serikali Kuu kuandaa hesabu kwa viwango vipya vya uhasibu vya Kimataifa (*IPSAS Accrual Basis*). Kwa mara ya kwanza, hesabu za Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 zitaandaliwa kwa kutumia viwango hivyo. Wizara imeandaa miongozo mbalimbali na kufanya mikutano elekezi ili kuwajengea uwezo wa uelewa Wahasibu na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti mapato na matumizi, Serikali imeandaa na kutoa miongozo ya usimamizi wa vihatarishi katika sekta ya umma pamoja na mwongozo wa uhakiki wa ubora wa ukaguzi wa ndani. Serikali pia imetayarisha mwongozo wa ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa ambao unategemea kuanza kutumika rasmi Julai, 2013. Miongozo hiyo ina lengo la kuboresha utendaji kazi wa ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya watumishi. Mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kulingana na uwezo wa mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kumudu gharama za maisha. Maeneo ambayo yalitiliwa mkazo ni pamoja na ongezeko la mshahara hasa kima cha chini, kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwenye mishahara, malipo ya mshahara kwa wakati na kuhakikisha watumishi wanalipwa mafao yao mara baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Utekelezaji wa MKUKUTA II umeonesha mafanikio katika maeneo mengi ingawa bado kuna changamoto. Mafanikio hayo ni pamoja na kuendelea kukua kwa pato la Taifa, kuongezeka kwa mapato ya kodi, kukua kwa sekta ya fedha na mikopo kwa sekta binafsi, kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya Serikali na kuimarika kwa utoaji na upatikanaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutathmini hali ya umaskini hapa nchini, Serikali imefanikiwa kukamilisha zoezi la ukusanyaji wa takwimu za Utafiti wa Hali ya Mapato na Matumizi katika kaya binafsi ya mwaka 2012. Uchambuzi wa takwimu hizo unaendelea na unatarajia kukamilika kabla ya Desemba 2013. Aidha, takwimu za Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika 2012, na Utafiti wa Hali ya Ajira na Kipato wa mwaka 2012 vitafanyiwa uchambuzi wa kina ili kutuwezesha kupata takwimu zitakazoonesha hali ya umaskini katika ngazi mbalimbali. Tafiti hizi zitatoa matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA katika nguzo ya kwanza ya Kupunguza Umaskini na Ukuaji wa Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nguzo ya pili ya MKUKUTA ya kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii, viashiria vingi vilionesha mabadiliko chanya. Viwango vya uandikishaji katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari vimeimarika. Aidha, uandikishaji katika ngazi ya vyuo vya ufundi na elimu ya juu uko katika kiwango cha kuridhisha. Matokeo haya yanatokana na utekelezaji wa juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya

shule, vyuo, Walimu, upanuzi wa miundombinu ya ufundishaji na kuongezeka kwa mikopo ya elimu ya juu. Changamoto iliyopo ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza katika ngazi zote. Katika mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea pia kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za afya, lishe, upatikanaji wa maji safi na salama na utoaji elimu kwa umma kuhusu kinga ya malaria na athari za ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mali za umma, kuimarisha mfumo wa sheria na haki za binadamu, hususan katika ngazi za chini kwa kuongeza idadi ya mahakimu. Hatua hii imeboresha kasi ya utoaji maamuzi ya mashauri katika Mahakama zetu. Aidha, programu ya maboresho ya sekta ya sheria nayo iliendelea kutekelezwa, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa haki za raia zinaboreshwa na kulindwa, hususan wale walio katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi. Katika mwaka 2012/2013, Serikali ilifanya Sensa ya Watu na Makazi kama ilivyopangwa ambapo jumla ya shilingi bilioni 127.3 zilitumika. Matokeo ya sensa hiyo, yalibainisha kuwa Tanzania ina jumla ya watu milioni 44.9 sawa na ongezeko la asilimia 2.6 kwa mwaka ikilinganishwa na matokeo ya sensa ya mwaka 2002 ambapo ongezeko lilikuwa asilimia 2.9.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ongezeko la idadi ya watu ni kubwa kwa mikoa ya Dar es Salaam na Mjini Magharibi ambapo kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni asilimia 5.6 kwa mwaka, wakati Mjini Magharibi kasi hiyo ni asilimia 4.2. Aidha, Mkoa wa Dar es salaam una idadi kubwa ya watu ikilinganishwa na Mikoa mingine ukiwa na asilimia 10 ya idadi ya wakazi wote wa Tanzania Bara. Vilevile, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa mwaka 2012 umebakia karibu sawa na ule wa mwaka 2002. Wastani ulikuwa watu 4.9 kwa kaya mwaka 2012 ikilinganishwa na watu 4.8 mwaka 2002. Napenda niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inatumia takwimu

za sensa hii katika kuandaa sera, mikakati, mipango na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati na mipango yake. Nashauri wadau wengine wafanye hivyo pia wakati wa kuandaa mipango ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na uchambuzi wa kina wa matokeo ya Sensa ambayo yatahusisha viashiria vya kiuchumi na kijamii. Napenda nitumie nafasi hii kuwajulisha kuwa toleo linalofuata ni la mgawanyo wa watu kwa umri na jinsia katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ambalo litatolewa mwezi Julai, 2013. Matokeo yanayofuata ambayo yanahusu viashiria vya kiuchumi na kijamii yataendelea kutolewa kama yalivyoanishwa kwenye ratiba ya usambazaji na pia katika tovuti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha. Serikali iliendelea kutekeleza progamu ya maboresho ya sekta ya fedha ili kuhakikisha kwamba sekta hii inachangia kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kukuza Pato la Taifa. Katika mwaka 2012, huduma ya sekta ya fedha ilichangia asilimia 1.8 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2011. Aidha, katika kipindi hicho, sekta ya fedha ilikua kwa asilimia 13.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.7 mwaka 2011. Ongezeko hilo lilitokana na mafanikio ya utekelezaji wa maboresho ya sekta ya fedha ambayo yaliwezesha kuongezeka kwa idadi ya benki kutoka 49 Februari, 2012 hadi 51 Februari, 2013; kampuni za bima kutoka 26 mwaka 2011 hadi 28 mwaka 2012; na idadi ya *SACCOS* kutoka 5,424 Machi, 2012 hadi 5,559 Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi nchini ambapo Benki Kuu iliongeza mauzo ya fedha za kigeni katika soko la fedha za kigeni pamoja na mauzo ya dhamana za Serikali. Aidha, Benki Kuu ilipandisha kiwango cha chini cha fedha zinazotakiwa kuhifadhiwa Benki Kuu kwa ajili ya akiba ya amana za Serikali katika mabenki kutoka asilimia 30 hadi asilimia 40, pamoja na kupunguza kiwango cha kuhodhi fedha za kigeni kulingana na mitaji yao kwa mabenki kutoka

asilimia 10 hadi asilimia 7.5 kuanzia Desemba, 2012. Hatua hizo zilisaidia katika kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei usiojumuisha chakula na nishati (*core inflation*) kutoka asilimia 8.7 Mei, 2012 hadi asilimia 7.1 Mei, 2013. Vilevile, hatua hizi zilisaidia kuimarika kwa kiwango cha ubadilishanaji wa shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya utafiti wa huduma ndogo ndogo za bima kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi walio wengi. Utafiti umebaini kwamba kiwango cha matumizi ya huduma za bima bado ni kidogo, ambapo ni asilimia 19 tu ya watu wazima wanatumia huduma hizo (hii inajumuisha huduma za bima ya afya zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya). Utafiti umebaini pia kwamba uhitaji wa huduma ndogo ndogo za bima ni mkubwa na upatikanaji wa huduma hizo utasaidia katika juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Serikali iliendelea kuwahamasisha wananchi ili waone umuhimu wa kujiunga na huduma za bima.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* ili kuwezesha benki kutoa mikopo ya nyumba. Ili benki ziweze kupata mikopo hiyo, zinapaswa ziwe na hisa kwenye kampuni hiyo. Hadi kufikia Desemba 2012, benki 12 zimenunua hisa, Serikali kupitia Kampuni ya *TMRC* ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.2 kwa benki 12 wanachama, ambazo zilitoa mikopo 1,799 yenye thamani ya shilingi bilioni 106.2.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma ya Serikali ya kuimarisha usimamizi na maendeleo ya Sekta ya Fedha, Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa kuanzisha Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha ambayo ndani yake kutakuwa na kitengo cha kusimamia sekta ya huduma ndogo ndogo za fedha na kitengo cha sera za sekta ya fedha. Muundo huu mpya kwa sasa uko katika hatua ya kuridhiwa. Miongoni mwa majukumu ya idara hii ni kuandaa sera ya sekta ya huduma ndogo ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uanzishwaji wa benki za wananchi, Benki Kuu imekuwa ikitoa masharti nafuu yanayohusu mtaji wakati zinapoanza. Kwa mfano, wakati benki za biashara zinatakiwa kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 15, benki za wananchi zinatakiwa kuwa na shilingi bilioni mbili. Kwa upande mwingine, Serikali imekuwa ikihimiza uanzishwaji wa *SACCOS, VICOBA* na benki za wananchi ili kuwawezesha wananchi kupata mitaji kwa ajili ya biashara na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa umma. Bunge lako Tukufu limetunga Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 baada ya kubaini upungufu uliokuwepo katika Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004. Aidha, Bunge lako pia limetunga Sheria ya Ubia Na. 19 ya mwaka 2010 ambayo utekelezaji wake katika hatua ya kumpata mbia unatumia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hivyo kuna haja ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 ili kuzingatia maboresho na mabadiliko yanayohitajika.

Mbali na kuleta uwiano wa Sheria ya Ununuzi na Sheria ya Ubia, maboresho yanalenga kuweka misingi imara ya taratibu za kusimamia ununuzi wa umma; kufafanua majukumu ya Mamlaka za usimamizi wa ununuzi wa umma; na kuongezea madaraka ya kiutendaji Taasisi za ununuzi na zile zinazosimamia ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, maboresho yanalenga kupunguza muda wa kushughulikia malalamiko ya wazabuni na kupunguza muda wa mchakato wa ununuzi. Serikali inakusudia kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004, mara baada ya mabadiliko ya Sheria Na. 7, narudia, Serikali inakusudia kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004 mara baada ya mabadiliko ya Sheria Na. 7 kukamilika na Kanuni mpya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ubia Kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Serikali imeendelea kusimamamia sera yake ya

kushirikisha sekta binafsi ili iweze kuongeza Pato la Taifa. Katika mwaka 2012/2013, Serikali ilifanya uchambuzi wa awali wa baadhi ya miradi ya *PPP* katika sekta za ujenzi wa barabara na bandari. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze, bandari ya Katanga, bandari ya Mwambani, na bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Ubia ya mwaka 2010, changamoto iliyojitokeza ni kuwepo kwa vitengo na ofisi nyingi zinazoshughulikia masuala ya *PPP*. Kwa kutambua hili, Serikali katika mwaka 2013/2014 itaunganisha vitengo vya *PPP* na kufanya mapitio ya sheria na kanuni za ubia kwa nia ya kufanya maboresho. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Serikali imepanga kuanzisha mfuko maalumu utakaotumika kugharamia upembuzi yakinifu ili kuendeleza miradi ya ubia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine kuzungumzia deni la Taifa. Hadi mwishoni mwa Machi 2013, deni la Taifa (likijumuisha deni la umma na sekta binafsi) lilikuwa shilingi bilioni 23,673.53 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 20,276.6 Machi 2012 likiwa ni ongezeko la asilimia 17. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 18,282.02 ni deni la nje na shilingi bilioni 5,397.50 ni deni la ndani. Deni la nje, linajumuisha deni la umma la shilingi bilioni 15,203.34 na deni la sekta binafsi ni shilingi bilioni 3,078.69.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha deni la nje kinajumuisha deni halisi shilingi bilioni 16,087.43 na malimbikizo ya riba ya shilingi bilioni 2,194.59. Deni la ndani linajumuisha hati fungani za muda mrefu kiasi cha shilingi bilioni 4,261.03 na dhamana za Serikali za muda mfupi kiasi cha shilingi bilioni 1,136.48. Mikopo hiyo iligharamia miradi ya maendeleo, narudia, mikopo hiyo iligharamia miradi ya maendeleo hususan miundombinu kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhimilivu wa Deni la Taifa. Serikali inasimamia deni la taifa kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Deni la Taifa pamoja na Sheria ya Mikopo,

Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Kwa kuzingatia Sheria hiyo, mwaka 2012, Serikali ilifanya tathmini ya kuangalia uhimilivu wa deni la Taifa. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, viashiria vyote vya kupima uhimilivu wa deni vilivyokubalika kimataifa vinaonesha kuwa, deni la Taifa ni himilivu katika muda mfupi na muda wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mathalani, uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Taifa kwa Pato la Taifa ni asilimia 18.9, ikilinganishwa na ukomo wake wa asilimia 50 na kiashiria cha uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Taifa kwa mapato yanayotokana na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ilikuwa asilimia 53.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 200 kwa *standard* za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni. Serikali imepiga hatua kubwa katika kufanikisha zoezi la nchi kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni na ipo kwenye hatua ya kupata kampuni za kufanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, kazi hii imepangwa kukamilika mwaka 2013/2014 ambapo itawezesha nchi kukopa kwa gharama nafuu katika masoko ya fedha ya kimataifa kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu. Aidha, kampuni za Tanzania nazo zitaweza kupata mitaji kwa urahisi zaidi kutoka kwenye masoko ya mitaji ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kiuchumi wa Kikanda. Serikali imeendelea kuimarisha ushiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa *(SADC).* Ushiriki wetu katika jumuiya hizi ni mojawapo ya mkakati wa kuhakikisha tunaitumia jiografia ya nchi yetu kwa kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umefikia hatua ya kuanzisha Umoja wa Fedha na majadiliano ya Itifaki hiyo yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika mwezi Novemba 2013. Aidha, hatua zinachukuliwa

za kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja ambapo yameainishwa maeneo katika sheria zetu yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha ushiriki wa nchi katika soko hili.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Sheria zitakazorekebishwa ni zile zinazohusika na taratibu za kuwezesha watanzania kuwekeza mitaji yao katika nchi za Jumuiya; lengo likiwa kurahisisha biashara ya mitaji na huduma ili kuchochea uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo wa *SADC*, ambapo taratibu za kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya *SADC* zimekamilika. Itifaki hii itarahisisha taratibu za uwekezaji katika nchi za *SADC*, kuwezesha nchi za *SADC* kuwianisha sera za kodi hasa eneo la vivutio vya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kupitia Itifaki hii, nchi za *SADC* zitaweza kubuni na kutekeleza sera za kuimarisha uchumi na fedha kwa pamoja kwa lengo la kuwa na utulivu wa uchumi katika ukanda huu na hivyo kuvutia uwekezaji. Ili kuhakikisha azma hii inatekelezwa kwa vitendo, nchi za *SADC* zinakamilisha utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013. Mafanikio na changamoto za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2012/2013 kwa kila sekta yameelezwa kwa kina katika hotuba za bajeti za Wizara husika ambazo Bunge lako Tukufu limepata fursa ya kuzijadili na kuzipitisha. Kwa kuzingatia hilo, nitaeleza kwa kifupi baadhi ya mafaniko na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato. Bajeti ya mwaka 2012/2013 ilitekelezwa kwa mafanikio, hususan katika ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi; utoaji wa huduma za jamii; kuimarisha ulinzi na usalama, pamoja na utengamano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, hususan mapato ya kodi kutoka wastani wa shilingi bilioni 540 kwa mwezi kwa mwaka 2011/2012 hadi shilingi bilioni 640 kwa mwezi kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wastani huo wa mwezi, kiwango cha juu cha makusanyo kilifikiwa mwezi Desemba 2012, ambapo makusanyo ya kodi na yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 890. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi. Pato la Taifa limeendelea kuimarika mwaka 2012 ambapo ukuaji halisi ulikuwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2011. Ongezeko hili la ukuaji lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano, pamoja na kuimarika kwa uzalishaji viwandani kutokana na jitihada za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika sambamba na matumizi ya nishati mbadala katika uzalishaji viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano ndiyo ilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa asilimia 20.6 mwaka 2012. Pamoja na kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji, sekta ya mawasiliano ilichangia asilimia 2.3 tu katika Pato la Taifa ikilinganishwa na sekta ya kilimo ambayo pamoja na kukua kwa kiwango kidogo ilichangia asilimia 24.7 katika Pato la Taifa mwaka 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wamejikita katika shughuli za kilimo, hivyo hii ni sekta ambayo serikali inaitilia mkazo ili kuhakikisha kuwa inaleta mafanikio yanayotarajiwa nawengi, ikiwemo kupunguza umaskini. Serikali imefanya jitihada kubwa za kuboresha sekta hii lakini bado imeendelea kukua kwa kiwango kisichozidi asilimia tano kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha sekta ya kilimo ili ikue kwa kasi zaidi na kuongeza

kipato na hivyo kupunguza umaskini kwa wananchi walio wengi. Juhudi hizo zinahusisha kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua; kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa wakati zikiwemo mbolea, dawa na mbegu bora; kuondoa kodi katika zana mbalimbali za sekta ya kilimo ili kuongeza tija; kuimarisha masoko ya mazao, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na uhifadhi; na kuimarisha barabara vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendeleza juhudi za upatikanaji wa umeme na maji vijijini. Vilevile, Serikali itaimarisha sekta nyingine za kiuchumi zenye kutoa ajira kama vile sekta za ujenzi na uzalishaji viwandani, pamoja na kupanua wigo wa kinga ya jamii ili kuongeza ushiriki wao kwenye shughuli za uchumi na hivyo kuinua Pato la wananchi na kuongeza kasi ya kupunguza umaskini wa kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei. Wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2012 uliongezeka kwa asilimia 16.0 ikilinganishwa na asilimia 12.7 mwaka 2011. Upandaji huu wa bei ulitokana hasa na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia na kupanda kwa bei za chakula kulikotokana na mahitaji makubwa ya chakula katika baadhi ya nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba chakula peke yake huchangia asilimia 47.8 ya bidhaa na huduma zinazotumika katika ukokotoaji wa fahirisi ya bei kwenye kapu la bidhaa za walaji, ikifuatiwa na usafiri (asilimia 9.5) na nishati (asilimia 9.2).

Mheshimiwa Spika, makundi haya ni muhimu sana katika kuchochea mwelekeo wa bei za bidhaa na huduma mbalimbali. Katika kukabiliana na kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, Serikali ilichukua hatua kadhaa zikiwemo:-

(i) Kuhakikisha kuwa kunakuwa na ugavi mzuri wa chakula unaoendana na mahitaji nchini. *(Makofi)*

(ii) Kupanua kilimo cha mazao ya chakula na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea, madawa na mbegu bora. *(Makofi)*

(iii) Kuimarisha miundombinu ya usafirishaji. *(Makofi)*

(iv) Kuimarisha upatikanaji wa umeme. *(Makofi)*

(v) Kupandisha kiwango cha riba ya Benki Kuu inayotozwa kwa mikopo iendayo kwa taasisi za fedha nchini kutoka asilimia 7.58 hadi asilimia 12.58.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ziliwezesha kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei kutoka asilimia 18.2 mwezi Mei 2012 hadi asilimia 8.3 mwezi Mei 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika sekta mbalimbali. Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 826.1 kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa umeme na kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ikijumuisha ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi Kinyerezi; kukamilisha ujenzi na kuanza kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito katika vituo vya Ubungo - Dar es Salaam (MW 105) na Nyakato - Mwanza (MW 60); kuendeleza miradi ya umeme vijijini katika mikoa 16; na kuendeleza upembuzi yakinifu katika miradi ya Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Liganga. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba 2012, kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Grid ya Taifa kilikuwa MWh 5,759,756 ikilinganishwa na MWh 5,153,400 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 11.8.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji iliendelea kupewa kipaumbele katika mwaka 2012/2013 kwa kuendeleza ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 682 kupitia mpango wa vijiji kumi kwa kila Halmashauri; uboreshaji wa mamlaka za maji mijini;

na ujenzi wa miundombinu ya maji, ikiwemo bomba la maji la Ruvu Chini hadi Dar es Salaam. Ili kutekeleza miradi ya maji, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 106.6 katika ngazi ya Wizara na shilingi bilioni 98.4 katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 537.40 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya tiba, kinga na ustawi wa jamii. Fedha hizo pia zilitumika katika kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya; kuimarisha stadi na kujenga uwezo wa rasilimali watu; na kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya, Mlonganzila - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 2,421.5 katika sekta ya elimu kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali katika shule za msingi, sekondari, elimu ya watu wazima, vyuo vya ufundi stadi, na vyuo vya elimu ya juu. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ulipaji wa mishahara kwa wakati; kuajiri walimu wapya 27,773 (Walimu 13,633 wa shule ya msingi, 14,060 wa sekondari na 80 wa vyuo vya ualimu) na kuwalipa stahili zao; kugharamia uendeshaji mashuleni (*capitation*); kutoa mikopo kiasi cha shilingi bilioni 326.1 kwa wanafunzi 96,350 wa elimu ya juu; kuanza ujenzi wa maabara katika shule mbili kwa kila Halmashauri 132 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 102.3 kimetolewa; ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada 27,159,106 kwa ajili ya shule za msingi; na kuendelea kuboresha miundombinu ya kutolea elimu katika ngazi zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 1,044.2 kwa ajili ya kujenga na kukarabati barabara za lami; kufanya matengenezo maalumu na ya kawaida kwenye barabara za changarawe; kuboresha barabara za wilaya pamoja na kujenga na kukarabati madaraja. Aidha, fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vivuko vitatu na maegesho; kukarabati vivuko vitano; na kufanya upembuzi yakinifu wa kujenga barabara na vivuko katika maeneo mengine nchini. Vilevile, Serikali iliendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara za Dar es Salaam na miji mingine mikuu ili kupunguza msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uchukuzi ilipewa jumla ya shilingi bilioni 181.8 kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo: kuanzisha usafiri wa treni ya abiria jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari na adha ya usafiri jijini Dar es Salaam; kuboresha na kurejesha huduma za treni za abiria na mizigo katika reli ya kati na *TAZARA*; na kuendeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Songwe, Katavi, Mwanza, Kigoma na Tabora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha utawala bora, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 27.0 kwa ajili ya mchakato wa marekebisho ya Katiba ikiwa ni pamoja na kukusanya kura za maoni katika mikoa yote 30 ya Tanzania Bara na Zanzibar na shilingi bilioni 40 kutekeleza mradi wa vitambulisho vya Taifa. Aidha, shughuli zingine muhimu zilizotekelezwa ni kukamilisha rasimu ya awali ya katiba mpya, kuchapisha nakala za rasimu ya katiba mpya na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali nchini pamoja na kuendesha mikutano ya Mabaraza ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu wa chakula kwenye baadhi ya maeneo nchini, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 42.87 mwaka 2012/2013 zilizotumika kununua tani 53,269.70 za nafaka kwa ajili ya kuongeza chakula cha hifadhi ya Taifa. Aidha, Serikali ilisambaza chakula cha msaada kwa wananchi wenye mahitaji katika Halmashauri 47 na kuuza jumla ya tani 16,653 kwa wasagishaji wa nafaka ili kurahisisha usambazaji wa unga wa sembe na hatimaye kupunguza mfumuko wa bei nchini. Vilevile, uzalishaji wa chakula katika msimu wa mwaka 2012/13 ulifikia tani milioni 13.34 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 11.97.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, changamoto bado ni nyingi, ambazo ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na upatikanaji wa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara kwa wakati na hivyo kuchelewa kupeleka fedha kwenye sekta husika. Changamoto nyingine ni: madai ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma wa

ndani na nje; kuimarisha miundombinu; kupata thamani ya fedha katika ununuzi wa umma; kuongeza ubora na tija katika uzalishaji; kutumia fursa za kijiografia katika ukuzaji wa uchumi; upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika; riba za mikopo; kusimamia deni la Taifa; kudhibiti mfumuko wa bei na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni: huduma za jamii hususan elimu, afya, na maji bado hazijafikia viwango vinavyotarajiwa; kuongeza fursa za ajira; kukuza ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi *(PPP);* na upatikanaji wa huduma za mikopo ya kilimo. Changamoto hizo zitaendelea kutafutiwa ufumbuzi hatua kwa hatua katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Aidha, Serikali imejipanga kukabiliana na baadhi ya changamoto hizi katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2013/2014. Bajeti ya mwaka 2013/2014 itazingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye: Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014 na mfumo mpya wa utekelezaji wa vipaumbele vyenye matokeo makubwa na ya haraka (*Big Results Now – BRN*); Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na programu za maboresho katika sekta ya umma. Lengo likiwa ni kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya bajeti kwa mwaka 2013/2014. Bajeti ya mwaka 2013/2014, imejielekeza katika kufikia shabaha na malengo ya uchumi jumla yafuatayo:-

(i) Pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.0 mwaka 2013, na asilimia 7.2 mwaka 2014. *(Makofi)*

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ibaki kwenye viwango vya tarakimu moja, ambapo mfumuko

wa bei unatarajiwa kushuka zaidi kufikia asilimia 6.0 Juni 2014. *(Makofi)*

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 20.2 mwaka 2013/14 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 17.7 kwa mwaka 2012/13. *(Makofi)*

(iv) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 5.0 ya Pato la Taifa mwaka 2013/14. *(Makofi)*

(v) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi *(M3)* katika wigo wa asilimia 15.0 Juni 2014 utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei.

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne mwaka 2013/2014.

(vii) Kupunguza tofauti ya viwango vya riba vya kuweka na kukopa. *(Makofi)*

(viii) Kuimarisha thamani ya shilingi na kuwa na kiwango imara cha ubadilishanaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misingi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2013/2014. Ili kufikia malengo yaliyoainishwa hapo juu, misingi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 ni hii ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarisha na kudumisha amani, usalama, utulivu na utengamano. Ni imani ya Chama

kinachotawala, Serikali iliyopo madarakani kwamba tusipokuwa na amani, usalama na utulivu, haya niliyoyasema hapa juu ni vigumu kuyapata. *(Makofi)*

(ii) Kuendelea kuboresha viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii vikiwemo Pato la Taifa, biashara ya nje, fedha, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii.

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipya vya mapato. Kwa nafasi hii, napenda kuwashukuru timu ya Waheshimiwa Wabunge iliyochangia mawazo makubwa katika eneo hili. *(Makofi)*

(iv) Kuboresha usimamizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

(v) Kuimarisha mfumo wa *IFMS* na kuhakikisha unatumika kuweka mihadi ya huduma na bidhaa kabla ya malipo.

(vi) Kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano hasa vipaumbele vyenye matokeo makubwa na ya haraka pamoja na MKUKUTA II.

(vii) Kuboresha mfumo wa utekelezaji wa vipaumbele na uwajibikaji. *(Makofi)*

(viii) Kuendelea kuimarisha sera za fedha ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti ya riba za amana na za mikopo.

(ix) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa Tanzania. Huu ni wakati wa kuboresha uwekezaji wa sekta binafsi, tukitaka uchumi uendelee kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera za Mapato. Katika mwaka 2013/2014, Serikali inakusudia kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi. Sera za mapato zinajumuisha kupanua wigo wa kodi kwa kubainisha vyanzo vipya na kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vilivyopo. Aidha, hatua zaidi zitachukuliwa kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi. Tunalenga misamaha ya kodi ile isiyo na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, sera na hatua zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014, zinalenga kuimarisha uwezo wa Serikali kukusanya mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi kutoka nje na kupunguza kutegemea kodi zinazotokana na biashara za kimataifa ambazo zimeanza kushuka kutokana na kuongezeka kwa biashara za ushirikiano wa kikanda katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikakati ya pamoja ya kuongeza mapato ya Serikali, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa hatua uliyochukua ya kuunda Kamati ya Spika ili kuishauri Serikali kuhusu vyanzo vya mapato ambapo baadhi ya mapendekezo yake yamezingatiwa katika Sera za Mapato kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itatekeleza baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na *Labs* ya kubuni vyanzo vya mapato. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kuanza kuuza vitalu vya misitu na uwindaji kwa njia ya mnada na kufanya tathmini ya mali na ardhi ili kuimarisha makusanyo ya tozo ya mali na kodi ya ardhi. Hatua nyingine za kumairisha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi tayari zimeshatangazwa kupitia bajeti za Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2013/14, itatekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kupunguza utegemezi. Moja ya hatua muhimu itakayotekelezwa katika mwaka 2013/14 ni kuangalia upya misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza kama nilivyosema awali. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kupunguza misamaha ya kodi kwa kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za utalii. Aidha, Sheria ya Uwekezaji itafanyiwa marekebisho ili kupunguza misamaha ya kodi na kubakiza misamaha yenye tija tu na yenye kuchochea uwekezaji mkubwa katika sekta ya uchumi;

(ii) Kuendelea kuunga mkono jitihada za kuanzisha kituo kimoja cha kutoa huduma bandarini *(one stop centre)* katika bandari. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuanzisha *One Stop Border Posts* katika mipaka kwenye vituo vya Holili, Mutukula, Sirari, Horohoro, Kabanga, Tunduma, Rusumo na Namanga;

(iii) Kuendelea kuwajengea uwezo Watumishi wa Serikali wakiwemo wa Mamlaka ya Mapato ili kupata ujuzi wa kudhibiti mbinu za kukwepa kodi zinazotumiwa na makampuni makubwa hasa katika sekta za mawasiliano, madini na gesi, ukiwemo ujuzi wa kukagua uhamishaji wa gharama, yaani *transfer pricing* hivyo kudhibiti mianya ya kupotea kwa mapato yetu;

(iv) Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inaendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kieletroniki za kutoa risiti *(Electronic Fiscal Devices - EFDs),* ambazo zimeunganishwa moja kwa moja na Mamlaka kwa mtandao wa kompyuta ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mapato yake stahiki, tutafuatilia na kuona utaratibu huu unafanikiwa. Aidha, Mashine hizi zinasimamiwa kupitia mtandao wa kielektroniki ambapo hupeleka moja kwa moja taarifa kwenye hifadhi kuu ya Mamlaka kila siku;

(v) Kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi, hususan katika sekta ya gesi, mafuta na madini ili kusimamia ipasavyo mapato yatokanayo na rasilimali zetu; na

(vi) Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania itaanzisha mfumo mpya ujulikanao kama *Revenue Gateway* ambao utaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai, 2013. Mfumo huu unalenga kuboresha mifumo iliyopo ya ulipaji kodi na upatikanaji wa taarifa za malipo ya kodi kwa njia ya mtandao. Aidha, mfumo huu utarahisisha uhamishaji wa fedha kutoka kwenye benki za biashara hadi Mfuko Mkuu wa Serikali. Vilevile, mlipakodi atalazimika kujisajili kwa ajili ya kufanya malipo kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kabla ya kulipa kupitia mfumo wa Tanzania *Interbank Settlement System (TISS)*. Mtumiaji wa mfumo huu atanufaika kwa kupata taarifa kwa njia ya barua pepe kuhusu malipo yake ya kodi aliyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, Sera za mapato katika mwaka 2013/14, zinalenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 11,154.1, hii ikiwa ni sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni shilingi bilioni 10,412.9 na mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 741.1. Mapato yanayotokana na vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 383.5, sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado ina changamoto ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa kutegemea mapato ya ndani. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali itakopa kutoka soko la ndani shilingi bilioni 552.3, sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, katika mwaka 2013/14, Serikali itakopa shilingi bilioni 1,147.6 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali za muda mfupi zinazoiva.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya misaada na mikopo ya masharti nafuu. Washirika wa Maendeleo

wamekuwa wakichangia katika bajeti ya matumizi ya maendeleo. Katika mwaka 2013/14, Serikali inatarajia kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kiasi cha shilingi bilioni 3,855.2 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 1,163.1; misaada na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 2,191.6; na mifuko ya kisekta ni shilingi bilioni 500. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia matumizi ya fedha za Washirika wa Maendeleo na kuhakikisha zinaleta ufanisi na tija katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi zao za kuchangia maendeleo yetu, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo yetu kama ifuatavyo: Nchi za Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Ireland, Italia, Japani, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi, pia taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, *BADEA, Global Funds, OPEC Fund, Saudi Fund*, Umoja wa Ulaya, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kwa pamoja tunawashukuru sana na tunathamini michango yao waliyotusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/14 na changamoto za upatikanaji wa mapato ya ndani, Serikali itakopa kutoka nje mikopo yenye masharti nafuu ya kibiashara shilingi bilioni 1,156.4, sawa na Dola za Marekani milioni 700. Mikopo hiyo itatumika kugharamia miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/14. Uamuzi wa kuendelea kukopa kwa masharti nafuu ya kibiashara unazingatia uhimilivu wa Deni la Taifa uliopo na kunufaisha uchumi ili uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Serikali itatekeleza Sera za Matumizi kama ifuatavyo:-

(i) Kuwianisha matumizi na mapato yanayotarajiwa; tutumie tunachopata kwa malengo tuliyoweka kwenye Bajeti;

(ii) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haitazidi asilimia 5.0 ya Pato la Taifa;

(iii) Mafungu yatazingatia viwango vya matumizi vitakavyoidhinishwa na Bunge;

(iv) Kutenga fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo kwa mujibu wa Bajeti iliyoidhinishwa; na

(v) Kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida kwa mwaka 2013/14 yanalenga katika kufanikisha maeneo yafuatayo:-

(i) Kugharamia nyongeza ya mishahara pamoja na kulipa mishahara kwa wakati;

(i) Kuboresha huduma za kiuchumi na maendeleo ya kijamii; kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kuendelea na utoaji wa vitambulisho vya Taifa hayo tutagharamia;

(iv) Kukamilisha uchambuzi wa takwimu za sensa ya watu na makazi;

(v) Maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015; na

(vi) Kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje

yaliyoiva pamoja na madai mbalimbali ya watumishi na wazabuni yaliyokwishahakikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/13, Serikali ililenga kupunguza matumizi yasiyo ya lazima katika maeneo mbalimbali kama vile semina, usafiri wa ndani na nje, ununuzi wa samani, maonesho mbalimbali na katika magari. Matokeo ya hatua hizi yameleta mafanikio kadhaa ikiwemo yafuatayo: Semina na warsha zimepunguzwa; manunuzi ya magari mapya yamepunguzwa na yananunuliwa kwa kibali cha Mheshimiwa Waziri Mkuu tu na ukubwa wa injini umepunguzwa na kubaki zenye ukubwa uliokubalika (*cc 3,000* au chini ya hapo); maonesho pia yamepunguzwa; mfano, Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma hayakufanyika mwaka 2012/13; ununuzi wa samani kutoka nje nao umepungua.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Serikali itaendelea kudhibiti matumizi yake katika maeneo mbalimbali ikiwemo kutumia malipo ya simu kabla ya huduma; kutumia utaratibu wa ununuzi wa magari (*under bulk procurement)* kwa pamoja, ambao utapunguza gharama za ununuzi; kupunguza matumizi ya magari ya Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha magari Watumishi wa Serikali wanaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale maafisa hawa watakapokuwa wamenunuliwa magari, hawataruhusiwa kutumia magari ya Serikali, watatakiwa kutumia magari yao ili kuhakikisha tunapunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima; kuoanisha kanuni za ununuzi wa umma za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa lengo la kuimarisha ununuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kuhimiza matumizi ya samani zinazotengenezwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyotengeneza samani, *furniture and fittings* vinahamasishwa kujitokeza kwa ajili ya kazi hii, vitumie nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya

maendeleo, bajeti itazingatia kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao mwaka 2013/14 unaingia mwaka wa tatu wa utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Miundombinu: Miundombinu ya nishati; usafirishaji (barabara, reli, viwanja vya ndege, usafiri wa majini); TEHAMA; maji safi na maji taka na umwagiliaji;

(ii) Kilimo: Ikijumuisha mazao ya chakula na biashara, malighafi ya viwandani, ufugaji, uvuvi na misitu;

(iii) Viwanda: Vinavyotumia malighafi hususan za ndani na kuongeza thamani, viwanda vikubwa vya mbolea na saruji, viwanda vya kanda maalum za kiuchumi, kielektroniki na TEHAMA;

(iv) Maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi kwa kutilia mkazo sayansi, teknolojia na ubunifu;

(v) Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha; na

(vi) Huduma za jamii: Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii kwa maana ya elimu, afya na maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa ugawaji wa fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Sera ya Ugatuaji wa Madaraka na Rasilimali. Aidha, Serikali itaimarisha mifumo ya ndani ya mapato na matumizi kwa kutoa miongozo mahususi ya ukaguzi wa ndani, kuimarisha utendaji wa kamati za ukaguzi, kutoa mafunzo ya usimamizi na uimarishaji mifumo ya udhibiti wa ndani kwa Wakurugenzi

wa Halmashauri. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawezeshwa kuainisha uwezo wa pato la kila Halmashauri na fursa zilizopo katika ukusanyaji wa mapato ya ndani; na kujenga uwezo wa Halmashauri katika matumizi ya mfumo wa *IFMS*; kuhuisha baadhi ya vyanzo vya mapato ya ndani ili kuongeza mapato; kuboresha mfumo wa uthamini wa majengo kwa kutumia kanuni za jumla; kuhamasisha Halmashauri kutumia teknolojia rahisi ya mitandao ya simu za mkononi katika kufanya malipo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao, Serikali itahakikisha kwamba mafungu yanapata fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mashauriano ya Kamati ya Bunge ya Bajeti na Serikali, pamoja na mahitaji mengine ya Serikali, jumla ya shilingi bilioni 338.6 zimeongezwa katika Bajeti hii kama mchanganuo unavyoonesha kwa maana ya mapato ya ziada.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niseme naomba usikivu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Wakati wa mchakato wa kujadili Wizara mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge mlikuja na mapendekezo mazuri ya kuondoa kero zilizopo katika uchumi wetu na kero zilizopo katika jamii ya Wananchi wetu, Serikali ilitafakari uzito wa hoja na kuangalia matatizo halisi yaliyopo kwa Wananchi wetu. Katika kutizama hilo na kuwa pamoja na hoja za Wabunge kwa kupitia Kamati mbalimbali pamoja na Kamati ya Bajeti, Serikali imefanya maamuzi kama ifuatavyo:-

(i) Kuhusu ombi la Tume ya Usuluhishi na Uamuzi la kuongezewa milioni 350, ili fedha hizo zitumike kwa shughuli za usuluhishi wa migogoro ya wafanyakazi, Serikali imetafakari na kuona ni hoja yenye uzito, kwa hiyo tumeliidhinisha; *(Makofi)*

(ii) Kuhusu ombi la fedha kwa ajili ya kugharamia uchambuzi wa mapato ya ziada, Serikali imeridhia bilioni 5.6;

(iii) Kuhusu Idara ya Kurugenzi ya Mashitaka, kuomba zaidi ya shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kufanikisha kazi zao, Serikali tumeridhia shilingi bilioni kumi; *(Makofi)*

(iv) Kuhusu ombi la Mfuko wa Mahakama ili kukidhi mahitaji yao ya fedha za maendeleo ya shilingi bilioni 20, Serikali imeidhinisha;

(v) Kuhusu ombi linalohusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kuwa na fedha za kutosha kukidhi ruzuku ya mbolea, Serikali tumefanya maamuzi kuongeza bilioni 21,150. *(Makofi)*

(vi) Mheshimiwa Spika, Serikali ni sikivu, inachambua, inaangalia umuhimu, inatizama shida za Wananchi, hatukuishia hapo, tumefanya pia yafuatayo:- *(Kicheko/Makofi)*

(vii) Tumetazama kwa undani juu ya ombi la Wizara ya Viwanda na Biashara la kuhitaji kuwekeza kikamilifu kwenye *EPZ* yetu ya Kurasini *Logistics Hub* ya shilingi bilioni 30, tumeridhia. Tunathamini uwekezaji na uwekezaji ukiwekezwa vizuri katika maeneo hayo, nchi itanufaika. *(Makofi)*

(viiii) Ombi la Wizara ya Maji, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafikisha maji kwa Wananchi wetu vijijini na uchambuzi mzuri ulioletwa na Kamati yetu ya Bajeti na Kamati ya Kilimo, tumeridhia bilioni 184.5. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Serikali ina uchungu na matatizo ya maji kwa watu wake. *(Makofi)*

(ix) Kuhusu ombi la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; hawa ni wazazi wetu, ni mama zetu na tunatambua kama Kamati zilivyosisitiza, tukiimarisha

hapa tumeimarisha familia. Ombi la *two billion* tumeidhinisha. *(Makofi)*

(x) Ombi la Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kukidhi matumizi mbalimbali ya upungufu wa makusanyo yao ya shilingi bilioni 10.8 tumeidhinisha. *(Makofi)*

(xi) Limekuja lile fungia kubwa; Wizara ya Nishati na Madini, ombi lile la kuhakikisha kwamba sasa Wananchi wetu wanastahili kuwa na umeme vijijini. Hatuwezi kuwa na *Economic Inclusion* ikiwa tuna jamii inalala gizani. Tuhakikishe umeme unafika kule ili usaidie kuhamasisha shughuli za kilimo na nyingine shughuli za uzalishaji. Kwa hiyo, ombi la umeme kufikisha vijijini, Serikali tumeidhinisha bilioni 186.9 za nyongeza**.** Hii ni nyongeza. *(Makofi)*

(xii) Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, tayari Serikali tulikuwa tumewatengea *REA* jumla ya bilioni 153; tumetafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge tukaona zina uzito mkubwa tukaongeza fedha hiyo. *(Makofi)*

(xiii) Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni. Roho ya Taifa ni vijana. Kulikuwa na ombi, Mfuko wa Vijana uongezewe bilioni tatu tumeidhinisha. Pili, Wizara hiyo hiyo ndiyo inayosimamia matangazo hayo, unaona! Waheshimiwa wako juu huko *TBC,* hili Shirika letu liimarike lifanye kazi zake vizuri, tumeidhinisha bilioni sita. *TBC* iongeze usikivu ili Wananchi wasikie Serikali na Bunge lao linafanya nini. *(Makofi)*

(xiv) Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, tumetambua umuhimu wa mifugo, tumeidhinisha bilioni 20 za nyongeza. Hizo ni fedha za nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu niende haraka haraka.

**SPIKA:** Wizara ya Uchukuzi? Wizara ya Uchukuzi - *Vote 62.*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Uchukuzi iliomba bilioni 30 tumeidhinisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu niseme palipo na matumizi pana dharau. Ifuatayo ni maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyinginezo za mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuongeza mapato na kupanua wigo wa kodi hususan kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, itaendelea pia kupunguza misamaha ya kodi katika muda wa kati kutoka asilimia 4.3 ya Pato la Taifa katika mwaka 2011 hadi walau asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, Serikali itaongeza juhudi za kukusanya mapato ya ndani, kuharakisha majadiliano na Washirika wa Maendeleo na wakopeshaji mbalimbali katika kutafuta mikopo na misaada kwa wakati. Ninatoa wito kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba wanatimiza masharti na taratibu za kupata fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mfumo Mpya wa Uandaaji na Utekelezaji wa Vipaumbele vya Miradi ya Maendeleo kama ilivyoelezwa hapo awali kwenye Hotuba ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa. Stephen Masatu Wassira (Mb), Serikali imeainisha maeneo ya kimkakati ambayo yatafungua fursa ya mapinduzi ya kiuchumi na kuleta matokeo makubwa kiuchumi na kijamii kwa muda mfupi. Maeneo hayo ni utafutaji wa mapato, kilimo, maji, elimu, nishati na miundombinu ya uchukuzi. Serikali imedhamiria kutekeleza miradi kwenye maeneo hayo katika kipindi cha muda wa kati. Utekelezaji madhubuti wa vipaumbele hivi utafanikisha kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa spika, ili kuongeza ufanisi katika

utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Serikali imeweka mikakati ya kuongeza nidhamu ya kupanga na kutekeleza Miradi ya Maendeleo ili kupata matokeo yanayowiana na thamani halisi ya fedha. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeainisha maeneo makuu sita kama nilivyoeleza hapo awali, ambayo yatazingatiwa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Aidha, kama mnavyofahamu, Serikali imeunda chombo *(Presidential Delivery Bureau),* kitakachoratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi katika sekta zilizobainishwa.

Mheshimiwa spika, katika mwaka 2013/14, Serikali imeweka kipaumbele katika kutatua kero ya maji kwa Wananchi, ambapo shilingi bilioni 747.6 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji mijini na vijijini. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya uchukuzi ambayo inajumuisha barabara, reli, madaraja, bandari na viwanja vya ndege, Serikali imetenga shilingi bilioni 2,169.0 katika mwaka 2013/14, ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,940.0 mwaka 2012/13. Kati ya fedha hizo zilizotengwa mwaka 2013/14, shilingi bilioni 196.8 ni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya reli ikilinganishwa na shilingi bilioni 134.2 zilizotengwa mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 46.6. Aidha, Serikali imedhamiria kuongeza bajeti na kuchukua hatua za kuishirikisha sekta binafsi katika kuimarisha miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sekta ya Nishati na madini, juhudi zitaelekezwa katika kuongeza uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ambapo jumla ya shilingi bilioni 1,426.9 zimetengwa kwa ajili hiyo ikilinganishwa na shilingi bilioni 731.8 mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Serikali itachukua hatua zifuatazo katika kuboresha Sekta ya Fedha:-

(i) Kutunga Sheria ya Mfumo wa Malipo nchini kwa ajili ya kuwa na utaratibu wa usimamizi wa mifumo ya malipo nchini ili kuboresha matumizi ya kielektroniki katika kufanya malipo, hususan kwa kutumia simu za mikononi, huduma za benki kwa njia ya mtandao, vituo vya mauzo na mashine za kutolea fedha *(ATM);*

(ii) Kuandaa Sera ya Bima ya Taifa; na

(iii) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Taasisi ndogo za Fedha, 2002.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Serikali itaendelea na hatua za kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa kanuni na miongozo ambayo itajikita katika kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii na kuifanya kuwa endelevu na yenye mchango katika maendeleo ya wanachama wa mifuko na nchi kwa ujumla;

(ii) Kusajili Mifuko, Mameneja Uwekezaji *(Fund Managers)* na Watunza Mali *(Custodians)* kwa ajili ya kutenganisha majukumu kwenye uendeshaji wa Mifuko ili kuleta ufanisi zaidi; na

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto nilizozieleza awali, Serikali imeandaa mikakati ya kukabiliana nazo katika mwaka 2013/14 kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la tija katika kilimo, Serikali itaboresha mfumo wa kilimo, mifugo na uvuvi uwe wa kibiashara badala ya ule wa kujikimu; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji; kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo; kuimarisha huduma za ugani; upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, kusimamia upatikanaji wa masoko; na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha za umma, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa kada za uhasibu, ununuzi, uhakiki mali na ukaguzi wa ndani. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi wa mali za Serikali na kufanya uhakiki wa mali za Serikali katika Wizara, Mikoa na Halmashauri ili kuboresha daftari la mali za Serikali na kubaini mali zisizokuwa na tija kwa ajili ya kuzifuta.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kudhibiti matumizi, Serikali itapunguza matumizi kwenye maeneo ambayo hayataathiri utoaji wa huduma za msingi. Aidha, Serikali itapitia kanuni za ununuzi ili kuhakikisha kuwa huduma na vifaa vinavyonunuliwa vinaendana na thamani ya fedha. Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma, kumekuwepo na kanuni za ununuzi tofauti kati ya zinazotumika katika Serikali Kuu na zile zinazotumika katika Serikali za Mitaa. Uzoefu uliopo unaonesha kuwa, kanuni hizo zimekuwa na changamoto nyingi za kiutekelezaji. Ili kutatua tatizo hilo, Serikali imepanga kuoanisha kanuni za ununuzi wa umma zinazotumika katika Serikali Kuu na zile zinazotumika katika Serikali za Mitaa. Hatua hii itaboresha usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma. Ili kuhakikisha ununuzi wa umma unatekelezwa kulingana na Sera na Sheria husika, Wizara ya Fedha itasimamia shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa Deni la Taifa, Serikali inakamilisha taratibu za kuanzisha Idara ya Usimamizi wa Deni la Taifa ndani ya Wizara ya Fedha ambayo itaanza kazi mwaka 2013/14. Aidha, Serikali inapitia upya Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa wa mwaka 2002 pamoja na kuifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 iliyorekebishwa mwaka 2004, ili kutambua uanzishwaji wa Idara ya Kusimamia Deni la Taifa kwa mujibu wa Sheria na kuiboresha ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, Bajeti ya Serikali inatekelezwa kama ilivyokusudiwa, Serikali itawajengea uwezo watumiaji wa Mfumo wa Malipo *(IFMS)* kuhusu maeneo yaliyoboreshwa katika toleo la *Epicor* 9.02; kuhakikisha mihadi na malipo yote yanafanyika kwa kutumia mfumo wa *IFMS;* na kufanya ukaguzi wa ununuzi kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali itaweka utaratibu wa kuibua miradi, kuifanyia upembuzi yakinifu na kuichambua kabla haijatengewa fedha katika bajeti ya mwaka husika ili kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa wakati na Serikali inapata thamani halisi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia fursa za kijiografia katika ukuzaji wa uchumi, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji hususan barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege; kuongeza upatikanaji wa nishati ya umeme; kuboresha huduma za utalii; kupunguza gharama za kufanya biashara nchini ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje; na kuimarisha ulinzi na usalama katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Serikali itaendelea kudhibiti mfumko wa bei kwa kuhamasisha uzalishaji na usambazaji sawia wa mahitaji muhimu kama vile chakula, mafuta ya nishati, sukari, vifaa vya ujenzi na huduma za usafiri. Aidha, Serikali itatumia hifadhi ya taifa ya chakula kusambaza chakula katika masoko kwa ajili ya kudhibiti bei.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, Serikali itaimarisha kamati za kisekta za kuratibu mifumo ya kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; kuhimiza Wananchi kutumia nishati mbadala; kuhamasisha Wananchi kupanda mazao yanayostahimili ukame; kutumia chakula kilichopo kwa tija na uangalifu ili kukidhi mahitaji ya msingi; kuchukua tahadhari ya upatikanaji wa umeme

wa uhakika; na kuelimisha Wananchi wachukue tahadhari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuepuka uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Serikali itaendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuongeza mapato na kupanua wigo wa kodi hususan kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, itaendelea pia kupunguza misamaha ya kodi katika muda wa kati kutoka asilimia 4.3 ya Pato la Taifa katika mwaka 2011 hadi kufikia walau asilimia moja. Hivi karibuni uchambuzi wa misamaha ya kodi umeonesha kwamba, misamaha mingi ya kodi imetokana na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye maeneo ya kimkakati kupitia Kituo cha Uwekezaji. Aidha, Serikali ilisamehe kodi na ushuru kwenye mafuta ya kuendeshea mitambo ya umeme wa dharura na pia kusamehe kodi na ushuru kwenye uagizaji wa sukari na mchele ili kuziba pengo la upungufu wa bidhaa hizo hapa nchini. Vilevile misamaha pia imekuwa ikitolewa kwa wawekezaji katika Maeneo Maalum ambao wanazalisha bidhaa zinazouzwa nje *(EPZ* na *SEZ),* ujenzi wa miundombinu na baadhi ya miradi inayofadhiliwa na wahisani ili kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo yenye gharama kubwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kupunguza misamaha zitaelekezwa zaidi katika kupunguza misamaha isiyo na tija na yenye uwezekano wa kutumika vibaya. Kwa sasa Serikali inakamilisha mapitio ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kupunguza misamaha. Aidha, Serikali inakamilisha kazi ya utafiti wa kuchambua misamaha yote ya kodi ili kuleta mapendekezo ya kupunguza misamaha isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuendelea kufanya vibaya katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, Serikali iko katika hatua nzuri ya kukamilisha utafiti wa kuangalia vyanzo vya mapato na kuwianisha mifumo inayotumika katika ukusanyaji wa mapato hayo. Mapendekezo ya utafiti huo yatazingatiwa kwenye kipindi cha mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya kiuchumi na mapato, katika mwaka 2013/14, ninapendekeza kufanya maboresho ya sheria mbalimbali za kodi kama ifuatavyo: Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148; Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147; Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220; Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82; Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168; Sheria ya Petroli *(Petroleum Act)* SURA 392; Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38; Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; Marekebisho mengine madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyinginezo mbalimbali; na vilevile Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148:-

(i) Kufuta msamaha wa *VAT* unaotolewa kwenye huduma za utalii chini ya Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kipengele cha 14. Aidha, hatua hii itahusisha huduma zifuatazo: *(i) Tourist Guiding (ii) Game Driving (iii) Water Safaris (iv) Animal or Bird Watching (V) Park Fees (vi) Tourist Charter Services (vii) Ground Transport.* Hatua hii inalenga kutekeleza azma ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi. Hata hivyo, msamaha wa ushuru wa forodha utaendelea kutolewa kwenye vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kutoa huduma za utalii;

(ii) Mheshimiwa Spika, kutoa msamaha wa *VAT* kwa wazalishaji wa nguo nchini zinazozalishwa kwa pamba ya ndani kwa bidhaa na huduma zitakazotumika tu kwenye uzalishaji wa nguo hizo kupitia Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza *VAT* kwa wazalishaji kwa kiwango cha asilimia sifuri chini ya Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, yaani *VAT.* Kwa hatua hii, mzalishaji wa nguo zinazotumia pamba ya hapa nchini hatalipa *VAT*

kwenye manunuzi yake ya malighafi yanayohusiana za uzalishaji wa nguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 48,977.6.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza viwango vya chini vya kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 14 hadi asilimia 13. Hatua hii inalenga katika kutoa nafuu ya kodi kwa mfanyakazi. *(Makofi)*

Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama vilivyo kwenye Jedwali linalofuata. Jedwali linaonesha jumla ya mapato na kiwango cha kodi ya sasa. Halafu kuna Jedwali linalofuata linaloonesha vilevile viwango vinavyopendekezwa, jumla ya mapato na kiwango cha kodi kipya.

**Viwango vya sasa**

| **Jumla ya Mapato** | **Kiwango cha Kodi** |
|---|---|
| Mapato ya jumla yasiyozidi Shilingi 2,040,000/= | Asilimia sifuri (0%) |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 2,040,000 lakini hayazidi shilingi 4,320,000/= | 14% ya kiasi kinachozidi Shilingi 2,040,000/= |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 4,320,000/= lakini hayazidi shilingi 6,480,000/= | Shilingi 319,200/= + 20% ya kiasi kinachozidi Shilingi 4,320,000/= |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 6,480,000/= lakini hayazidi shilingi 8,640,000/= | Shilingi 751,200/= + 25% ya kiasi kinachozidi Shilingi 6,480,000/= |

| | |
|---|---|
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 8,640,000/= | Shilingi 1,291,200/= + 30% ya kiasi kinachozidi Shilingi 8,640,000/= |

**Viwango vinavyopendekezwa**

| **Jumla ya Mapato** | **Kiwango cha Kodi** |
|---|---|
| Mapato ya jumla yasiyozidi Shilingi 2,040,000/= | Asilimia sifuri (0%) |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 2,040,000 lakini hayazidi shilingi 4,320,000/= | 13% ya kiasi kinachozidi Shilingi 2,040,000/= |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 4,320,000/= lakini hayazidi shilingi 6,480,000/= | Shilingi 296,400/= + 20% ya kiasi kinachozidi Shilingi 4,320,000/= |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 6,480,000/= lakini hayazidi shilingi 8,640,000/= | Shilingi 728,400/= + 25% ya kiasi kinachozidi Shilingi 6,480,000/= |
| Mapato ya jumla yanayozidi Shilingi 8,640,000/= | Shilingi 1,268,400/= + 30% ya kiasi kinachozidi Shilingi 8,640,000/= |

(i) Kuanzisha kodi ya zuio ya asilimia kumi ya kamisheni *(commission)* ya usafirishaji wa fedha kwa njia ya simu za mkononi. Kodi hiyo itakusanywa na kampuni za simu kutoka kwa wakala wanaotoa huduma za kusafirisha fedha kupitia simu za mkononi;

(ii) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia tano kwenye malipo yatokanayo na huduma mbalimbali

kama vile huduma za ushauri wa kitaalamu na nyinginezo *(Consultancy services and other services),* kwa wanaotoa huduma hizi wa ndani na wanaotkka nchi za nje. Imegundulika kuwa mara nyingi wanaotoa huduma huwa hawalipi walio wengi. Kwa hiyo, ili Serikali kuhakikisha kwamba, inawapa nafasi watu wote kulipa kodi kwa mujibu wa sheria, tunaleta kodi hii. Kodi hii itatozwa bila kujali kama kuna Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi *(TIN)* au la. Lengo la hatua hii ni kudhibiti na kulinda mapato ya Serikali;

(iii) Kutoza kodi ya zuio kwenye bidhaa zinazonunuliwa na Serikali na Taasisi zake kwa kiwango cha asilimia mbili bila kujali kama kuna Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (*TIN*) au la. Lengo la hatua hii ni kudhibiti na kulinda mapato ya Serikali;

Hapa tunalenga wale *suppliers* wanao-*supply* Serikalini kwa hiyo, nao tunawakata *withholding tax* kuhakikisha kwamba kodi yao wanayostahili walau tuna-*withhold two percent*;

(iv) Kufuta msamaha wa kodi ya zuio kwenye ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakazi (*non-resident).* Hatua hii inalenga katika kupunguza misamaha ya kodi na kuhuisha mapato ya Serikali; na

Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa pamoja zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 131,686.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji *(Non-Utility Motor Vehicles)* ya umri wa zaidi ya miaka kumi kutoka asilimia 20 hadi asilimia 25. Hatua hii inalenga katika kupunguza

uagizaji wa magari chakavu, kulinda mazingira na kupunguza ajali; *(Makofi)*

(ii) Kuanzisha kiwango kipya cha Ushuru wa Bidhaa cha asilimia tano kwenye magari ya uzalishaji *(Utility Motor Vehicles)* yenye umri wa zaidi ya miaka kumi yanayotambuliwa katika *HS Code 87.01, 87.02* na *87.04.* Hatua hii haitahusisha magari chini ya *HS Code* 8701.10.00; na *HS Code* 8701.90.00 ambayo kimsingi ni matrekta yaliyounganishwa; na magari yasiyounganishwa chini ya *HS Code* 8702.10.11; 8702.10.21, 8702.10.91; 9702.90.11, 8702.90.21; 8702.90.91; *HS Code* 87.04; 8704.10.10; 8704.21.10; 8704.22.10; 8704.23.10; 8704.31.10, na 8704.32.10, 8704.90.10. Lengo la kuanzisha kiwango kipya cha ushuru ni kupunguza uagizaji wa magari chakavu, kulinda mazingira na kupunguza ajali. Aidha, matrekta na magari yasiyounganishwa hayatatozwa ushuru huu kwa nia ya kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya uunganishaji wa magari na hivyo kuongeza ajira na mapato ya serikali;

(iii) Kurekebisha viwango vya Ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya Petroli kama ifuatavyo:-

(a) mafuta ya Dizeli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 215 kwa lita hadi shilingi 217 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi mbili tu; kwa sababu Serikali inatambua kwamba magari makubwa, mabasi yanayohudumia Wananchi na yanayoshughulika na ubebaji mkubwa wa mizigo wa nchi hii, yanatumia dizeli. Kwa hiyo, tunaelewa kwamba, tukipandisha sana kodi kwenye dizeli basi *effect* itakuwa kubwa kwenye uzalishaji. Kwa hiyo, hilo tumezuia kwa kuongeza *only* shilingi mbili.

Mheshimiwa Spika, sentensi hiyo naisoma; mafuta ya dizeli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 215 kwa lita hadi shilingi 217 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi mbili tu kwa sababu hizo nilizozisema. *(Makofi)*

(b) mafuta ya Petroli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 339 kwa lita hadi shilingi 400 kwa lita; na

(c) bei ya mafuta ya taa haitabadilika inabaki ile ile shilingi 400.30;

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtaletewa haya mabadiliko.

**SPIKA:** *Hansard* inasema anayosema siyo haya aliyoandika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mafuta ya taa narudia, yanabaki bei ile ile, kwa maana ya kodi inabaki kodi ile ile shilingi 400.30. *(Makofi)*

(iv) Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia kati ya 10 hadi asilimia 25 kwenye bidhaa mbalimbali zinazozalishwa au kuingizwa nchini kama vile; mazulia, vipodozi, mafuta ya kujipaka, bidhaa na mifuko ya ngozi, bunduki na risasi, boti za kifahari, ndege na helikopta;

(v) Kuanzisha kiwango cha Ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, zinazotambulika katika *HS Code* 94.03. Hatua hii inalenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa samani kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, hatua hii itachochea ukuaji wa ajira na kuongeza mapato ya Serikali;

(vi) Kutoza Ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5 kwenye huduma zote *(all mobile phone services)* za simu za kiganjani/mkononi badala ya muda wa maongezi tu *(airtime alone).* Katika ushuru huu asilimia 2.5 zitatumika kugharamia matatizo ya elimu hapa nchini. *(Makofi)*

(vii) Kuongeza wigo wa kutoza Ushuru wa bidhaa kwenye huduma za simu za mezani (*zinazojulikana kama simu za TTCL*) zisizokuwa na waya;

Namba nane hiyo msiisome.

**SPIKA:** Wanagawa *addendum* sasa hivi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee.

(viii) Kurekebisha viwango *maalum (specific rates)* vya Ushuru wa bidhaa zisizokuwa za mafuta kama vile vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali, sigara na kadhalika kwa asilimia kumi kama ifuatavyo:-

(a) Vinywaji baridi, kutoka shilingi 83 kwa lita hadi shilingi 91 kwa lita; hilo ni ongezeko la shilingi nane tu kwa lita;

(b) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (Juisi) iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini kutoka shilingi nane kwa lita hadi shilingi tisa kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi moja tu kwa lita;

(c) Ushuru wa bidhaa kwenye Juisi iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini kutoka shilingi 100 kwa lita hadi shilingi 110 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 10 kwa lita;

(d) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 310 kwa lita hadi shilingi 341 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 31 kwa lita;

(e) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 525 kwa lita hadi shilingi 578 kwa lita; yaani ongezeko la shillingi 51 kwa lita;

(f) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75, kutoka shilingi 145 kwa lita hadi shilingi 160 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 15 kwa lita moja;

(g) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,614 kwa lita hadi shilingi 1,775 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 161 kwa lita;

(h) Vinywaji vikali, kutoka shilingi 2,392 kwa lita hadi shilingi 2,631 kwa lita; sawa na ongezeko la shilingi 239 kwa lita moja;

(i) Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezwa; narudia, Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezwa;

(ix) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 8,210 hadi shilingi 9,031 kwa sigara elfu moja; sawa na ongezeko la senti 82 tu kwa sigara moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 19,410 hadi shilingi 21,351 kwa sigara elfu moja; ikiwa ni ongezeko la shilingi 1 na senti 94 kwa sigara moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 35,117 hadi shilingi 38,628 kwa sigara elfu moja; ikiwa ni ongezeko la shilingi 3 na senti 50 tu kwa sigara moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *("cut filler')* kutoka shilingi 17,736 hadi shilingi 19,510 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa Bidhaa kwa *"Cigar"* unabaki kuwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Ushuru wa Bidhaa kwa pamoja, zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 510,017.50.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwezo wa Serikali katika kugharamia ukarabati wa miundombinu ya barabara ambayo ni muhimu katika kuleta maendeleo na kujenga uchumi hapa nchini, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, SURA 220 kama ifuatavyo: Kuongeza kiwango cha Ushuru wa mafuta *(fuel levy)* kutoka shilingi 200 kwa lita hadi shilingi 263 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 63 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 155,893.50.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82 kama ifuatavyo:-

Kupunguza tozo ya kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi *(Skills Development Levy "SDL")* kutoka kwenye kiwango cha sasa cha asilimia sita hadi kiwango cha asilimia tano. Aidha, sambamba na kupunguza kiwango cha sasa cha *SDL,* Taasisi za Serikali zisizotegemea bajeti ya Serikali kwa kiwango kikubwa katika kujiendesha pia zitalipa tozo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 28,213.90.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168 ili kuongeza viwango vya ada ya mwaka ya leseni za magari *(Annual Motor Vehicle Licence Fee)* kama ifuatavyo:-

(i) Gari lenye ujazo wa Injini *501.cc – 1500.cc* kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000;

(ii) Gari lenye ujazo wa Injini *1501.cc – 2500.cc* kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 150,000 hadi shilingi 200,000;

(iii) Gari lenye ujazo wa Injini zaidi ya *2501.cc* kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 200,000 hadi shilingi 250,000; na

(iv) Magari yenye ujazo wa Injini chini ya *501.cc* hayatatozwa ada ya leseni za magari. Hakuna kutoza bodaboda, yaani bajaji hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nasema hivi; magari yenye ujazo wa Injini chini ya *501.cc* hayatatozwa ada ya leseni za magari. Hii ni pamoja na bodaboda na bajaji. Vijana wetu watulie wafanye kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii itatekelezwa kupitia tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 19,710.90.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Petroli *(Petroleum Act)*, SURA 392: Ili kutekeleza dhamira ya Serikali ya kusambaza umeme vijijini, napendekeza kuanzisha Tozo ya mafuta ya petroli *(petroleum levy)* ya shilingi 50 kwa lita ambayo itakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).* Mapato yatakayokusanywa kutoka kwenye tozo hiyo yatatumika kugharamia mahitaji ya Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* katika kusambaza umeme vijijini. Tupeleke umeme vijijini. Hatua hii itatekelezwa kupitia tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 123,725.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38: Napendekeza kutoza asilimia 25 ya ushuru wa forodha unaopaswa kutozwa kwenye bidhaa

zinazotambulika kama "*Deemed Capital Goods*" (yaani kutoa msamaha wa kodi wa asilimia 75 kwenye bidhaa hizo badala ya asilimia 90 za sasa) na kuziondoa baadhi ya bidhaa kwenye orodha ya kupata msamaha. Bidhaa hizo ni zile ambazo hazina uasilia wa kuwa bidhaa za mtaji *(capital goods)* kama vile vifaa vya ofisi, samani, sukari, vinywaji (viburudisho), bidhaa za mafuta ya petroli, magari madogo *(Non Utility Motor Vehicles)*, viyoyozi, majokofu na vifaa vya kielektroniki, mashuka, vijiko, vikombe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004: Mawaziri wa Fedha kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tulikutana tukafanya Kikao cha Mashauriano kuhusu masuala ya Bajeti *(Pre-Budget Consultations of EAC Ministers for Finance)* tarehe 7 Juni, 2013 Mjini Arusha. Kikao hicho kilipendekeza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha *(EAC-Common External Tariff "CET")* na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC-Customs Management Act, 2004*) kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopendekezwa kufanyiwa marekebisho kwenye viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha ni:-

(i) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambuliwa katika *HS Code* 1001.99.20 na *HS Code* 1001.99.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda na wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano hiyo; na

(ii) Kutoza ushuru wa asilimia 25 kwenye bidhaa za mchele na sukari wakati bidhaa hizo zinapoingizwa nchini kwa msamaha maalumu wa Serikali baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa hizo kwa sasa zinatozwa Ushuru wa pamoja wa

Jumuiya ya Afrika Mashariki wa asilimia 100 kwa sukari na asilimia 75 kwa mchele.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC-Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa mashine na vipuli vya reli vinavyoagizwa na Shirika la Reli Tanzania. Hili tuliomba sisi. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu kwenye gharama za kuboresha reli na kuimarisha usafirishaji wa reli;

(ii) Kufuta utaratibu wa kutokukagua mizigo inayoingizwa na wafanyabishara ujulikanao kama "*Compliant Trader Scheme*" ambao uzoefu umeonesha kwamba unatumiwa vibaya na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa kulipa kodi sahihi na hivyo kuipotezea Serikali mapato yake halali;

Tunatengeneza *Administrative Framework* ya ku-*manage* hili.

(iii) Kuimarisha mfumo wa uthamini *(valuation)* wa bidhaa kutoka nje ya nchi ili kuondoa tatizo la upotevu wa mapato kutokana na uthamini usio sahihi. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa *Import Export Commodity Database (IECDB);*

(iv) Kuendelea kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha *(duty remission)* kwa malighafi ya kutengeneza sabuni inayojulikana kama *LABSA* inayotambuliwa katika *HS Code* 3402.11.00; *HS Code* 3402.12.00 na *HS Code* 3402.19.00 kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja. Hatua

hii inalenga katika kuimarisha uzalishaji na kukuza viwanda vidogo na vya kati vya sabuni hapa nchini;

(v) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye mifuko ya plastiki inayotumika katika uzalishaji wa nishati ya gesi *(plastic bag biogas digesters*). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala na kutunza mazingira;

(vi) Kuongeza ushuru wa forodha kwenye mawe yanayotumika katika mashine za kusaga bidhaa mbalimbali kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 25. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye mitambo ya kusafisha uchafu katika maji *(Water treatment effluent plant)* unaotoka viwandani kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha viwanda vya ndani kutumia mitambo hii ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na kupunguza gharama za uzalishaji viwandani;

(viii) Kuendelea kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye migahawa ya Majeshi ya Ulinzi kwa kipindi cha mwaka mmoja mwingine;

(ix) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha kwa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 135,526.90.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za Kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake.

(i) Kwa kutambua kwamba Sekta binafsi ndiyo

yenye msukumo mkubwa katika maendeleo ya uchumi Duniani kote, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya *Public Procurement Act, 2011* na *Public Private Partnership Act 2010* ili kuwezesha *unsolicited PPP Proposals* kutohusika na utaratibu wa ushindani ikiwa ni njia mojawapo ya kuvutia wawekezaji katika Miradi ya Maendeleo kwa manufaa ya kiuchumi ya nchi yetu;

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili limekuja kwa sababu hivi karibuni na kwa muda mrefu, tumeshuhudia wawezaji mahiri mbalimbali wenye fedha zao wanakuja kutambua fursa za kuwekeza Tanzania, lakini kwa kuwa wao wametambua wenyewe, *the unsolicited*; kwa hiyo, sheria ilikuwa haiwaruhusu. Tunataka turekebishe pale mwekezaji anapokuja na hela yake anakidhi kuwekeza kwenye maeneo ambayo yataleta *economic impact* kwa nchi yetu aweze kuwekeza.

(ii) Kurekebisha Sheria ya Fedha Za Umma, SURA 348, Sheria ya Msajili wa Hazina SURA 418 na Sheria ya Wakala za Serikali, SURA 245, ili kuweka sharti kwa wakala na taasisi za serikali kuwasilisha kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi (badala ya mapato ya ziada) ya taasisi na wakala hizo kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2013, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha hilo, sasa naomba niseme sura ya Bajeti ya mwaka 2013/14.

Kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na shabaha ya bajeti, sura ya bajeti itakuwa kama ifuatavyo: Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni

18,249 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 11,154.1, sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 383.5, sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuendelea kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,855.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,163.1 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 2,692.1 ni mikopo na misaada kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta shilingi bilioni 500.4.

Mheshimiwa Spika, ili kuziba nakisi ya bajeti, Serikali inatarajia kukopa kutoka katika vyanzo vya ndani na nje shilingi bilioni 2,856.3. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,147.6 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na mkopo wa ndani shilingi bilioni 552.3 ambao ni asilimia moja ya Pato la Taifa na shilingi bilioni 1,156.4 ambazo ni mikopo yenye masharti ya kibiashara zitatumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Tunakopa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, jumla ya shilingi bilioni 18,249 zimekadiriwa kutumika katika mwaka 2013/14, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya hizo; matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 12,574.9 ambayo yanajumuisha shilingi bilioni 4,763 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Serikali, Taasisi na Wakala za Serikali; Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 3,319.2, na Matumizi Mengineyo shilingi bilioni 4,492.6.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/14, jumla ya shilingi bilioni 5,674 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2,982 kitagharamiwa kwa fedha za ndani. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 552.3 zinatokana na mkopo kutoka vyanzo vya ndani, shilingi bilioni 1,156.4 ni mikopo ya masharti ya

kibiashara, shilingi bilioni 386.2 ni mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 887.1 zitatokana na asilimia nane ya mapato ya kawaida. Kiasi cha shilingi bilioni 2,692.6 kitagharamiwa kwa fedha za nje, misaada na mikopo ya Miradi ya Maendeleo ikijumuisha Mifuko ya Pamoja ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama ulivyoelezwa hapo juu, mfumo wa bajeti kwa mwaka 2013/14 unakuwa kama ifuatavyo:-

| Mapato | Shilingi Milioni | |
|---|---|---|
| A. Mapato ya Ndani | | 11,154,071 |
| (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 10,412,937 | |
| (ii) Mapato yasiyo ya Kodi | 741,134 | |
| B. Mapato ya Halmashauri | | 383,452 |
| C. Mikopo na Misaada ya Kibajeti | | 1,163,131 |
| D. Mikopo na Misaada ya Miradi ya Maendeleo ikijumuisha MCA (T) | | 2,692,069 |
| E. Mikopo ya Ndani | | 1,699,860 |
| F. Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara | | 1,156,400 |
| **JUMLA YA MAPATO YOTE** | | **18,248,983** |
| Matumizi | | |
| G. | | 12,574,949 |
| (i) Deni la Taifa | 3,319,156 | |
| (ii) Mishahara | 4,763,196 | |
| (iii) Matumizi mengineyo | 4,492,566 | |

| | | |
|---|---|---|
| Wizara | 3,738,316 | |
| Mikoa | 49,701 | |
| Halmashauri | 4,549 | |
| **H. Matumizi ya Maendeleo** | | **5,674,034** |
| (i) Fedha za Ndani | 2,981,965 | |
| (ii) Fedha za Nje | 2,692,069 | |
| **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | | **18,248,983** |

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, bajeti ya mwaka 2013/14 imelenga kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; na kuanza kutekeleza maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika *Labs.* Madhumuni ya mipango na mikakati hii ni kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo ningependa kulisisitiza ni sote kwa pamoja kuongeza ushirikiano katika kusimamia majukumu na matumizi ya fedha na rasilimali zetu vizuri ili kuongeza ufanisi. Masuala yote tuliyoyajadili katika Bunge hili ni ya msingi sana; hivyo, kama tutayafanyia kazi kwa ufanisi, tutafikia matarajio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo yanalenga kuitoa Tanzania katika kundi la nchi maskini na kuingia katika kundi la nchi zenye viwango vya kati vya mapato na hali bora ya maisha.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imelenga pia kuongeza makusanyo ya mapato, hasa ya ndani kwa kuanzisha vyanzo vipya na kuboresha vilivyopo. Lengo likiwa ni kujitosheleza kwa mapato yatakayowezesha kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma kwa Wananchi. Katika kikao hiki cha Bunge la Bajeti, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza kuongeza

fedha kwa baadhi ya mafungu ili kuyawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, imezingatia kiasi kikubwa cha mapendekezo hayo. Ili kutekeleza mapendekezo hayo, imelazimu kufanya maboresho zaidi katika kodi na tozo mbalimbali kwani isingewezekana kugharamia mapendekezo hayo kiurahisi bila kuathiri upande wa kodi. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mnielewe katika hili na kuniunga mkono ili mafungu yaweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake inaendelea kuboresha miundombinu ya kiuchumi, kifedha na kijamii ili kuongeza fursa za ushiriki wa Wananchi katika uzalishaji na kuboresha hali zao za maisha. Bajeti inalenga pia kuongeza upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika, kuendeleza ardhi na kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miuondombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege na mawasiliano. Hii itasaidia pia kutumia vyema fursa za kijiografia zinazotokana na kupakana na nchi zisizokuwa na bahari. Aidha, bajeti hii inalenga kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu kupitia mfumo mpya wa utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ambapo italeta matokeo makubwa kwa haraka. Tumezingatia vipaumbele vyote pamoja na maji.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14 imezingatia mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na Kamati za Kisekta za Bunge kadiri hali ya fedha ilivyoruhusu. Ushauri uliotolewa na Kamati hizo na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, zilifanyiwa kazi kadiri ilivyowezekana. Aidha, kwa utaratibu huu mpya wa mzunguko wa bajeti ambao ulipitisha bajeti za mafungu mbalimbali, maelelezo yangu haya ni kuhitimisha mjadala wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, yote niliyoyasema yanawezekana iwapo kila mmoja wetu na Wananchi kwa ujumla tutatimiza wajibu wetu, kila mmoja kwa nafasi yake,

kwa kushiriki na kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza sera na mipango tuliyojiwekea tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa mara nyingine tena kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Asanteni sana. Hoja imeungwa mkono, kama kawaida yetu waombaji wa kuchangia hoja hii mlishajaza fomu wakati ule, kwa hiyo, majina yenu yatatoka Siku ya Jumatatu. Tutachangia mpaka tarehe 24. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia Bajeti ya Taifa na walisha-*submit* maombi yao, wajiandae vizuri, tupate michango yenye elimu kwa Wananchi na yenye manufaa ambayo Wananchi wanakaa kwa furaha kuwasikilizeni mnavyochangia mambo yenu kwa uzuri.

Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Wasaidizi wake, Naibu Mawaziri na Wataalam wote wa Wizara hiyo, naamini na Serikali nzima tulishiriki kutengeneza, maana hii ni Bajeti ya Taifa. Kwa hiyo, nawapongezeni sana na tunawapongeza zaidi kwa kuwa wasikivu kwa upande wa madai ambayo Wabunge walikuwa nayo katika ngazi ya Kamati na hatimaye kwenye Kamati ya Bajeti. Serikali na sisi wote, tutaboresha utaratibu wa bajeti uwe shirikishi zaidi na uwe unawajibika zaidi kwa Wananchi na kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

Pia utaratibu wetu uweze kusimamia Serikali kama Mheshimiwa Waziri ulivyosema hapa. Sisi tungependa kusimamia yale uliyoahidi hapa yasimamiwe vilevile na kama kuna jambo tofauti, basi liletwe ndani ya Bunge na siyo vinginevyo; nadhani tutakwenda mbele.

Baada ya kusema hivyo, naomba niwatambue wageni tulionao, nitawatambua kwa makundi kwa sababu mko wengi na wote mliopo hapa tumewapa kadi na wengine wasiokuwepo pia tunawakaribisha.

Kwanza, tuna wageni wa Familia ya Mheshimiwa William Mgimwa, Waziri wa Fedha, ambao wanaongozwa na mke wake Mrs. Jane Mgimwa; asimame alipo. Wanakushangilia kwa sababu mume wako alipokuwa anakosekana nyumbani alikuwa anajaribu kutengeneza Bajeti ya Serikali; tunakushukuru kwa uvumilivu. *(Makofi)*

Tutambue pia uwepo wa Mrs. Pinda, Mke wa Waziri Mkuu; alipo naomba asimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine naomba niwatambue kwa ujumla jumla. Kwanza, tunaye Katibu Mkuu Kiongozi, nadhani yupo, ahsante sana. Nilishamtambua Mama Pinda. Kuna Kamishna Mkuu wa *TRA;* naomba asimame alipo. Kuna Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; naomba asimame. Tuna Mkuu wa JKT; naomba asimame. Pia wale waliokwenda JKT kutokana na Wabunge, mnatakiwa kwenda kufanya mafunzo ya paredi kwa Siku ya Mashujaa tarehe 25, lakini mafunzo tarehe 3, mtaandikiwa nadhani mmepewa taarifa. Nitawaleta hao wakafanye mazoezi ya paredi maana ni askari wanaotarajiwa kuwepo. *(Makofi)*

Tunaye Kamishna Mwandamizi wa Magereza; naomba asimame, ahsante. Tuna Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa; naomba asimame. Tuna Mratibu Msaidizi Mkuu wa Baraza la Usalama la Taifa; naomba asimame. Sikuwataja majina. Kuna Mkurugenzi Mkuu wa Vitambulisho vya Taifa. Tuna Makamanda wa Vikosi vya Majeshi Dodoma; naomba wote wasimame walipo, naona wenyeji wetu, ahsanteni sana. Yupo na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, mama yetu Mheshimiwa Nchimbi. *(Makofi)*

Vilevile yupo Mwenyekiti wa Bodi ya *CHC* na yeye nadhani yupo asimame. Tuna Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi; tafadhali naomba asimame alipo. Tunaye

Mkurugenzi Mkuu wa *Tanzania Private Sector Foundation;* ahsante sana. Tuna Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*; naomba usimame, mwenyeji wetu pia; na tuna Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha *St. John's;* naomba usimame, ahsante sana. Halafu kuna Waheshimiwa Mabalozi, wengine niliwataja asubuhi. *If you can all rise together. I couldn't make up your names; please, all the High Commissioners and Ambassadors who are around here* naomba wasimame. *(Makofi)*

Tuna washiriki wa Maendeleo, *General Budget Support Development Partners;* nao wasimame wote. Katibu Mtendaji Tume ya Mipango na wasaidizi wake wasimame walipo. Kuna Wakuu wa Taasisi za Elimu ya Juu Dodoma; naomba wasimame walipo. Tuna Wakuu wa Mashirika ya Mifuko ya Jamii Tanzania nao walipo wasimame; ahsante sana. Kuna Wakuu wa Wilaya katika Mkoa wa Dodoma wasimame walipo. Kuna Mwenyekiti wa TUGHE Taifa na Viongozi wenzake wasimame nao walipo; ahsante sana. Kuna Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dodoma; naomba Viongozi wetu wasimame kama wapo. Kuna Maafisa kutoka Wizara ya Fedha; ndiyo hawa niliowapongeza. Kuna Waandishi wa Habari walioalikwa rasmi wasimame tuwaone maana hawa ndiyo wadau wetu. *(Makofi)*

Kuna Maafisa wa Dawati wa Wizara Bungeni, yaani kila Wizara ina Afisa Dawati wa Bunge, nao wasimame walipo sijui mko wapi! Pia tuna wahisani 17 wa Program*u* ya Nne ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wakiongozwa na Bwana Jimmy Haridey na Nick Haiton, ambao ni Wenyeviti; karibuni sana. Siwezi kutaja kila aliyeko hapa, naomba niseme wote tunawashukuru kwa kuja kutusikiliza. Kwetu sisi ni hatua kubwa sana ya mzunguko wetu wa bajeti hii tuliofikia na wengine tutaendelea kuzungumza nao kufanya tathmini ya utaratibu huu.

Pamoja na hayo, nina matangazo machache kwa Waheshimiwa Wabunge; kuna wale waliokaribishwa kwa ajili ya Sumbawanga Ng'ara, ilikuwa wakutane saa saba

lakini mgeni wao Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa na shughuli ya *Cabinet.* Kwa hiyo, hawakukutana lakini anaomba wakutane baada ya kuahirisha hiki kikao, wakutane Dodoma *Hotel;* wale waliopata mwaliko wa Sumbawanga Ng'ara kuzindua kitabu.

Kesho wale wa *APNAC,* Mkutano wa *APNAC* wa kupambana na mambo ya rushwa, utaanza kesho saa tatu asubuhi. Kwa hiyo, muwahi itakuwa *African Dreams Conference Centre* na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na atafika saa hiyo.

Tulikuwa tumeeleza kwamba, tutakuwa na tafrija ya kumpongeza Spika Mstaafu, ilikuwa ifanyike tarehe 15, lakini kutokana na matukio ya misiba na vitu kama hivyo, haitawezekana tutangaza tena tarehe nyingine kabla ya kuahirisha kikao hiki.

Mheshimiwa Shah, Mwenyekiti wa Kikundi cha Wabunge Maskauti, anaomba awatangazie Waheshimiwa Wabunge Maskauti wa kikundi hicho kuwa, kesho tarehe 14 kutafanyika kikao cha kikundi hicho saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tutaendelea kujadili Hotuba ya Bajeti Siku ya Jumatatu. Majina ya walioomba kuchangia tunayo, ni vizuri wakajiandaa tuweze kuendelea kama tulivyo sasa hivi. Kwa jioni hii, naomba niwashukuru sana kwa kazi tuliyofanya wiki nzima, kazi ilikuwa ngumu lakini tumeifanya kwa urahisi kwa sababu ya ushirikiano mkubwa tuliokuwa nao. Kwa hiyo, naomba niwatakie *weekend* njema, mkasome tena hiki kitabu vizuri, Jumatatu tuweze kuonana pamoja.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.20 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 17 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*